EAST AFRICANA COLLECTION

# MADA: MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA ZA S.A. MOHAMED

MOSES MATONGO SARARA

(1997)

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya "Master of Arts" katika Chuo Kikuu Cha Nairobi"

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0100567 7

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

# UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote ulimwenguni"

**M.M. SARARA**

(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu".

Mw. Mwenda Mbatiah

Mw. Lisanza Muaka



UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0101010 7

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia Mke wangu Anne Bosibori Matongo na Mtoto wangu Chris Chacha ambao walivumilia umbali wa masafa kati ya Kisumu na Nairobi wakati nilikuwa nikiendelea na masomo yangu. Walinikosa sana lakini walijitolea kunipa moyo wa kuendelea.

Siwezi pia kumsahau ndugu yangu Michael Sarara aliyenipa makazi na msaada wa kifedha mara kwa mara. Si ndugu wote walivyo kama alivyokuwa kwangu. Nyote mnastahili pongezi za dhati na ninasema ahsante sana.

# YALIYOMO

UNGAMO .................................................... (i)

TABARUKU .................................................... (ii)

YALIYOMO .................................................... (iii)

SHUKRANI .................................................... (vi)

SURA YA KWANZA .................................................... 1

1.0. ***UTANGULIZI*** .................................................... 1

1.1. *TATIZO LA UTAFITI* .................................................... 2

1.2 *MADHUMUNI YA TASNIFU* .................................................... 3

1.3. *SABABU ZA KUSHUGHULIKIA TATIZO* .................................................... 4

1.4. *MIPAKA YA TASNIFU* .................................................... 4

1.5. *YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI* .................................................... 5

1.6. ***MSINGI WA NADHARIA*** .................................................... 11

1.7. **NJIA ZA UTATIFI** .................................................... 18

1.8 TANBIHI .................................................... 19

1.9 MARAJELEO .................................................... 20

SURA YA PILI .................................................... 21

2.0. ***UTANGULIZI*** .................................................... 21

2.1. ***JAMII INAYOSAWIRIWA MCHEZONI*** .................................................... 21

2.2. ***MUHTASARI WA HADITHI*** .................................................... 24

2.3. ***MATATIZO YANAYOIKUMBA JAMII*** .................................................... 26

2.4. ***UBEPARI*** . . . . . . . . 28

2.5. *MATABAKA NA MIKINZANO YAKE KATIKA JAMII* . . . . . . . . 35

2.6 ***MAPAMBANO YA KULETA UKOMBOZI*** . . . . . . . . 38

2.7. ***UUNDAJI WA JAMII MPYA*** . . . . . . . . 42

2.8. ***MWANAMKE NA UDHALIMU*** . . . . . . . . 45

2.9. ***HITIMISHO*** . . . . . . . . 47

TANBIHI . . . . . . . . 52

MAREJELEO . . . . . . . . 54

SURA YA TATU . . . . . . . . 55

3.1. *MUHTASARI WA HADITHI YA KIVULI KINAISHI* . . . . . . . . 55

3.2. ***WAKATI NA MATATIZO YA JAMII YA GININGI*** . . . . . . . . 56

3.3. ***UTAWALA WA KIIMLA*** . . . . . . . . 61

3.4. *UFISADI NA UOZO WA JAMII* . . . . . . . . 66

3.5 *ELIMU KWA WANYONGE* . . . . . . . . 69

3.6 HARAKATI ZA UKOMBOZI WA WANYONGE . . . . . . . . 73

3:7 *UJAMAA - MATUMAINI YA KESHO* . . . . . . . . 78

HITIMISHO . . . . . . . . 80

TANBIHI . . . . . . . . 82

MAREJELEO . . . . . . . . 84

SURA YA NNE . . . . . . . . 85

4.0 UTANGULIZI . . . . . . . . 85

4:1 ***MATATIZO YA AMEZIDI NA CHANZO CHAKE*** . . . . . . . . 87

4:2 **UMASKINI** . . . . . . . . . . 88

4:3 **UAJIBIKAJI KAZINI** . . . . . . . . . . 90

4:4 **RUSHWA NA UFISADI KATIKA JAMII** . . . . . . . . . . 92

4:5 **ELIMU KWA JAMII** . . . . . . . . . . 95

4:6 KASUMBA YA KIKOLONI . . . . . . . . . . 97

4:7 HITIMISHO . . . . . . . . . . 99

TANBIHI . . . . . . . . . . 100

MAREJELEO . . . . . . . . . . 101

SURA YA TANO . . . . . . . . . . 102

HITIMISHO . . . . . . . . . . 102

**MAREJELEO** . . . . . . . . . . 109

## SHUKRANI

Nawashukuru sana wasimamizi wangu katika kazi hii Mw. Mwenda Mbatiah na Muaka Lisanza kwa kuniongoza na kunielekeza katika njia inayofaa nilipoendelea na utafiti wangu. Kazi hii haingekamilika bila msaada wao kwani walinielewa sio tu katika shida zangu za usomi bali pia za kinyumbani. Ni wahadhiri wachache sana wanaotaka kusikia hali ya mwanafunzi inaendeleaje katika jamii yake.

Aidha nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na lugha za Kiafrika hasa wale waliopata kutufunza darasani kama vile Mw. Mosoti, Mw. Mgullu, Mw. Wasike na Mw. Kinene. Tulifaidika kwa mwongozo walioutoa katika mijadala yetu darasani.

Namshukuru pia mkuu wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika Daktari Nyombe kwa msaada wake na juhudi zake mbali mbali za kuhakikisha kuwa masomo yangu yaliendeshwa barabara.

Siwezi na siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu, Iribe wa Mwangi, Moseti 'Bro' Obuchi, Musyoka wa Mwangangi na Ndungu wa Njuguna kwa kunitia moyo katika kazi yangu. Katika mijadala yetu, tulitofautiana na kukubaliana bila ya kukosana. Tulichukuliana mizigo kwa upendo.

Mwisho namshukuru sana Bi. Janet Ochieng kwa kukubali kuipiga chapa kazi hii. Wengi waliteta eti Kiswahili ni kigumu lakini yeye alijitolea muhanga na kuhakikisha kuwa kazi hii imekuwa tayari kwa wakati ilipotakiwa.

Kwa wote niliowataja na wale ambao nafasi haikuniruhusu, nasema tena shukrani.

# SURA YA KWANZA

## 1.0. *UTANGULIZI*

Said Ahmed Mohamed amepata kuandika riwaya kadhaa na vitabu viwili vya mashairi. Maandishi yake yamepata kusomwa kwa wingi na masomaji hapa Afrika Mashariki na kwingineko. Lakini hivi karibuni, pamoja na kuandika riwaya na mashairi, sasa ameingilia uwanja wa drama na kuanzia mwaka wa 1988 hadi sasa, ameandika tamthilia tatu - Pungwa (1988) Kivuli Kinaishi (1990) na Amezidi (1995).

Hadi sasa, unapomtaja S.A. Mohamed, watu wanakumbuka tu riwaya na mashairi yake na si wengi wanaojua kuwa amepata kuandika tamthilia kadhaa. Hata wale walio na habari, si wote ambao wamezisoma hizi tamthilia.

Swali tunalojiuliza ni je, amesema nini katika tamthilia hizi na yana maana gani kwetu kama jamii? Hii ndiyo sababu tukachagua somo la maudhui ili kuona maswala muhimu anayoyajadili na yana uzito gani katika jamii zetu.

Kama tungelikuwa na wakati wa kutosha, tungelipenda sana kujua iwapo yale aliyoyazua katika tamthilia zake yana tofauti yoyote na yale aliyoyasema katika riwaya na mashairi yake. Lakini kwa ajili ya wakati, hatutatekeleza lengo hilo. Aidha kulijibu swali kuwa ni kwa nini aamue kuandika tamthilia sasa ni swali muhimu lakini linalohitaji tasnifu nyingine.

Kwa hivyo, sisi tutahakiki tamthilia za S.A. Mohamed kimaudhui na kuona yale yanayotufaidi sisi kama wanajamii na tutamhakiki kwa misingi ya nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti. Iwapo tutatofautiana na mhakiki mwingine kuhusiana na kazi hizi, basi sababu kubwa itakuwa ni nadharia tulizozitumia.

Sisi katika tasnifu yetu tutajishughulisha zaidi na matatizo yanayotokea katika jamii, chanzo cha matatizo hayo, harakati za kuibadilisha hali hiyo na jamii mpya inayotarajiwa kutokana na

mageuzi hayo.

## 1.1. *TATIZO LA UTAFITI*

Tasnifu hii inakusudia kuchunguza jinsi ambavyo Said Ahmed Mohamed anayashughulikia na kuyajadili maswala ya kijamii katika tamthilia zake tatu. Tamthilia zenyewe ni Pungwa (1988), Kivuli Kinaishi (1990) na Amezidi (1995).

Wengi wa wale waliozihakiki na kuzichambua kazi za S.A. Mohamed wamejikita katika riwaya na mashairi yake na kufikia sasa hakuna aliyefanya uhakiki wa kina kwa kuangalia tamthilia zake kwa pamoja ili kujitokeza na maoni muhimu yanayopatikana katika tamthili hizi. Kwa hivyo, tasnifu hii inanuia kuliziba pengo lililopo katika kazi zake za tamthilia kimaudhui.

## 1.2 *MADHUMUNI YA TASNIFU*

Madhumuni ya tasnifu hii ni kuyafafanua na kuyaweka wazi mawazo mazito na muhimu yanayoikumba Jamii ambayo yanajitokeza katika tamthilia zake. Mwandishi yeyote hajiandikii mwenyewe bali huwaandikia wanajamii ambao wanapaswa kuelimika na kufaidika kwa njia moja au nyingine. Mwandishi huwa amekusudia wanajamii wachukuwe hatua fulani baada ya kuamshwa na kazi zake.

Hata hivyo, sio wanajamii wote watakaokuwa na uwezo wa kuyasoma na kuyalewa yote anayosema mwandishi wazi wazi kwani mwandishi huenda asiyaseme yote wazi wazi kutokana na uoga wa kukabiliana na wale wasiopendelea maoni yake na wana nguvu za kumzima. Hapa ndipo mhakiki huwa ni kiungo maalum cha kumfasiria msomaji ili aone mambo kwa uwazi zaidi na pia apate undani wa yale ambayo hakuyaelewa aliposoma hapo awali.

Kwa hivyo, ni madhumuni yetu kuzihakiki kimaudhui tamthilia za Said Ahmed Mohamed ili kufafanua maana na ujumbe aliokusudia uwafikie wasomaji wake.

## 1.3. *SABABU ZA KUSHUGHULIKIA TATIZO*

Kama tulivyoona katika sehemu ya tatizo la utafiti, tamthilia za Said Ahmed Mohamed hazichashughulikiwa vilivyo na wahakiki na wachambuzi waliotangulia. Kwa hivyo, tuliona kuwa kunayo sababu ya kuliziba pengo hili la kutokuwepo tahakiki za kazi hizi na hivyo kutoa mchango katika kukuza taalum ya uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

Aidha, matatizo anayoyashughulikia katika tamthilia zake yanapatikana ulimwenguni kote mbali na nchi kunakozungumuzwa kiswahili. Kuyamulika kutafanya wasomaji wengi zaidi kuelewa hali ilivyo kadiri Kiswahili kitavyozidi kuenea katika pembe zote za dunia. Maudhui kama vile ukombozi, usawa, elimu kwa jamii, uajibikaji kazini ni mambo yasiyotambua kabila, rangi au jinsia. Yanastahili kushughulikiwa kwa sababu ni ya manufaa kwa jamii kote ulimwenguni.

Uhakiki ni mbinu mojawapo ya kuiendeleza lugha ya Kiswahili mbali na fasihi ya kiswahili. Sisi pia tulionelea kuwa kuna sababu ya kutoa mchango wetu katika kuikuza na kuiendeleza lugha yetu kwani "Titi la mama litamu, jingine halishi hamu.."

Hatimaye, tasnifu hii tunaamini kuwa itatoa changamoto kwa wahakiki na wasomi wengine ili wachambue na kuhakiki zile sehemu nyingine kama vile fani na matumizi ya lugha.

## 1.4. *MIPAKA YA TASNIFU*

Uhakiki wetu ni wa kifasihi na unajikita katika tamthilia. Tumezingatia tamthilia tatu za S.A. Mohamed na hatutahusika na kazi zake za riwaya na mashairi isipokuwa pale zitakapotilia mkazo katika kufafanua maudhui yanayopatikana katika tamthilia zake. Tutayahakiki maudhui bila ya kujiingiza katika fani. Iwapo fani itatajwa, basi itakuwa inahusiana moja kwa moja na jinsi inavyofanikisha maudhui katika kazi hizi.

Maudhui madogo madogo ambayo yanatilia nguvu yale makuu yatajadiliwa chini ya vichwa vya yale makuu na wala hayataangaliwa moja moja.

## 1.5. *YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI*

Katika utafiti wetu, tumegundua kuwa wahakiki wengi waliopata kuzihakiki na ku zichambua kazi za Said Ahmed Mohamed wamejikita katika riwaya na mashairi yake. Katika uchunguzi wetu, tulikumbana na kazi chache mno ambazo zimewahi kuangalia kazi zake za tamthilia.

Mohamed (1990), ambaye ni mwandishi mwenyewe, alitoa makala katika jarida la Mwamko ambapo alijadili matumizi ya lugha katika kazi za fasihi na kugusia tamthilia ya Kivuli Kinaishi ambayo wakati huo ilikuwa bado imo katika hali ya mswada. Tunatofautiana naye kwani sisi tunashughulikia maudhui na yeye alitazama swala la matumizi ya lugha. Hata hivyo, tutafaidika kwayo kwani tutaona jinsi matumizi ya lugha yalivyofanikisha Kuwasilisha ujumbe.

Miriji (1991) aliandika tasnifu yake ya B.A. na kuipatia anwani ya Mtindo Katika Pungwa ni hatua katika kuwasilisha ujumbe. Kama inavyodokezewa katika anwani, yeye aliegemea katika upande wa mtindo na sisi tunayajadili maudhui katika tamthilia zake. Aidha aliweza tu kuangalia tamthilia moja ya Pungwa ihlhali sisi tunajadili zote tatu ili kupata mtazamo mpana zaidi kutokana na uandishi wake wa tamthilia.

Wakati akifanya utafiti wake, tamthilai ya tatu, Amezidi, ilikuwa haijatolewa.

Mbali na hawa, hatukupata uhakiki au uchambuzi wowote unaozihakiki tamthilia za Said Ahmed Mohamed.

Kwa vile tamthilia zake hazijafanyiwa uhakiki wa kutosha, tungelipenda kuangaza kwa kifupi

elementi muhimu za drama ili tuone kama zimefikia kiwango cha tamthilia au ingelifaa abakie kwenye uwanja wa riwaya na mashairi.

Mlama (1983:203) anaeleza kuwa tamthiliya ni sawa na michezo ya kuigiza. Anaendelea:

> **Tamthilia ni utungo wa drama ambayo ni aina moja ya maandishi ya sanaa za maonyesho.**

Kwake, sanaa za maonyesho ina maana ya sanaa ambayo huwasilisha ana kwa ana, tukio fulani kwa hadhira kwa kutumia usanii wa kiutendaji. Kwa hivyo, tamthilia yaweza kuandikwa au isiandikwe bora tu iweze kuwasilisha wazo linalotaka kuwakilishwa mbele ya hadhira.

Hussein (1983:202) anasema kuwa drama iliyoandikwa huishia kwenye fasihi na ile inayoenda jukwaani moja kwa moja bila kuandikwa au kupitia kwenye kitabu, huishia kwenye ulimwengu wa jukwaa.

Drama sisi tutaitumia kwa maana ya maonyesho yoyote ya sanaa yanayoonyeshwa jukwaani yawe ni mashairi, nyimbo au tamthiliya. Tamthiliya kwa upande mwingine ni maonyesho ya sanaa ambayo yanahitaji vitendo na uongeaji wa watu wawili au zaidi.

Katika uandishi wowote wa tamthilia ambayo ni sehemu ya drama, mambo kadhaa huwa ni muhimu katika kuifanikisha kimaudhui na kifani.

Tukimrejelea Hussein (1983:194-202), anatuonyesha Aristotle alivyopendekeza uandishi wa tamthilia ufanywe. Aristotle alitaja mambo sita aliyoyaona kuwa ni muhimu katika uandishi wa tamthilia.

Mwanzo kabisa kulitakiwa kuwe na nyimbo pale mwanzoni kama utangulizi wa mchezo. Aidha, alishauri kutumiwe matamshi yanayofaa na alipendekeza kutumiwe lugha ya Kishairi na yenye mizani badala ya kutumia lugha ya kawaida. Jambo hili lilipata kupingwa na wasomi kama vile Bretcht (1964) ambao waliona kuwa si wasomaji au watazamaji wote ambao wana ujuzi wa kuielewa lugha

hii ya kishairi na kuwa ingelikuwa kizuizi kikubwa cha kuufanya ujumbe ueleweke kwa urahisi.

Alionelea kuwa tamthilia ni sharti iwe na mtiririko wa vitendo hadi kileleni bila ya kukwamakwama njiani. Hapa alipendekeza kuwa mchezo wa kuigiza uwe na mwanzo au utangulizi, kitendo chenyewe kama sehemu ya katikakati na sehemu ya mwisho ambayo alipendelea iwe wimbo.

Sehemu ya nne aliyoiona kuwa ya manufaa ni wahusika. Wahusika hawa alitaka watawaliwe na matendo na wala si wao kuyatawala matendo. Kwa mfano ikiwa mfalme Edipode alitabiriwa kumwuua babake na kisha amuoe mamake, basi ilitokea hivyo hata kama alijaribu kukwepa hili kwa njia zote.

Aliona pia kuwa ni lazima kuwe na fikra au wazo linalomsukuma kuandika tamthilia, isiwe tu ni kuamka na kusema "leo nitaandika tamthilia". Wazo hili ni sharti liwe linatoa funzo kwa jamii ya wakati huo. Hatimaye alisisitiza kuwa utumiaji wa jukwaa ni muhimu katika tamthilia. Aristotle hangelifikiria tamthilia ya kuishia vitabuni tu bila ya kupelekwa jukwaani.

Styan (1960:13) anasema kuwa uandishi wa tamthilia sio tu kuweka watu pale ili waendelee kusemezana. Kunayo tofauti kati ya maneno ya kawaida na maneno ya tamthilia ambayo huwa machache kuliko mazungumuzo ya kawaida, sentensi zake huwa fupi na kukatishwa au kurudiwarudiwa jambo bila sababu maalum haviruhusiwi.

Uumbuji wa maneno na kuendeleza ari iliyoamshwa kwa watazamaji inatarajiwa idumishwe. Uchaguzi wa maneno yanayosemwa na vitendo ni muhimu sana katika kutekeleza hili.

Mbali na mazungumzo ya wahusika, matendo pia hupewa umuhimu mkubwa. Kuhusiana na jambo hili, Mlama (1983:205) anasema kuwa tunalichukua wazo na kuliweka katika hali ya kutendeka, kuwa matendo ndiyo hutoa lile wazo kwani hupewa uhai na kujengwa katika mgongano wa aina fulani. Mgongano ni wa lazima na pasipokuwa na mgongano katika matendo basi tamthilia huwa imekosa

uhai.

Hapa tunatenganisha mazungumzo na matendo kwa ajili ya usomi lakini katika hali halisi kwenye jukwaa, ni vigumu kuyatenganisha haya mawili. Maneno na vitendo yote husaidia katika kuusukuma mchezo mbele, kutoa ujumbe na yote mawili huchaguliwa kwa uangalifu mwingi.

Katika uteuzi wa matendo, mtunzi hana budi kutumia tu yale ambayo yanaendeleza wazo lake na kuachana na mengine yote. Aidha, matendo yake yawe na uwezo wa kuigizwa kwenye jukwaa isiwe kama tamthilia inasomwa au sinema. Hakuna haja ya kuandika tamthilia ambayo haiwezi kufika jukwaani na ambayo haiwezi kuaminika.

Kuna kipengele cha wahusika ambacho ni muhimu katika utunzi wa tamthilia. Mhusika huumbwa na msanii kwa maksudi fulani hata kama yana umuhimu mdogo kiasi kipi. Wahusika hawapachikwi tu pale bali wamejengwa ili kueleza wazo fulani. Wawe katikati ya migogoro kwani ndio wanoendeleza ile migongano katika tamthilia na pia migongano ile inawaathiri kwa sehemu kubwa.

Urefu wa tamthilia ni jambo muhimu kwani mchezo unapokuwa Mrefu sana watu huchoka na hupoteza mtiririko wa hadithi. Mchezo unaondelea kuonyeshwa kwa masaa manane utachosha watazamaji hata kama ni mzuri kiasi gani.

Mchezo ufululize na kutiririka kwa uwazi na bila kupoteza nia ya kwanza ya msanii. Mchezo usiende pole pole sana bila sababu, watu watachoka. Aidha usiende mbio bila sababu, watapoteza mtiririko na kutopata yale yaliyokusudiwa. Kwa hivyo ni heri mchezo utiririke bila kuingiliwa au kuvurugwa na mawazo yasiyooana au matendo yasiyoendeleza mchezo. Hapa sio lazima mchezo uwe sahili ndio uweze kufululiza au kutiririka - waweza kuwa tata lakini utiririke.

Kuteua maudhui unapoandika mchezo huwa ni muhimu sana. Uchaguzi wa maudhui uzingatie umuhimu wa maudhui katika jamii ya wakati huo. Uzito wa yale yanayoteuliwa uwe ni wa jamii nzima.

Hii ni kusema kuwa umma ufikiriwe wakati unapoteua maudhui. Kuhusu jambo hili Brecht (1964:7) anasema

> **"Watu daima wanatushauri tusiandike tu kile ambacho umma unataka lakini hili haliwezekani kwa sababu maandishi yako yanaadhiriwa na kipindi cha wakati unaoishi. Sanaa ambayo haina uhusiano na umma ni upuuzi mtupu. (TY)**

Kulingana na Brecht, uteuzi wa maudhui hauna budi kutawaliwa na hali ya umma wakati huo. Tamthilia si tu kwa ajili ya kuburudisha, kuchekesha na kuchangamsha au kusema tu maneno bali ni njia moja ya kutoa mafunzo, kukosoa, kurekebisha na kutoa mapendekezo.

Brecht pia amekuwa katika mstari wa mbele wa kuonyesha kuwa hadhira (wasomaji au wasikilizaji) ni sharti washirikishwe katika yale yanayotendeka jukwani. Hataki ile hali ya kutafuniwa na kumezewa na waigizaji jukwani. Anapendekeza hadhira ipewe nafasi ya kudadizi na kutafakari mambo yanayotokea kwenye mchezo.

Mhusika atumike tu kuelekeza hadhira katika kufanya uamuzi wao juu ya yale wanayoyaona na wala sio kuwaongoza kwa kila jambo.

Katika jambo hili la hadhira, msanii hana budi kujitambulisha na hadhira anayoiandikia kwa sababu hili litamwezesha kuamua aseme nini na aliseme vipi. Ngugi (1986:103) kwa mfano, anapendekeza kuwa msanii hawezi kuepuka kuunga mkono kundi fulani katika jamii na hivyo kujitambulisha nalo.

Pia mchezo huu upimwe na wasomaji, wahakiki na hadhira sio kwa kuona ni wangapi wamehudhuria au kuinunua tamthilia ile bali ni vipi umewaadhiri na kufanikisha malengo ya mtunzi. Hili ni jambo gumu sana kutekeleza kwani hadi sasa hakuna vipimo maalum vya kulitekeleza.

Hatimaye, udhamini ni muhimu sana unapoandika mchezo. Unaweza ukaandika mchezo na ukakosa wasomaji na hata usifike jukwaani hata kama ni mchezo mzuri. Lazima kuwe na kundi ambalo

litakudhamini au kujitambulisha na maoni yako na hivyo kusaidia katika kuuendeleza mchezo wako.

Kwa hivyo, mbali na Aristotle na mapendekezo yake, tumeona kuwa kuna umuhimu wa kutilia maanani mazungumzo katika tamthilia. Isiwe tu ni kupachika maneno na kuyaita tamthilia. Matendo yateuliwe kulingana na wazo au fikra muhimu. Wahusika wateuliwe kwa uangalifu na waendeleze mchezo kwa kutumia matendo huku matendo yakiwaathiri. Urefu na mtiririko wa tamthilia vitiliwe maanani. Aidha maudhui ni ya lazima, tena ya wakati uliopo. Hadhira ihusishwe na pia msanii ajitambulishe na kundi fulani katika jamii. Kuwe na njia fulani ya kupima mafanikio ya mchezo. Hatimaye kuwe na udhamini.

Hizi basi ndizo elementi muhimu za drama na S.A. Mohamed akiwa ni mwandishi wa hivi majuzi katika uwanja huu, itatubidi tuzipime kazi zake na kuona kama amejimudu kama mwanatamthilia au la.

## 1.6. ***MSINGI WA NADHARIA***

Tumechagua kutumia nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti ambayo ilitokana na uyakinifu. Ili kuielewa nadharia hii barabara, inakuwa muhimu kuangalia historia ya uyakinifu kwa kifupi huku tukiazimia kuonyesha kutoridhisha kwa mawazo ya uyakinifu kulikosababisha kuzuka kwa uyakinifu wa kisoshalisti.

Gitahi (1980:7) anaeleza uyakinifu kama nadharia au mazoea katika sanaa na Fasihi inayohusiana na maumbile au maisha halisi ambayo hujaribu kuonyesha ukweli ulivyo bila kutoa mawazo ya kiutopia. Jambo la kwanza basi ni kuwa nadharia hii inaeleza maisha halisi kisanaa huku ikionyesha ukweli wa jamii ulivyo bila ya kutilia maanani mambo ya kidhahania.

Naye Suchkov (1969:319-320) katika kueleza chimbuko la uyakinifu anasema:

> **Mfumo wa uyakinifu katika sanaa na fasihi ulizuka pale ambapo wanajamii walikumbwa na tatizo la kutaka kuelewa chanzo cha matatizo ya jamii kwa jumla (TY).**

Anaendelea kusema kuwa nadharia hii ilizuka mnano karne ya kumi na nane watu walipoanza kung'amua kuwa mahitaji ya jamii yanatawaliwa na sababu za kiuchumi na wala hayatokani na fikra za watu wala majaaliwa. Mawazo haya yalikuwa kinyume na yale ya awali yaliyotokana na imani za kidini yaliyosisitiza kuwa chochote utakachokumbana nacho kitakuwa tayari kimeshapangwa na hakuna awezaye kukiepuka.

Nadharia hii ya uyakinifu ilijaribu kuonyesha mtu binafsi akiwa na mikinzano ya ndani kwa ndani huku akiishi katika jamii

Halafu ilionyesha mahusiano ya mtu binafsi na jamii nzima kwa jumla. Hapa

mtafaruku mkuu ukawa ni haki ya mtu binafsi huku ikipingana na haki ya jamii nzima. Ikaonyesha pia mitafaruku na mikinzano miongoni mwa wanajamii kwa jumla kama ilivyojitokeza katika kipindi maalum. Mikinzano na mitafaruku hii haikuonyeshwa kwa mujibu wa matabaka katika jamii kama walivyokuja kupendekeza wana-marx baadaye. Mwisho, ilijaribu kuonyesha muundo wa jamii yenyewe bila ya kujishughulisha na chanzo cha matatizo ya jamii hiyo na suluhisho kwa matatizo hayo.

Uyakinifu wa mwamko nao, kama uyakinifu, ulitokea wakati ambapo wanajamii wa kule Ulaya walianza kugundua kuwa maisha si majaaliwa bali hutokana na vitendo mahsusi vyenye asili yake katika jamii. Wakaanza kuuliza na hata kupinga majibu yaliyotolewa, hasa na dini, kama sababu za mambo kuwa yalivyokuwa katika jamii nyakati hizo. Walianza kuieleza jamii walivyoiona bila kutoa sababu zozote za jamaii ile kuwa vile au kutoa mapendekezo yoyote jinsi ingaliweza kubadilishwa. Kazi yake kubwa ikawa kueleza ulimwengu wa kweli kisanaa.

Kutokana na upungufu huo wa kutoa tu maelezo ya jamii ilivyo bila kuonyesha chanzo cha matatizo yaliyokuwepo ikawa ndiyo sababu kubwa ya kusuka uyakinifu wa kiuhakiki.

Uyakinifu wa kiuhakiki ukapiga hatua sio tu kwa kuonyesha jamii ilivyo na matatizo yake bali pia ulionyesha matatizo ya kijamii na kimaadili ya wakati huo lakini bila ya kutoa chanzo cha matatizo hayo na suluhisho ambamo majibu yangelipatikana. Sababu hii ya kutotoa chanzo wala suluhisho kwa matatizo yaliyoikabili jamii ikawa ndiyo sababu ya kuzuka kwa uyakinifu wa kisoshalisti.

Nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti ina uhusiano wa karibu na umarx. Ilianza rasmi tangu mwaka wa 1932 huko Usovieti wakati kikao cha kwanza cha kitaifa

kilipoitishwa ili kutoa mwongozo kwa waandishi wa kisovieti. Kikundi cha kuchunguza, kutayarisha na kutoa mapendekezo kiliundwa. Madhumuni yake yalikuwa ni kutazama kwa makini zaidi kazi iliyokuwa imefanywa wakati huo kuhusiana na maendeleo ya nadharia ya uhakiki wa kifasihi ya Umarx na kutoa mapendekezo ya siku zijajo.

Gorky (hakuna mwaka: 264) ambaye ni mmoja wa wale walioiunga mkono nadharia hii kwa dhati alieleza upungufu wa nadharia ya uyakinifu wa kiuhakiki uliosababisha kuzuka kwa uyakinifu wa kisoshalisti kwa kusema:

> **Wakati ukionyesha matatizo na uozo wa jamii na kumulika maisha na visa vyake, matatizo ya mtu binafsi yakiwa chini ya himaya ya familia, mafunzo ya imani za kidini na sheria dhalimu za nchi, uyakinifu wa kiuhakiki haukuweza kuonyesha jinsi ya kuikata minyororo hii. (TY).**

Anachokisema hapa ni kuwa ingawa jamii ilionyeshwa kama ilivyokuwa na matatizo yake kutambuliwa na kuelezwa, hakukutolewa chanzo cha matatizo hayo wala kutolewa suluhisho au pendekezo la kutatua matatizo hayo.

Mara nyingi iwapo kuna wale waliojaribu kutoa mapendekezo, basi walifanya hivyo kwa kupendekeza mambo ya kiutopia au yale yaliyowasaidia wanyonyaji ili warekebishe makosa yao na waendelelee kunyonya zaidi.

Uyakinifu wa kisoshalisti umepiga hatua moja zaidi kwani mbali na kuiona jamii ilivyo, nadharia hii pia inaonyesha mikinzano iliyoko katika jamii na kuonyesha chanzo chake. Pia hutoa pendekezo la namna ya kutatua matatizo hayo ili kuunda jamii bora. Ili kutekeleza haya, mambo kadhaa ambayo ndiyo uti wa mgongo wa nadharia hii ni sharti yatiliwe maanani.

Kwa mfano, ilipokubaliwa na waandishi wa kisovietu mnamo mwaka wa 1934 ili kutoa mwongozo kwa waandishi wa fasihi wa kisovieti, ilielekea kutilia maswala fulani uzito. Fokema (1977:97) akinukuu kutoka kwa maazimio yaliyopitishwa katika kamati hiyo anasema:

> **Uyakinifu wa kisoshalisti ambao ndio msingi wa fasihi ya kisovieti na uhakiki wake unahitaji kusema ukweli, kutoa matukio halisi kihistoria na namna jamii ilivyoendelea kimapinduzi. Na kwa wakati huo huo ukweli na historia viambatanishwe na itikadi na elimu ya wafanya kazi katika moyo wa kijamaa (TY).**

Mambo kadhaa yanajitokeza hapa. Kwanza, mwandishi ni sharti aseme ukweli ulivyo katika jamii kwa kuonyesha hali halisi ilivyo bila kuficha wala kupendelea popote. Kipindi maalum kionyeshwa kwa misingi ya historia. Jamii ya sasa ielezwe kwa kurudi nyuma na kuona jinsi ilivyofika pale ilipo sasa huku sababu za kuifanya iwe vile ilivyo zitolewe katika historia.

Katika kutoa matukio halisi kihistoria, msanii hana budi kuonyesha jamii hiyo ilivyopiga hatua kimapinduzi. Marx na Engeles (1963:42) waliamini kuwa kutokana na sababu za kiuchumi, hutokea matabaka ambapo tabaka moja huhodhi nyenzo zote za uzalishaji mali hivyo kulifanya liwe na nguvu na uwezo mwingi kiuchumi. Hili huwa ni la wachache katika jamii lakini wenye uwezo kifedha. Kwa upande mwingine, kuna tabaka la chini ambalo ndilo la wengi wasiomiliki chochote ila jasho lao na nguvu zao ambazo wanaziuza kwa wenye mali ili wakidhi mahitaji yao. Hili ni tabaka la wanyonge kifedha, walio wengi lakini wasio na nguvu. Daima, matabaka haya huwa na mitafaruku, mikinzano na migongano katika jamii huku wagandamizwaji wakijizatiti ili kutwaa na kumiliki nyenzo za uzalishaji mali na walio na mali na wakandamizaji wanatumia ukatili, vitisho na ulaghai ili kuendelea kuhodhi mali ile.

Kwa hivyo, mwandishi aonyeshe matabaka haya na mikinzano na mitafaruku hii ilianzaje na kuendelea kihistoria. Jamii haibaki wima bali daima imo kwenye mabadiliko kufuatia sheria za kiupembuzi na shughuli za kimapinduzi. Aonyeshe mabadiliko yaliotokea kimapinduzi. Aonyeshe pia kuelewa kwake kwamba mabadiliko ya kijami hufuata kanuni au sheria za kiuchumi kwani ndicho kipengele muhimu kinachotawala mahusiano yote katika jamii, yawe ni ya kisiasa, kitamaduni, kiitikadi, na mifumo yote ya kijamii kwa jumla.

Itikadi na elimu ya wafanyakazi vinatiliwa mkazo kwani hili ni muhimu ili kuwazindua na kuwahimiza watende jambo kwa ajili ya kuleta mabadiliko mema.

Mwandishi anao wajibu wa kujiona kama mwalimu wa jamii. Atumie fursa yake kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na wanajamii wanaoonewa kwa kuwafungua macho ili waitambue fasihi potovu inayowapovusha macho. Msanii hawezi kuepuka kujitambulisha na kundi moja analoliunga mkono, na kwa mujibu wa nadharia hii, ni wale walio wengi na wenye kukandamizwa. Yale anayowafundisha yatilie mkazo matatizo na chanzo cha matatizo hayo katika jamii. Aidha, aonyeshe uwezo wa mwanadamu wa kujikwamua na matatizo hayo kwa mujibu wa kuiboresha hali yake. Maandishi ya kujisikitikia na kukata tamaa hayana nafasi katika nadharia hii. Wajue kuwa wana jukumu la kutekeleza katika mapinduzi au mabadiliko haya ya kuleta ujamaa, mwandishi anapaswa kuonyesha matumaini ya kesho katika kazi zake. Jamii ya kesho inayojitokeza ionyeshe matumaini kwa kufuata misingi ya kijamaa ambapo ubepari utakuwa umeng'olewa na haki na usawa kutapakaa jamii nzima; iwe ni jamii yenye haki, usawa, utu na matumaini mema.

Ngara (1985:16) anatoa muhtasari wa teneti muhimu za nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti. Anasema:-

**Uyakinifu wa kisoshalisti hupendekeza kuwa maisha ni vitendo, na uundaji kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa binadamu kwa kuzingatia uwezo wake wa kuyashinda mazingira. Inatangaza furaha ya kileleni hapa duniani ambayo binadamu anajaribu kuitekeleza kwa kujaribu kuwafaidi wote waliounganishwa na kuwa jamii moja (TY).**

Anasema kuwa moja ya sifa muhimu za nadharia hii ni kuwa ina mtazamo na muelekeo wa maisha ya kesho, ambapo jamii yenye furaha, ufanisi na ya kijamaa itajengwa. Kwa hivyo, Fasihi inayojengwa kwa misingi ya nadharia hii inatazamiwa kuonyesha uhalisia katika jamii kupitia mtazamo wa Umarx.

Mitafaruku ya matabaka ionyeshwe kihistoria hadi leo. Kisha ionyeshe na kueneza matumaini ya ujamaa.

Katika kuonyesha mikinzano ya matabaka, mwandishi ajitambulishe na wafanyakazi!. Mabadiliko au mapinduzi yaonyeshwe kihistoria hadi sasa na yanavyotarajiwa kuelekea kesho. Usawa, haki na ushirikiano wa umma vitiliwe mkazo.

Hii basi ndiyo nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti, inayopendekeza jamii ionyeshwe ilivyo na matatizo yake, chanzo cha matatizo hayo na jinsi ya kuyatatua. Imulike jamii ile kimatabaka huku ikionyesha namna shughuli za mapinduzi zilivyoendelea hadi sasa na kutoa muelekeo wa kesho. Katika kufanya hivi, mwandishi wa Fasihi ajitambulishe na wengi wanaonyanyaswa. Hatimaye aweze kuona jamii ya kesho yenye matumaini, usawa, haki na ushirikiano - jamii ya ujamaa ambapo mali ni kwa faida ya wote na wala si wachache.

Kwa hivyo, tutazihakiki tamthilia za Said Ahmed Mohamed na kuona iwapo ameonyesha jamii ilivyo huku akiangaza matatizo na chanzo cha matatizo hayo. Tutaona pia iwapo ameyaonyesha matabaka na migogoro yake katika jamii kihistoria

hadi sasa na iwapo amejitambulisha na kundi moja katika jamii.

Tutazipima kazi zile kwa kuona kama ametoa elimu kwa kundi analolitetea.

Hatimaye, tutajadili iwapo ametoa jamii bora na yenye usawa katika kazi zake - jamii yenye usawa, utu na matumaini mema.

## 1.7. NJIA ZA UTATIFI

Utafiti wetu utakuwa wa maktabani. Tutazisoma tamthilia za mwandishi na kazi zake nyingine ili kupata mtazamo wake kiitikadi. Pia tutasoma kazi za wale waliotangulia kuhakiki tamthilia zake na kupata maoni yao. Aidha, tutasoma makala na vitabu mbali mbali vinavyohusiana na drama kwani kazi tunazozihakiki ni kazi za drama.

## 1.8 TANBIHI


Mlama, P.O., 1983 — "Utunzi wa tamthiliya katika mazingira ya Tanzania" katika Fasihi III Makala Za Semina, UK. 203

Hussein, E., 1983: — "Hatua mbalimbali za kubuni na kutunga tamthilia kufuatana na misingi ya Ki-Aristotle" Katika Fasihi III, Makala Za Semina UK.194

Kama nambari 2 hapo juu.
UK 194-202

4Styan, J.L., 1960 — The Elements of Drama, Cambridge University Press, UK.13

Kama nambari 1 hapo juu:
UK.205

Brecht, B., 1964: — Brecht on Theatre (Kilitafrisiriwawa na willett,J) Shenval Press, London UK.7

Ngugi Wa Thiongo 1986 — "Writing against new colonialism" katika Kristen, H (Mhariri); Criticism and Ideology, second African writers' conference, stockhom UK. 103.

Gitahi, G., (1980): — The Development of a Writers Social Perspective; An Assessment of Ngugi Wa Thiongo's Selected Texts, M.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi UK.7

Suchkov, B., (1969): — "Realism And Its Historical Development" Katika Prof. S. Mozhnyagen (mhariri), Problems of Modern Aesthetics, Progress Publishers, Moscow, UK. 319-320

Gorky, M., (Hakuna mwaka): — On Literature, Progress Publishers, Moscow UK. 264.

Fokkema, D.W., (1979): — Theories of Literature In The Twenthieth Century, C. Hurst & Co., London.

Ngara, E., 1985: — Art and Ideology in the African Novel, Heinman, Nairobi UK.16...

## 1.9 MARAJELEO


Beard na Verma, 1981: Katika Judith, B. (Mhariri) "Doing your research project" A Guide For First Time Researcher in Education and Social Sciences, Milton Keynes, Philadephia open University press, Philadephia.

Brecht, B., 1964: Brecht on Theatre (Kilitafriswa na willett,J) Shenval Press, London.

Fokkema, D.W., (1977): Theories of Literature In The Twenthieth Century, C. Hurst & Co., London.

Gitahi, G., (1980): The Development of a Writers Social Perspective; An Assessment of Ngugi Wa Thiongo's Selected Texts, M.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi

Gorky, M., (Hakuna mwaka): On Literature, Progress Publishers, Moscow.

Hussein, E., 1983: "Hatua mbalimbali za kubuni na kutunga tamthilia kufuatana na misingi ya Ki-Aristotle" Katika Fasihi III, Makala Za Semina Dar-es-salaam

Minji, t., 1991: Mtindo Katika Pungwa ni Hatua katika kuwazilisha ujumbe, B.A. chuo cha Nairobi kitivo cha elimu, Kikuyu.

Mlama, P.O., 1983: "Utunzi wa tamthiliya katika mazingira ya Tanzania" katika Fasihi III Makala Za Semina, Dar-es-salaam

Mohamed S.A. 1988: Pungwa, Longman Kenya Ltd, Nairobi

\- 1990:Kivuli Kinaishi Oxford University Press, Nairobi

\- 1990:"Ulimwengu wa Mwandishi wa Kiswahili kilugha" Katika mbatian, M., (Mhariri) Mwamko nambari tatu

\- 1995:Amezidi, East African Educational Publishers, Nairobi.

Ngara, E., 1985: Art and Ideology in the African Novel, Heinman, Nairobi.

Ngugi Wa Thiongo 1986: "Writing against neo-colonialism" katika Kristen, H (Mhariri); Criticism and Ideology, African writers conference Bolushaningens,stockhom

Suchkov, B., (1969): "Realism And Its Historical Development" Katika Prof. S. Mozhnyagen (mhariri), Problems of Modern Aesthetics, Moscow,

Styan, J.L., 1960: The Elements of Drama, Cambridge University Press, cambridge

# SURA YA PILI

## 2.0. *UTANGULIZI*

Katika sura hii, tutachambua na kujadili maudhui yote makuu yanayopatikana katika tamthilia ya Pungwa ambayo ni tamthilia ya kwanza ya mwandishi iliyochapishwa mwaka wa 1988. Kisha tutatoa maoni ya kijumla kuhusu maudhui hayo na kazi yenyewe kama hitimisho la sura hii.

## 2.1. *JAMII INAYOSAWIRIWA MCHEZONI*

Kama tulivyoona katika sehemu ya nadharia, msanii anayeandika kwa misingi ya nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti ni sharti aonyeshe ni jamii ya wakati upi anayoizungumzia katika kazi yake ya sanaa.

Jamii inayozungumziwa katika mchezo wa Pungwa ni jamii iliyokwisha kujitawala baada ya kupata uhuru wa bendera na wimbo wa taifa. Jambo hili linathibitishwa kupita kwa sauti ya mzuka ambayo inadokezea kuwa huyu mzuka haonekani machoni mwetu lakini ako karibu ingawa pia ako mbali.. Aliondoka na kumbe bado yupo. Hii inadhihirisha kuwepo kwa ubepari na ukoloni mambololeo hata kama ukoloni mkongwe uliondoka.

Utumiaji wa sauti ni mbinu ya uandishi wa drama na mwandishi ameitumia ili kuonyesha ile hali ya kufumbwa macho na kufikiri kuwa tuna uhuru na kumbe kuna wale wanaotutawala kupitia mlango wa nyuma. Hatuwezi kuwaona ila tu kuhisi na kusikia sauti zao au maoni yao ambayo kwa hakika ndiyo yanayotawala. Mzuka nalo limetumika hapa kimajazi kwani mzuka ni aina ya pepo au shetani na linawakilisha hawa mabepari na wakoloni ambao huwezi kuwaona ila kuwahisi na kusikia sauti zao. Ni mizuka tu ambao wanaweza kuwa na tabia kama hizi na neno hili ni uteuzi mwafaka. Tunakumbushwa hapa ule mchezo wa Hussein (1971) aliouita Mashetani. Mashetani walitumika kimajazi kusimamia ukoloni na ukoloni mamboleo.

Ingawa jamii inayozungumziwa hapa ni jamii ya kiafrika, mwandishi anatahadharisha kuwa huu si mchezo wa mahali pamoja. Katika dibaji yake anatueleza:-

**Inaelekea kwamba mila na desturi hizi za Pungwa Ziko sehemu nyingi Afrika na Asia - na pengine dunia nzima. Hata zile nchi ambazo twaambiwa zimeendelea pungwa haijapotea kabisa, ingawa kila jamii ina mbinu zake za pungwa, tofauti na zile za jamii nyingine.(Hakuna ukurasa).**

Kwa hivyo huu mchezo wa pungwa ni mchezo wa sehemu zote ulimwenguni - Afrika, Asia na hata nchi za kimagharibi. Mradi iwe ni nchi inayoendelezwa kwa misingi ya ubepari na unyonyaji, basi hii shughuli ya kuwapunga hawa mashetani wakatili, walaghai na wanyonyaji itaendelea. Kwa vile ubepari hauna mipaka, mwandishi naye hakutaka kuiwekea mipaka tamthilia yake kwani matatizo yanayotokana na ubepari na ukolonii mamboleo ni yale yale na hayatambui mipaka.

Nchi nyingi za ulimwengu zilizokuwa chini ya utawala wa ukoloni zilipoanza kupata uhuru, kulikuwa na hali ya matumaini makubwa ya kuona siku bora katika maisha ya usoni. Wananchi walifurahi kuwa muradi sasa ni "wenzetu" walio madarakani na wala sio weupe, bila shaka watawakumbuka. Lakini haikupita muda kabla ya ukweli kudhihirika na uongo kujitenga. Wale walioshika hatamu za uongozi walidhamiria kujinufahisha wao wenyewe na aila zao.

Viongozi hawa, wakishirikiana na mabepari wa ng'ambo, walianza kupora mali ya taifa na kuihamisha hadi banki za ng'ambo na kuiweka huko. Matokeo yakawa ni ufukara kwa walio wengi na ambao ndio hutoa jasho wanapozalisha mali ile.

Ngugi (1986:96) anasema kuwa kipindi hiki cha uhuru kilitoa viongozi wapya ambao waliunda tabaka jipya katika jamii huru ambao kwa hakika halikutofautiana na lile la wakoloni. Kilichokua tofauti ni ngozi; palipokuwa na mtu mweupe sasa pakatwaliwa na mweusi bali matendo yakabakia yale yale.

Tawala hizi mpya katika mataifa huru zikawa zinabanwa kutoka nje na ndani mwa nchi.

Kutoka nje ikawa ni mataifa ya kimagharibi, mengi yao yakiwa ni wakoloni wa zamani, yalitaka serikali mpya zifuate maagizo na masharti kwa ajili ya kuangalia maslahi yao. Aidha, walifinywa kutoka ndani na wanachi waliong'amua kuwa uhuru haukuwaletea nafuu kwa kuwaondolea ufukara na kuwa ukatili uliendelezwa na kuzidishwa dhidi yao. Wakashuhudia uporaji wa hali ya juu wa mali ya taifa na walipofungua midomo yao kwa nia ya kuteta, polisi wakaachiiliwa dhidi yao kwa virungu na buti zao.

Jamii, kupitia kwa waandishi wa magazeti, Fasihi, wanasiasa wazalendo na walimu pamoja na wanafunzi katika vyuo vikuu wakaanza kupiga makelele dhidi ya usaliti huu. Wengi wao wakanyamazishwa ama kwa kutiwa kizuizini au kwa kuuawa kinyama ili wawe onyo kwa wengine wenye tabia kama yao.

Kutokana na kutokuwepo usawa katika jamii kama tulivyoona hapo awali, wengi wa viongozi waporaji na wezi wa mali ya umma wakaanza kuhamisha pesa walizoziiba na kwenda kuziweka katika mabenki ya Ulaya huku wenzao wakihasirika na kufa kwa njaa na umaskini mwingi. Tendo hili linadhihirisha uoga wao kuwa siku moja walio wengi watakuja kudai haki zao na kuwanyang'anya na kuirejesha mali waliyowaibia. Hivyo, huzikimbiza na kwenda kuzificha katika mabenki ya siri huko Uswizi na nchi nyinginezo. Fauka ya hayo, tamaa yao kuu ya kutaka kulundika zaidi na zaidi huwafanya wapeleke raslimali zao kule ng'ambo kwani faida inayolipwa na mabenki kule ni ya juu na hivyo utajiri wao utazidi kuongezeka zaidi na zaidi.

Kwa hivyo, tamthilia ya Pungwa pamoja na zile nyingine mbili, zimejengeka katika hali kama hii ambapo jamii imejipatia uhuru lakini badala ya matunda ya uhuru kugawanywa kwa usawa, ni wachache ndio wanaofaidika huku wakishirikiana na mabepari kutoka nje ya nchi. Wanaojaribu kuipinga hali hii wanadidimizwa, kuangamizwa na kuzikwa kabisa. Ni jamii iliyo huru lakini iliyojaa wizi, uporaji na ukatili mwingi. Ni jamii yenye maadui wawili - mabepari mchwara (wa ndani mwa nchi) na wale wa nje.

## 2.2. *MUHTASARI WA HADITHI*

Tamthilia ya Pungwa ni juu ya familia ya mtu na mkewe ambao ni watu wenye mali, madaraka, uwezo na watumishi nyumbani.

Mchezo unapoanza, tunawaona Bwana na Bibiye wakiwa wamelala katika chumba cha kulala ambacho mwandishi anakiita "fahari ya chumba" na kitanda wanachokilalia kinasimuliwa kama "tanda la kujimwaya kwa usingizi mnono wa raha". Hali tunayochorewa hapa ni ya watu waliopata chao na wanaishi kwa raha na uluwa. Hata hivyo, kinyume na tunavyotayarijia kwamba watapata usingizi wa raha kutokana na chumba chao cha fahari na tanda lao la kujimwaya, tunaona Bwana akigutuka usingizini huku amejawa na ndoto za ajabu sizizompa raha hata kidogo.

Tunagundua baadaye kuwa Bwana anaumwa kutokana na maradhi ya kuugua akili na anahitaji matibabu. Mwandishi anauita ugonjwa huu kuwa ni ugonjwa wa kishetani na unahitaji tiba. Anakunywa dawa za kizungu lakini hasifai chochote. Ndipo Bibiye anaamua kumwita mganga wa kienyeji.

Mganga wa kienyeji (Mahoka) anapofika, anamuagua kwa kusema kuwa Mgonjwa ana shetani lakini anashindwa kumtibu kwa sababu anatumia ngoma na maneno tu - mambo ambayo hayafui dafu mbele ya shetani.

Mambo yanazidi na Bibiye anaamua kumwita Mzee Burhari ambaye ni mganga na mnajimu anayeagua na kutabiri kwa kutumia elimu ya nyota. Baada ya kupiga ramli anautambua ugonjwa wake kuwa ni pepo anayeitwa Mfakamizi ambaye hula shaba, chuma, makaa, dhahabu, almasi, kahawa, karafuu, katani na vinginevyo. Anashauri kuwa tiba tu ya Bwana ni kupungwa ndiko kutakakomletea nafuu. Bwana naye anakataa kupungwa kwa sababu ya masharti ya tiba yanayotolewa. Masharti haya yanakuwa magumu kwa Bwana kwani yanaashiria mabadiliko ambayo yatamhitaji awache kutenda aliyozoea kutenda. Anatakiwa

afunge asile kitu kwa siku saba, avae matambara kwa siku saba kila mtu amwone, apigwe kindumbwendumbwe apite akichezwa shere mitaani kwa siku saba, arejeshe kila anachodaiwa kwa milioni wanaomdai na aache kukaa bure, awe anatoa jasho lake ili ale kwa kutumia jasho lake. Huu ni mwito wa kumtaka awachane na unyang'anyi wake na badala yake ajipatie riziki yake kwa kutoa jasho lake.

Kama ilivyotarajiwa, anaukataa uaguzi huu na kuupinga kwa hali na mali. Ingawa mzee Burhani anatoa uaguzi wa kweli na kutoa mapendekezo ya kumtibu anashindwa kumtibu hasa kwani pepo wa Bwana ni mkubwa na mwenye nguvu zaidi. Badala yake, Burhani anaamua kushirikiana naye na sasa Bwana anaamua kumlisha, kumvisha, na kumneemesha kwa utajiri wake na kumpa utajiri wa kiwango cha nchi hiyo ili anyamaze.

Inaishia kinyume kuwa mganga anapungwa na shetani badala ya shetani kupungwa na mganga.

Hatua ya mwisho ya kumpunga na kumtibu ni ile ya simba na kikosi chake ambacho ni mkusanyiko wa mafukara wasio na kazi, watumishi, walinzi na watamba -na-njia na vifaa vyao vya kupungia si maneno na ngoma bali ni marungu, singa na silaha nyinginezo, umoja wao na vifaa vyao. Anakubali kucheza ngoma wanoicheza lakini kwanza ni lazima atolewe mashetani wake kichwani kwanza. Baada ya kuondolewa mashetani anaadhibiwa kwa mkwaju kwa minajili ya kurekebisha tabia yake na mchezo unamalizikia hapo kwa wimbo.

Hii basi ndiyo hadithi inyopatikana katika tamthilia ya <u>Pungwa.</u>

## 2.3. *MATATIZO YANAYOIKUMBA JAMII*

Wanaotumia nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti kama tulivyoona, hupendekeza kuwa matatizo ya jamii ni lazima yaelezwe yalivyo bila ya kuuficha ukweli. Chanzo cha matatizo haya pia ni sharti kifuatiliwe kihistoria na kuona yalianzaje hadi kufikia hivi leo. Moja ya matatizo haya ni umaskini.

Tatizo la umaskini limeenea nchini kote. Kuna umaskini mwingi ambao unaathiri makundi mbalimbali katika jamii. Makundi haya yanayoogelea kwenye lindi la umaskini ni kama vile walinzi, watumishi wa nyumbani (Mwantabu, Kibwege na Kijuha), Mahoka, Mzee Burhari, na Simba na kundi lake.

Walinzi wanafanya juhudi za kuilinda mali ya Bwana na maisha yake lakini hawafaidiki na chochote isipokuwa mshahara mdogo usioweza kuwaondolea matatizo yao. Watakuwa walinzi hadi siku watakapoacha kazi na waende kujifia nyumbani kwao. Ile mali wanayoilinda punde itasafirishwa hadi Ulaya na haitawafaidi chochote. Hawana habari kuwa yule wanayelinda mali kwa niaba yake ni mwizi, tena mwizi wa mali yao wenyewe ambayo wameitolea jasho.

Watumishi wa nyumbani nao wanazidi kutumika kipunda huku hali zao zikizorota kiuchumi. Wanadharauliwa na kutukanwa bila kupewa heshima yoyote ilhali wao ndio hufanya kazi ya kuwastarehesha Bibiye na Bwana.

Iwapo wataendelea kutii na kutumikia Bwana na Bibiye na kulipwa kimshahara wanachopokea basi hali yao ya umaskini itazidi kuendelea.

Mahoka na Mzee Burhani ambao hupiga makelele dhidi ya maonevu na unyonyaji ni maskini ambao wakipatiwa kitu kidogo wanafunga midomo yao na kuendelea kushirikiana na wanyonyaji. Ukata ndio shida yao na wakipata fursa ya kujiendeleza basi hunyamaza kimya kama Mahoka alivyosema kuwa maskini hana kinyongo na anaweza kufanya lolote mradi tu atalipwa. Mzee Burhani naye ananunuliwa kwa mapesa ya Bwana na kuwekwa "mfukoni" hivi kwamba kelele zake zimekoma na hasizikiki tena. Mwenyewe anaitikia kuwa akichukuliwa

katika utajiri, kelele zake za uaguzi zitakoma.

Nacho kile kikundi kinachoongozwa na Simba kinadhihirisha umaskini wake kwani kimevaa magwanda na hata hakimudu viatu mguuni bali kikundi chote kinakanyaga chini.

Pupa na ubinafsi ni tatizo jingine linaloikumba jamii katika tamthilia ya Pungwa. Pupa ya kupata mali na kutajirika haraka limekuwa tatizo kubwa kwa viongozi na wengine wenye fursa ya kujitajirisha kwa haraka. Bwana ana vitabu vya akiba katika nchi za nje kama vile Geneva ambacho kina dola elfu mia moja; Paris franc elfu mia mbili, mia sita na sabini;.
Ujapani Yen milioni mia tatu; cha Ujerumani Magharibi kina Deustch Mark elfu mia tano na cha U.S.A. kina dolla elfu mia tatu. Huu ni utajiri mkubwa sana kwa familia moja. Pamoja na haya, nyumba yao imepambwa kwa kila aina ya vitu kutoka nga'mbo: Kanzu kutoka Marekani; viatu kutoka Italia, Manukato kutoka Paris, Kila gari inayoingia, Televisheni na video kila aina mpya. Wana kasri na chumba chao cha kulala ni chumba cha fahari na tanda lao ni tanda la kujimwaya. Yote haya Bwana anayafanya kwa ajili yake na Jamii yake tu. Kwa hakika hawahitaji haya yote ili kujikimu mahitaji yao. Ni ulafi, uroho na ubinafsi tu ndivyo vinavyowasumbua.

Bibi naye anajishughulisha na miradi mingine kama vile kufuga kuku wa mayai na wa nyama, ngo'mbe wa maziwa na wa nyama, mbuzi na kondoo; wote kwa ajili ya faida yake. Bado hawajatosheka bali Bwana anawadai wengi shilingi laki tano, ana nyumba za kukodisha, amenunua "shares" au hisa katika makampuni mbalimbali, na ana ushirika wa kusafirisha matunda nje. Huu si utajiri tena, ni ugonjwa na ni kichaa cha kutafuta pesa.

Sauti ya wazee inasema:-

> **Tazameni nyinyi mlivyo, mmejaa Pupa! Wazee wetu hawakuwa wakiishi hivi. Waliishi peponi, walipendana, walishirikiana, walitamka pamoja, wakafurahi pamoja.**
> **(U.K. 21).**

Kwa ajili ya ulimbikizaji mali namna hii wanatumia kila mbinu ili wahifadhi kile walichokipata kwa njia isiyo ya halali. Wale wanaoumpinga katika shughuli hii na kumnyima fursa ya kujiendeleza, anawadidimiza wakadidimia dididi, wengine akawasagasaga wakasagika kama unga na wengine akawazika kwenye kaburi lenye kina kirefu kisicho mwisho. Hili ni tatizo la ukatili katika jamii.

Kwa hivyo tumeona matatizo makuu kuwa ni ya aina tatu; umaskini, puba na ubinafsi na ukatili. Katika kuonyesha matatizo yanayopatikana katika jamii pia ni lazima tutafute chanzo cha matatizo haya. Kwa hivyo, katika sehemu zinazofuata, tutatafuta chanzo cha matatizo haya kama inavyodhihirika katika tamthilia ya Pungwa.

## 2.4. *UBEPARI*

Ubepari ni mfumo wa kiuchumi unaowaruhusu watu wachache kumiliki "raslimali" na njia kuu za uchumi wa taifa. Nyenzo zote za uzalishaji mali huhodhiwa na walio wachache katika jamii. Ni mfumo usiotambua usawa na ambapo malipo hayaambatani au kulingana na jasho linalotolewa. Wanaotoa jasho jingi hulipwa mshahara kidogo ilhali wale ambao wamehodhi vifaa vyote vya ushalishaji mali hupata faida kubwa bila ya kuitolea jasho.

Karl Marx (1959:324-) akieleza kuzuka kwa ubepari anasema kuwa ulisababishwa na mabadiliko ya mbinu za kuzalisha mali ambapo viwanda vilichukuwa nafasi ya kwanza ya kujipatia riziki na uendelezaji wa maisha huku vikichukuwa nafasi ya mashamba ambayo hapo awali ndiyo yaliyoweza kutumiwa ili kuzalisha mali. Waliokuwa mashambani waliamua kuuza mashamba yao na mengine kutwaliwa nao kuelekea mjini ili kutafuta kazi viwandani. Hali hii ya kutwaliwa kwa mashamba ilisababisha kupatikana kwa vibarua waliolipwa malipo ya chini viwandani kwani walihitaji kula na kulisha jamii zao. Vibarua hawa wakawa ndio soko la kununua nguvu rahisi na pia la kuuzia zile bidhaa walizozitengeneza wao wenyewe viwandani kwa bei iliyowekwa na wenye viwanda.

Kutokana na kulipa mishahara duni na kuweka bei wao wenyewe, wenye viwanda walipata faida nyingi hivyo kusababisha watu wachache kuwa na mali nyingi ingawa hawakuitolea jasho huku wengi walijaribu kuuza nguvu zao ili wayakimu maisha yao ya kila siku. Wingi wa watu wasio na kazi, mishahara duni na bei iliyopendelea wanaviwanda ikawa ndiyo nguzo ya kuuhimili ubepari. Lugha ikawa ni pesa na faida kwa mabepari nao mafalahi wakazidi kufukarika. Wingi wao, uhaba wa kazi na mishahara duni vikawa kama silaha dhidi ya mafalahi. Serikali za kibepari ambazo ziliendeshwa na mabepari hao hao zikaendelea kuwatoza maskini kodi licha ya umaskini wao. Walipoteta, ikawa ni kutumia askari na virungu ili kuwanyamazisha.

Mabepari hawa walipomaliza kung'angania mali iliyokuwa huko kwao wenyewe kwa wenyewe, walivuka mipaka na bahari ili kwenda kutafuta malighafi ya kutumia viwandani mwao. Matokeo ni kwamba walichukuwa nchi za wenyewe na kuzigawanya miongoni mwao kwa ajili ya kupata malighafi, vibarua nafuu na soko la kuuzia bidhaaa zao. Huu ukawa ndio mwanzo wa ukoloni na makoloni.

Wakoloni waliposomba walighafi na kuhakikisha kuwa wamezifanya nchi hizo kufilisika, na kuona kuwa hakuna tena faida ya kuendelea kuyaweka makoloni haya, walianza kutoa uhuru kwa nchi hizi lakini si kabla ya kutayarisha kundi litakalochukuwa hatamu za uongozi kwa misingi na katiba zilizowekwa na hawa wakoloni ambao kwa hakika waliendeleza ubepari. Uhuru wa bendera na wimbo wa taifa ulipopatikana, mfumo wa kibepari ulikuwa umeimarika na hivyo makubaliano kati ya viongozi wapya na wakoloni waliokuwa wakiondoka ikawa ni ahadi za kuendelea kuyalinda maslahi ya mabepari kwa kutumia katiba walizopokea kutoka kwa mabwana zao.

Mashirika na makampuni makubwa yaliendelea kumilikiwa na mabepari wale wale na faida nyingi ikaendelea kuhamishwa hadi Ulaya. Mabepari hawa wa kigeni wakawachagua wananchi wachache na kuwafanya wakurugenzi ili ionekane kama kwamba wenyeji ndio waliosimamia makampuni, mashamba na uongozi serikalini- yalifanywa kuonekana kama ni ya wenyeji lakini ukweli ni kwamba hayakuwa yao.

Wengi wa wale walioshika hatamu za uongozi serikalini, makampuni, mashamba na mashirika makubwa makubwa wakawa mbioni kujitajirisha kwa haraka bila ya kuwajali wananchi wa kawaida waliotakiwa kuwalinda na kutumikia. Uporaji wa mali ya umma ukawa ndio shughuli kuu ya viongozi hawa wapya. Mbali na kushirikiana na wanyonyaji wa kutoka nje kupitia kwa makampuni, mashirika na mashamba yao, waliweza pia kuwanyonya wenyeji kwa kufuja na kuamisha mali ya taifa iliyotokana na kodi iliyolipwa na waninchi. Unyonyaji ukawa katika sehemu mbili, moja iliyoendelezwa na mabepari wakongwe kupitia makampuni yao na wa pili ukatoka kwa mabepari mchwara waliotokana na viongozi wenyewe wa nchi zinazonyonywa.

Tamthilia ya Pungwa imejengeka katika hali ambayo tayari uhuru upo na walio na madaraka na nguvu kifedha katika nchi hizi huru wamo mbioni kutafuta mali bila kujali maafa yatakayotokana na vitendo vyao. Uporaji na ulimbikizaji wa mali ya taifa katika mikono ya walio wachache umetapakaa katika jamii na unawakilishwa na jamii ya Bwana na Bibiye.

Bwana na Bibiye yametumika kimajazi ili kutumika kama kiwakilisho tu cha mabepari wengine popote katika nchi zinazoendelea. Kwa kutumia mbinu hii, mwandishi amefanikiwa kuonyesha kuwa ubepari hauna mipaka kwani jina Bwana na Bibiye laweza kutumika kokote kule sababu ni jina la kijumla, sio jina maalum. Majina yenyewe pia yana ule ubwana ndani yake na kuonyesha kuwa wao ni watukufu na wenye mali na heshima.

Unapokuwa na Pesa hata ukiwa kijana wa umri mdogo utaitwa "mzee" hata na wazee wenye umri kuliko wako. Kwa hivyo jina Bwana na Bibiye linasimamia ile mali yote waliyopora na yale maisha yao ya raha na uwezo wao kifedha.

Aidha, S.A. Mohamed ametumia majina haya kuonyesha jinsi wananchi hawa walivyopata madaraka na kuwadharau wananchi wenzao waliopaswa kuwalinda na ambao ndio wanao walipa mshahara kutokana na kodi wanayoitoa. Sasa wana watumishi, walinzi na wafanyakazi wengi ambao wanawaita Bwana na Bibiye.

Jina Bwana na Bibiye pia limetumika kuonyesha lile tabaka jipya lililoundwa kutoka kwa

wananchi wenyewe ambalo sasa limechukuwa nafasi za wakoloni na kuwa mabwana wapya na mamsahibu wapya. Kwa hivyo majina haya yawakilisha tabaka la juu jipya katika jamii huru kama tutakavyoona baafpye.

Mwandishi ameupa ubepari mtazamo wa kihistoria kwa kuonyesha kuwa ndio chanzo cha matatizo yanayozikumba nchi nyingi zinazoendelea.

Kwa kutumia chanzio ambako wimbo unasikika, mwandishi ametumia mbinu ya ki Aristotle kututangulizia oni zito na muhimu litakalotawala tamthialia yote. Aristotle alipendekeza kuwa wimbo utangulie unapoandika tamthilia naye msanii hapa ametumia mbinu aliyoiita chanzio.

Katika chanzio, tunapata historia ya ubepari ingawa kwa ufupi. Sauti ya mzuka inasema kuwa ana shahada mara tatu. Hili linamaanisha kuwa amepitia tayari hatua tatu. Hili litaeleweka zaidi hasa tugunduapo kuwa shahada ina maana ya maji ya kuoshea maiti.

Hatua ya kwanza ni ile ya ubepari wa mwanzo kabla ya makoloni kuanzishwa na ubepari kusambaa. Ubepari wa aina hii ulikufa wakati wale waliong'ng'ania kujiendeleza katika nchi zao bila kutafuta masoko huru ya nje, malighafi na vibarua rahisi. Hawa walifilisika na kutoweka katika historia.

Hatua ya pili ya ubepari ni wakati wa ukoloni mabepari waliponyakuwa nchi na malighafi za wenyewe na kuenda kuendelezea viwanda vyao na kutajirisha nchi za kwao. Hatua hii nayo ilitoweka na uhuru ukatolewa kwa nchi kandamizwa.

Hatua ya tatu nayo ikaanza wakati wa ubepari wa nyakati za ukoloni mamboleo. Hali hii ndiyo inayoendelea hadi leo. Ingawaje sasa ukoloni haupo lakini ubepari unaendelea chini ya ukoloni mambo leo. Sasa mabepari wanatawala lakini kwa mbali huku wakitumia vibaraka wao. Kuipatia hali hii mtazamo wa kihistoria, mwandishi anasema:-

> Kweli shahada mara tatu
> Moja ilikuwa jana,

Moja iko leo,

Na nyingine kesho ......(uk.3)

Madhumini ya mabepari si kuendeleza nchi wanazozinyonya bali ni kusomba hata punje ya nafaka na sukari kwa kunyakua faida yote wanayoipata ili waende kunufaisha wenzao.

S.A. Mohamed hakutaka kusingizia tu mabepari wa kutoka nchi za nje bali alijua kuwa wanashirikiana na wale wa ndani ili kufanikisha unyonyaji wao. Bila ya kushirikiana na hawa wa nyumbani, ni vigumu sana wale wa nje waweze kuendelea na wizi wa mali ya umma. Kuna pepo wa kwanza ambaye alivuka bahari saba na huyu ni ubepari wa ng'ambo. Kisha kuna pepo wa "kikwetu" au pepo wa "kienyeji" ambaye anawakilisha wale mabepari waliomo nchini wanaotumika kama daraja ya kuhamisha mali inyotokana na jasho hadi ng'ambo. Bali anavyosema mwandishi mwenyewe kupitia Bwana:

**BWANA: Kila mmoja ana nguvu zake kwa wakati wake ... na kiti ni mtu mmoja ... lakini naona huyu wa kienyeji kadhibitiwa na wa kigeni mara nyingi. (U.K. 24)**

Hivi ni kusema kuwa ule ubepari wa kienyeji hauwezi kujitoa kwa ule wa Ngambo hata kama utakata kufanya hivyo. Wakikataa kushirikiana na mabepari wa ng'ambo basi watawacha kuwahifadhi nao wataporomoka.

Ingawa mkoloni ameondoka na hayupo tena, hili halimaanishi kuwa ubepari umetoweka. Ni kweli kuwa mkoloni hayuko tena machoni petu lakini yale yote aliyoyaanzisha bado yangalipo kwani sera zake ndizo zinazoendelea kutumika. Mfumo wa kiuchumi ni ule ule, sheria za nchi ni zile zile, elimu ni ile ile ya wakoloni.

Ngugi (1986:96) anasema kuwa ukoloni mamboleo ulichukuwa sura mpya wakati Marekani ilipoanza kusambasa mirija yake ya unyonyaji. Miaka ya 70 ilidhihirisha mashirika ya kifedha na kiuchumi yenye asili ya kimarekani yakijitwalia masoko katika bara la Asia, Afrika na Amerika kusini huki yakisaidiwa na shirika la fedha duniani pamoja na Benki ya Dunia ambayo

yalitawala siasa, uchumi na hata utamaduni wa nchi zinazoendelea.

Kama tulivyotangulia kuona, ubepari wa nchi hizi ukawa unaendelezwa kwa viwango viwili. Kiwango cha kwanza kikawa ni kile cha viongozi wa nchi hizi zinazoendelea walipoanza unyonyaji na uporaji wa hali ya juu wa mali ya kitaifa kwa ajili ya tamaa, ubinafsi na maisha ya starehe kwa haraka.

Bwana na Bibiye, wakiwakilisha mabepari wa kienyeji au kikwetu (mabepari mchwara), wameshajipataia kasri la fahari, tanda la kujimwaya magari na mambo mengine ya thamani. Hili ni kundi lililo mbioni kutafuta mali kwa pupa ili wajipatie utajiri wa haraka na waupatie umaskini mgogo mradi sasa mkoloni ameondoka. Wamo mbioni hivi kwamba Bwana hana hata wakati wa kupumzika wala kunywa kikombe cha chai. Mawazo haya yanafanana na kuoana na yale ya Baba kitaru katika Hussein (1971:4) ambapo Baba kitaru naye yu mbioni kutafuta mali ili aukimbie umaskini.

Mama kitaru analalamika kuwa ana mkono mmoja na hawezi kufanya kila kazi jinsi Bibiye anavyolalamika.

Wengi wa viongozi huwa mbioni kutafuta mali kwa ajili ya kufurahisha jamii zao ambazo zinatamani maisha ya juu. Wanaogopa kushuka ngazi baada ya kupanda daraja. Hawataki kurudi kwenye kundi la maskini ambao sasa wanasema kuwa wananuka.

Bibiye anatamani kila litokalo Ulaya kwa imani kuwa ni bora kuliko kinachotengezwa nchini. Mahitaji kama haya hulazimu Bwana kufanya kazi kufa na kupona au atumie ujanja na ulaghai wa kalamu ili aendeleee kuwatimizia mahitaji yao.

Familia ya mtu mmoja imehodhi kila kitu kuonyesha jinsi walio wachache huhodhi kila nyenzo za uzalishaji mali. Hii ndiyo nguzo ya ubepari.

Kuwepo ubepari na ukosekanaji wa usawa na ujamaa husababisha ubinafsi na hali ya

kutowafikira wengine. Jambo ambalo ni sifa moja ya ubepari. Utu na udugu kwa majirani ni jambo la nadra kwani wanawafikiria tu wana waliowazaa. Wengine wote wanaonekana kama maadui, wafitini na wenye choyo au kinyongo dhidi yao. Kwa maoni ya Bwana, wale maskini hawana wa kumlaumu isipokuwa ujinga na uchache wa akili zao.

Lakini tujuavyo ni kwamba watu hawa si wajinga wala wachache wa akili bali ni kukosa nafasi za kujiendeleza ambazo tayari zimekwisha nyakuliwa na kuhodhiwa na Bwana na Bibiye.

Kutokana na ufahamu wao kwamba waliyoyapata hayakuja kwa njia ya halali, mali na madaraka hulindwa kwa vyovyote vile hata ikibidi kwa kukandamiza, kuangamiza au kuua. Bwana ameshawadidimiza hasimu zake, wengine akawasagasagwa kama unga na kuwazika wengine kwenye kaburi lenye kina kirefu kisicho mwisho. Kwa hakika hii ni siasa ya kumalizana, siasa ya kudidimiza wengine na wengine kusagasagwa kama unga. Mfumo wa kibepari unaendezwa kwa ukandamizaji, udhalimu na mauaji ili uweze kusimama.

Katika kazi hii, kiwango cha pili cha unyonyaji ni kile cha mabepari wa nchi zilizoendelea kunyonya zile zinazoendelea. Mabepari hawa wakishirikiana na wale wa nchini, huomba mali na faida yote na kuipeleka Ulaya. Bwana ana "deals" (Mipango) na Maganlal na Bw. Hans.

Bw. Hans anawakilisha mashirika na makampuni ya kutoka nje lakini yaliyojengwa katika nchi zinazoendelea. Maganlal naye anawakilisha wafanya biashara wa kati ambao wengi wao huwa ni wahindi wakora wanaoshirikiana na wasaliti kama Bwana wakihamisha pesa za nchi ambazo zinahitajika nyumbani kuliko kule ngambo, hadi nje na kuziweka huko.

Kama tulivyokwishaona, watu hawa hufanya hivyo kwa ajili ya faida kubwa wanayoipata wanapoweka pesa zao katika mabenki ya ngambo kwani sarafu kama vile dola huwa na thamani kubwa kuliko sarafu za huko kwao. Nao uchumi wa nchi zinazoendelea huzorota mara kwa mara kutokana na vitendo vya wahujumu uchumi kama vile Bwana, Maganlala na Hans. Hili linawafanya wakose imani na uchumi wao mbali na ukweli kuwa nchi hizi haziko wima kisiasa kutokana na hali hii ya unyonyaji na zinaweza kulipuka wakati wowote. Kwa hivyo, mbali na

tamaa, wao pia huogopa wale waliowanyanganya, kudidimiza na kusagasaga kwani wanaweza kuamua kuchukuwa kilicho chao na kulipisa kisasi.

Kwa maoni yetu, watu hawa ni hatari na adui wakubwa wa nchi zao hata kuliko mabepari kutoka nje. Hawa ndio hushirikiana na wahindi wakora na mashiriki ya kigeni yaliyomo nchini ili kuipora na kuisafirisha mali ya taifa kwa makubaliano kati yao. Bila ushirikiano wa wasaliti kama hawa, ingelikuwa vigumu kwa mabepari wa ng'ambo kutekeleza unyonyaji wao.

Uwezo wa watu hawa (akina Bwana na Bibiye) ni ule tu wa kuendeleza miradi midogo midogo na hawana uwezo wa kuanzisha miradi mikubwa kama vile viwanda. Akieleza juu ya watu hawa, Fanon (1967:141) anasema:

> **Watu hawa wanaotaka utajiri wa haraka wanakosa mawazo makuu au miradi yenye maana. Wanaendesha serikali wakitumia mawazo waliyoyasoma kutoka vitabu vilivyoandikiwa Ulaya bila kuelewa hali halisi iliyomo nchini mwao.(TY)**

Watu hawa hawako pale kwa ajili ya maendeleo ya taifa lao bali ni kiungo cha kutekeleza unyonyaji.

Kwa hivyo, mwandishi ameeleza kuwa moja ya sababu za kuwepo matatizo ni ubepari. Ubepari huu ameuweka katika sehemu mbili: wa nje na wa ndani. Aidha, ameufuatilia kihistoria na kuonyesha ulivyokuja, ukapeleka mizizi hadi leo. Yeye hakutaka kulaumu tu mabepari wa nje bali pia ameonyesha kuwa viongozi wetu wenyewe ni tatizo kwani wanachangia katika uporaji huu.

## 2.5. ***MATABAKA NA MIKINZANO YAKE KATIKA JAMII***

Mfumo unaojengeka katika misingi ya kibepari husababisha watu wachache kuhodhi mali zaidi ya ile wanayohitaji na huku walio wengi wakabaki bila chochote.

Ngara (1985:21) anasema kuwa katika jamii yenye matabaka, nguvu za kiuchumi huwa na

watawala ambao huhodhi nyenzo za uzalishaji mali. Anaendelea kusema kuwa tabaka hili hili ndilo pia husimamia elimu na itikadi katika jamii. Mawazo, imani na itikadi ya tabaka tawala huchukuliwa kuwa ya jamii nzima.

Katika swala hili la matabaka, Marx (1959:330) anaigawa jamii katika sehemu tatu. Kunalo tabaka la juu ambalo ni la watawala na mabepari wenye viwanda. Kuna tabaka la kati ambalo linahusisha makundi kama vile wenye viwanda vidogo vidogo, wafanya biashara ya maduka ya jumla, mafundi wenye ujuzi na wakulima. Kisha kuna tabaka la chini ambalo ni la watamba-na-njia, makahaba na wote wasio na kazi.

Tabaka hili la mwisho halidhamini kabisa na analiona kama tabaka lisilo na msimamo wala mwelekeo. Kwake, tabaka linalotegemewa kuleta mabadiliko katika jamii ni lile la wafanyakazi.

Katika tamthilia ya Pungwa, mwandishi ametambua matabaka mawili na hali ya jamii iliyo katika jamii ya mwandihsi. Jamii nyingi za kiafrika zimegawika katika matabaka mawili - la juu na la chini; tabaka la watawala ambao pia ndio wenye mali na lile la watawaliwa wasiomiliki chochote.

Tabaka la viongozi na wenye mali wanaishi katika anasa na raha. Kundi hili linawakilishwa vizuri sana na Bwana na Bibiye ambayo ni majina yanayoonyesha ule ubwana, utajiri na heshima zao kutokana na madaraka na ile mali waliyojilimbikia. Tabaka hili la juu halina raha vile tunavyotarajia. Wana wasiwasi kuhusu ukweli kuwa mali yao hawakuipata kwa hahali.

Kama tulivyoona, watu hawa wanawakilisha kundi ambalo lilikuwa mbioni kujinyakulia mali kwa pupa ili kupata utajiri wa haraka na kuupatia umaskini mgongo. Ni kundi lililochukuwa mahali pa watawala wa kikoloni na kuunda tabaka jipya la watawala na wafanyabiashara. Mwandishi anasisitiza ule ukweli kwamba kundi hili halina usalama wao hata kama lina mali nasi tunarudia jambo hili kwa sababu iyo hiyo.

Bwana na Bibiye wamewaajiri walinzi langoni ili kuhakikisha kuwa mali yao na usalama wao uko imara. Katika maisha ya kawaida, utawakuta watu hawa wamewaajiri walinzi milangoni, ving'ora vya hatari, seng'eng'e za stima, madirisha na milango ya chuma na mbinu nyingine za kujihami dhidi ya maadui wao.

Maadui hawa wamo katika makundi yote mawili. Kuna wale maadui wanaotoka katika tabaka lao la juu ambao kwa ajili ya mashindano, wivu, fitina na uroho wanapingana wenyewe kwa wenyewe. Hawa ndio wale waliosagwasagwa kama unga, wakadidimizwa na kuzikwa kabisa kwenye kaburi lenye kina kirefu. Kwa hivyo kuna mitafaruku na migongano baina ya watu wa tabaka la juu ambayo Marx anasema kuwa ni kwa manufaa ya wafanya kazi.

Adui wa pili ni wanyonge, wasio nacho ambao pia ndio wengi katika jamii. S.A. Mohamed anawaona hawa kama tabaka moja ingawa Marx aliwagawanya kwenye visehemu vitatu.

Kisehemu cha kwanza kilikuwa cha wenye viwanda vidogo, vidogo wenye maduka na wenye ujuzi fulani wa kiufundi ambao Marx alisema kuwa wanapinga mabepari kwa ajili ya kutaka nafuu wao binafsi. Sehemu ya pili katika kundi hili ni wafanyakazi ambao anawaona kuwa ndio wenye kuleta mabadiliko muafaka katika jamii nalo ni kundi la wafanyakazi. Kundi la tatu ni la watamba-na-njia na wengine wasio na kazi ambao Marx anawaita ni kundi hatari ambalo halijui liko wapi na linaelekea wapi. Mara watajiunga na watawala kupinga mageuzi na mara wajiunge na wafanyakazi kuleta mabadiliko. Ni wenye kigeugeu na hawawezi kutegemewa.

Said Ahmed Mohamed anakataa kuiangalia jamii ya kiafrika kwa mtazamo huu. Yeye anayaona makundi haya yote kama kundi moja la tabaka la chini.

Watu wa tabaka la wanyonge yanawakilishwa na walinzi, watumishi kama vile Kibwege, Kijuha na Mwantabu, Simba na kikundi chake, Mahoka na Mzee Burhani.

Mengi ya majina haya ni majazi yaliyoteuliwa maksudi ili kuwakilisha watu fulani katika kundi au tabaka hili. Mwantabu kwa mfano ni mtu mwenye taabu na shida mbali mbali na hili

linaonyesha shida na taabu walizonazo watu wa tabaka la chini. Kijuha ina maana ya mtu anayeishi kijinga na kudharauliwa kwa ajili ya kunyamaza kwake. Hii inaonyesha ile tabia ya watu wa tabaka la chini kuwa wajinga na kuendelea kulala kati kati ya matatizo yao yote. Kibwege nalo lina maana ya kimtu kijinga, fala na mpumbavu. Majina haya yote yanaonyesha ile dhana ya tabaka hili kuchukuliwa kuwa la watu wajinga, waliozubaa na wapumbavu. Watu waliolalia masikio.

Mahoka nalo lina maana ya mambo ya kijinga jinga ambayo hayawezi kuleta faida yoyote. Kwa hivyo huyu Mahoka anawakilisha kundi ambalo hutoa mapendekezo na maoni ambayo hayaleti faida yoyote kwa jamii. Suluhisho huishia tu katika ngoma na maneno.

Burhani nalo lina maana ya uwezo wa Mungu au kipawa cha Mungu. Hawa ni watu wanaoamini kuwa ni uwezo wa kimungu tu unaoweza kuleta mabadiliko. Ni watu wenye mawazo ya dini na wamo kwenye tabaka la chini lenye kuonewa na kuwa lishirikishwe katika shughuli za kiukombozi kama kundi zima bila kuwacha yeyote nje.

Mohamed amefaulu kutuchorea jamii ya matabaka mawili la juu na la chini katika jamii. Lile la kati kati ni la kupita tu kwani baadhi yao watapanda ngazi na kujiunga na watawala na baadhi washuke ngazi na kujiunga na wanyonge.

Jamii hii ni jamii ya matabaka na matabaka haya yameonyeshwa kihistoria, kwamba yalianza baada tu ya kuondoka mkoloni. Matabaka haya mawili daima yamo katika mikinzano kwani chambilecho Hussein (1971:56) "Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono".

## 2.6 ***MAPAMBANO YA KULETA UKOMBOZI***

Jamii iliyojengeka kimatabaka ni jamii inayokalia bomu. Inaweza kulipuka wakati wowote. Kuwepo matabaka katika jamii ni kichocheo cha kuzusha mapambano ambayo hatimaye

yataleta mapinduzi katika jamii - mapinduzi ya kuzua hali mpya ya haki na usawa-ya ujamaa.

Marx (1959:319) anasema kuwa historia ya jamii hadi leo ni historia ya mapambano baina ya matabaka. Kulingana naye, matabaka ni muhimu katika kuleta mapinduzi kwani huzua mikinzano na mitafaruku inauyoishia kwenye mapambano na hatimaye mageuzi ya mfumo wa jamii kiuchumi, kisiasa na kitamaduni.

Wanaopendekeza nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti husema kuwa ni muhimu mapambano haya dhidi ya unyonyaji yaelekezwe kwenye watawala kwani serikali ndiyo hutumiwa kulinda mali ya mabepari. Mageuzi yoyote yasiyogeuza serikali hayafai kitu kwani nguvu za uchumi bila nguvu za kisiasa ni jambo linalolegalega.

Mahoka, mtu mwenye kuongea mambo ya kijinga jinga, anaanza harakati za kumuagua Bwana. Baada ya kugundua kuwa Bwana amekumbwa na shetani ambaye anawanyonya maskini kwa kushirikiana na matajiri wa nchi zinazoendelea, anashindwa kutoa dawa muafaka ya kuuondoa ugonjwa huu. Anaishia tu katika kupiga ngoma na maneno matupu ambayo hayana faida. Anaenda tu kumuagua Bwana kwa vile ameitwa na Bibiye na atalipwa kwa jukumu hili.

Mahoka anawakilisha kipindi maaluum katika historia ya mapambano dhidi ya wanyonyaji wakati ambapo watu walitambua matatizo yaliyoikumba jamii lakini wasitoe suluhisho lolote isipokuwa kuyataja tu. Mahoka anawakilisha kile kipindi cha wakati wa uyakinifu ambapo jamii ilielezwa ilivyo bila ya kutoa suluhisho la kuirekebisha. Yeye anamuagua Bwana lakini tiba yake haitoi.

Aidha, wengi wa waandishi wa wakati huo walitaka kutoa maelezo kwa watawala ili warekebishe tabia zao na waendelee kutawala vyema. Waliitwa na serikali hizo na kupewa jukumu la kuonyesha matatizo na makosa ya watawala ili wajirekebishe. Hatua hizi zilishindwa kama alivyoshindwa Mahoka. Hatua ya pili katika historia ya mapambano ni ile ya Mzee Burhani.

Mzee Burhani anatambua matatizo ya Bwana kuwa ni Shetani na hata kutaja matatizo hayo kwa jina kuwa ni pepo aitwaye Mfakamizi. Huyu ni pepo anayewakilisha ubepari na hii ni kusema kuwa ubepari ndilo tatizo hapa kinyume na Mahoka ambaye alitaja tu shetani bila kueleza ni shetani wa aina gani. Burhani anaenda hatua moja mbele zaidi na kutoa tiba au suluhisho kwa ugonjwa wa Bwana. Suluhisho ni kumfanya Bwana ageuze mwenendo wake, awache kushirikiana na mashetani na aishi kama wengine. Asitegemee vyakula vya anasa na nguo za bei ghali ghali ambazo hutumia na ashirikiane na wenzake kwa kufanya kazi kwa mikono yake mwenyewe ili apate riziki kwa kutoa jasho badala ya kutegemea vya bwerere.

Ingawa Burhani anapiga hatua zaidi ya Mahoka, yeye pia anashindwa kwa sababu katika suluhisho lake, haonyeshi jinsi litakavyotekelezwa. Burhani anawakilisha kile kipindi cha historia ambapo kulizuka uyakinifu wa kiuhakiki ambapo matatizo yalionyeshwa na chanzo chake kutajwa. Kisha walitoa mapendekezo hayo yakashindwa kutekelezwa kwani hawakuonyesha namna bora ya kuyatekeleza. Wengi wao walipewa fursa ya kujiendeleza na wakanyamaza kwani nao pia walikuwa wahitaji.

Hadi sasa, watu hawa wapo kwani watapiga makelele wakitaka mabadiliko lakini wapatiwapo fursa ya kujiendeleza, hukaa kimya. Wanasiasa, wasomi, makundi ya kidini wote hupiga makelele dhidi ya serikali za wanyonyaji lakini waingizwapo katika jarida la kulipwa, midomo yao hufungika.

Hatua ya tatu ni ile ya Simba na kundi lake. Simba amewakusanya watamba-na-njia na makundi mengine yasiyo na kazi ama kazi za vibarua na kuwaongoza katika kuleta mapinduzi.

WanaMarx husema kuwa ukombozi wa wafanyakazi ni sharti utekelezwe na wafanyakazi wenyewe. Fanon (1967:192) anasema:

> **Unyonyaji wa kikoloni, umaskini na njaa isiyo kikomo humsukuma mwenyeji hadi kufikiria upinzani ulio wazi na maasi yaliyopangwa (TY)**

Mohamed anaelekea kuunga mkono mawazo ya Fanon kuliko yale ya Marx. Katika harakati

hizi, Simba hakuwakusanya wafanyakazi na kuwaongoza bali aliamua kutumia lile kundi la lumbeni proletariati ambalo Marx hakuliheshimu hata kidogo ingawa alikubali kuwa laweza kutumiwa ama na watawala au wafanyakazi.

Katika tamthilia ya Pungwa, mapambano yanaanza na hili kundi lisilo na mwelekeo na hatimaye kuwashirikisha wafanyakazi wote- watumishi nyumbani, walinzi na hata polisi. Hii hatua ya tatu ya kutumia silaha ili kuleta mapinduzi ya kweli ndiyo inayofaulu. Mabepari hawawezi kujirekebisha wao wenyewe na hawatatoa mamlaka kwa sherehe na ngoma. Wanyonge wanaulizwa kuwa imara ili kutetea haki zao.

Hata hivyo kuna upungufu wa mwandishi kwamba hakutuonyesha matayarisho ya mapinduzi haya. Inatarajiwa kuwa waelimishwe na kutayarishwa kielimu na kiitikadi ili wawe tayari kutekeleza mapinduzi. Tunawakuta Simba na wenzake kule mwisho mwisho na kuonekana kama kuwa walipachikua tu pale.

Kutoa maelezo machache kuhusu televisheni inavyosema hakututayarishi kukumbana na mapinduzi haya. Hata walinzi wanaulizwa ghafla na kujiunga na mapambano nao watumishi ni vivyo hivyo.

Kinachofanikisha mapinduzi haya ni wingi, umoja wao na silaha zao. Mapinduzi yenyewe hayakumwondolea mbali Bwana na Bibiye kwani nao pia wanahitajika katika ujenzi wa jamii mpya. Wanaadhibiwa kwa bakora ili wayarekebishe makosa yao.

S.A. Mohamed, ametuonyesha harakati za mapinduzi zilivyotekelezwa kihistoria hadi kufikia hatua ya usoshalisti ambayo ndiyo inayofaulu kuleta mabadiliko haya.

## 2.7. ***UUNDAJI WA JAMII MPYA***

Lengo la harakati za mapinduzi kulingana na Marx (1959:330) ni kuunda jamii mpya yenye haki na usawa. Ni jamii ambayo matabaka yatatoweka na mali ya mtu binafsi kutupiliwa mbali na badala yake kuundwa mali ya umma.

Hatua ya kwanza katika kutekeleza haya ni kuwezesha wafanyakazi kutwaa madaraka kupitia mapinduzi. Baada ya hatua hii, kunakuwa na nyingine ya kuufuta kabisa unyonyaji na kuondoa mali ya mtu binafsi. Mali hii itawekwa chini ya ulinzi wa wengi ambao wataitumia kwa faida ya wote.

Marx anasema kuwa baada ya hatua hii kufikiwa, hakutakuwa na haja ya serikali tena kwani anaiona serikali kama chombo kinachotumiwa na tabaka moja kulinyanyasa lile jingine.

Kwa hivyo, katika jamii ya Pungwa, shughuli zote zinazofanywa mwanzoni zinashindwa kuleta mabadiliko yatakayosababisha kuweko ujamaa. Shuguli za kumtibu Bwana kwa kutumia vidonge au madawa ya kigeni hazifaulu. Madwa haya yanawakilisha mapendekezo na marekebisho yanayotolewa na nchi za magharibi ili kuirekebisha hali iliyo kwisha haribiwa na viongozi wakishirikiana na mabepari wa nchi zile zile zinazotoa mapendekezo haya.

Mbinu nyingine ya kuleta jamii ya usawa ni ile inayotumiwa na Mahoka ambaye kama tulivyotangulia kuona ni mtu wa maneno na kupiga makelele tu. Huyu anawakilisha wale wanasiasa na wasomi ambao hupiga tu makelele kwa ajili ya kutoshirikishwa katika harakati za uporaji lakini pindi wapatiwapo nafasi, hukaa kimya na kuendelea "kula". Mbinu hii haiwezi ikaleta mabadiliko yoyote yenye maana.

Mzee Burhani naye anayo mbinu yake ambayo kwa kiasi kikubwa imepiga hatua kwani hataji tu matatizo bali anatoa mapendekezo ya kurekebisha hali hii na hata kutoa elimu ya itikadi. Lakini mbinu yake inakosa kufaulu kwa sababu yeye anajaribu kurekebisha watawala, jambo ambalo haliwezekani. Mwishowe anapewa mali na utajiri wa kiwango cha wale wengine wa

nchi hiyo na ananyamaza. Mbinu za watu hawa wanaosema kuwa wanatetea haki za wanyonge na kudai siasa ya ujamaa hunyamaza wanapoingizwa katika tabaka la juu. Kuwa wanasiasa, wahadhiri na wanafunzi ambao hudai kuwa ni wasoshalisti na wanaujamaa halisi wakati hawana chochote lakini wakipandishwa madaraka au kupewa fursa, wanakuwa kama wale mabepari wengine.

Mapinduzi yanayofaulu kuleta ujamaa ni yale yanaoyoongozwa na Simba na ambayo yana jumlisha makundi yote ya tabaka la chini. Jamii mpya iliyoundwa ni ya kijamaa kwani wamefaulu kuwanyang'anya Bwana na Bibiye mali yao na kuitaifisha.

Jambo hili linawakilishwa na yale matendo ya wafuasi wa Simba wanapojitupa kwenye masofa, vitanda, kufunguliwa T.V na video, kula matunda na kufurahi. Huku kutumia mali ya Bwana kwa ajili ya furaha ya wote inaashiria kutumia mali kwa faida ya wengi katika jamii.

**MTU MMOJA: mmmmmmm, matunda matamu**
**Haya sijapata kula**
**Mwingine: Maisha matamu (U.K55)**

Wao sasa ndio kwanza kusikia maisha waliyoishi Bwana yalivyo matamu na wanashangaa na kuyafurahia. Inaashiria maisha yalivyo mema chini ya ujamaa kwani kila mtu atafaidika na mali yao, inayotokana na jasho lao.

Jambo jingine katika jamii hii mpya ni kwamba sasa hawana viongozi mabwana bali wote sasa wako sawa. Hata Simba aliyewaongoza kwenye mapinduzi anakataa asiitwe kiongozi.

**BWANA**: Wewe ndio mkuu wao sio?
**SIMBA:** Sote tu wakuu hapa, na sote tu wadogo (u.k. 52).

Haya yanaonyesha kuwa jamii iliyoundwa sasa ni jamii yenye usawa, haki na ujamaa. Matabaka sasa yametoweka.

Lakini pia hapa mwandihsi ametupeleka mbio kwa kutufikisha kwenye jamii isiyo na viongozi wala matabaka bila ya kupitia ile hatua ya utawala wa wafanyakazi ambao ungekuwa utawala wa mwisho wenye matabaka na viongozi.

Mwishoe katika jamii hii mpya, kuna marekebisho yanayofanyiwa bwana na Bibiye ili wageuze tabia yao ya ubwana, ubinafsi na unyonyaji na baadaye wanaruhusiwa kujiunga na wengine katika ngoma hii mpya, ngoma ambayo wote wataicheza. Hakuna haja ya kuwaua na kuwasaka hawa waliokuwa juu wala kulipisa kisasi.

wanajamii wote wanahitajika katika ujenzi wa jamii mpya. Lakini lazima kwanza waadhibiwe kutokana na makosa ya kuihujumu jamii na watoe pesa zao zote kwa jamii.

Kwa hivyo, mwandishi ameunda jamii yenye ujamaa isiyo na matabaka wala viongozi. Watu wote sasa ni sawa katika jamii.

## 2.8. ***MWANAMKE NA UDHALIMU***

Katika kazi ilizotangulia za riwaya na mashauri, S.A. Mohamed daima amemsawiri mwanamke kama kiumbe dhaifu na mnyonge ambaye yuko chini ya himaya ya mwanamme. Anachukuliwa kama mnyonge na anayenyanyaswa na hivyo basi anahitaji kuendeleza harakati za ukombozi ili ajikomboe. Hapaswi kukubali kidunishwa na kudharauliwa na wanaume. Haya yamejikokeza wazi, miongoni mwa kazi nyingine, katika Asali chunga kumhusu semeni na wenzake, na Maimuna, Bi Tamima na wenzake katika Utengano. Lakini katika tamthilia hii ya Pungwa, mwandishi anaelekea kuchukuwa mkabala tofauti kumhusu mwanamke.

Wengi wa wale waliowadhulumu wenzao katika kazi zilizotangulia ni wanaume. Lakini katika kazi hii, tunaona mwanamme akishirikiana na mwanamke katika shughuli hii ya kunyanyasa na kuwanyonya wengi katika jamii wengine. Picha tunayoipata ni kuwa udhalimu ni udhalimu uwe unatekelezwa na mwanaumme au mwanamke ushitoshe ule wa mke unaelekea kuuzidi ule wa mwanamme hivi kwamba anakuwa ndiye chanzo cha Bwana kutenda mengi ya yale maovu yote.

Bibiye ndiye anayemshauri Bwana asiwe na uhusiano wowote na watu wa ukoo wake isipokuwa yeye mke na watoto wao waliowazaa. Hii ni sumu ya ubinafsi na hili linasababisha Bwana kukosa utu wala kujali maslahi ya wenzake.

Aidha, utawala wa Bibiye juu ya wanawake wengine ni wa kusikitisha. Anawakaripia, kuwakemea na kuwasuta watumishi wake kama maguo yaliyoisha thamani. Kwa mfano anawatukana kwamba wao ni maskini na wahitaji kama mzee Burhani.

Pia anawakumbusha kuwa yeye ndiye amewaajiri kazi na wanaweza kumwaga unga au kuachishwa kazi wakati wowote. Hili linawafanya watende kazi kipunda.

Majibu yake Bibiye ni yenye kiburi na dharau ya hali ya juu kwa watu ambao wanamhudumia na kumtumikia kipunda. Bibiye amemzidi Bwana maradufu katika ukosaji wa utu na udugu.

Maoni yetu ni kuwa mwandishi ameubadilisha msimamo wa kumtetea mwanamke kama kiumbe dhaifu na anayeonewa daima kwa sababu ya wakati. Wakatai akiandika riwaya na mashairi yake, hapakuwa na wanawake wengi madarakani kinyume na alipoanza kuandika tamthilia zake. Wakati huu wa kuandika tamthilia ya Pungwa (1988) tayari wamawake walikuwa wamepiga hatua kwa kushika nyadhifa mbali mbali uongozini. Wamepata vyeo vya juu serikalini, kwenye makampuni, vyuo na mashirika mbali mbali. Hivi sasa, ukweli wa tabia ya mwanamke mamlakani umeanza kujitokeza hadharani.

La muhimu zaidi ni kuwa unyonyaji na ukandimizaji ni ule ule na hauna jinsia: uwe wa mume au mke, unastahili kupingwa. Kwa hivyo, walio wengi wanapopambana ili kuleta hali sawa, wasisahau kukabiliana na mabibi wanyonyaji na wanyanyasaji kama Bibiye kwa kutumia wembe ule ule wanaomuelekezea Bwana. Yawe ni mapambano dhidi ya wadhalimu na wanyonyaji - wake kwa waume.

## 2.9. ***HITIMISHO***

Katika tamthilia ya Pungwa, mwandishi ametusawiria jamii iliyo na matatizo kama vile umaskini kwani wengi katika jamii wanatembea hata bila viatu kama tunavyoliona lile kundi la Simba. Kunao ukatili na udhalimu mwingi katika jamii; mambo ambayo yanaendelezwa na tabaka la juu linalowakilishwa na Bwana na Bibiye. Hawa wanatumia mbinu ya kuwafanya wengine wafilisike na hata kuwamaliza wengine kisiasa ili wao wanufaike. Ubinafsi pia ni tatizo linaloikumba jamii na ubinafsi huu umechanganyika na uroho na tamaa isiyokuwa na mwisho ya kutaka kulimbikiza mali, kuhodhi nyenzo zote za uzalishaji mali na kuihamisha faida yote na kwenda kuiweka katika mabenki ya Ulaya huku wananchi ambao ndio hutoa jasho kuizalisha ile mali hawafaidi chochote.

Ni vigumu mwandishi wa kazi yoyote ya Fasihi kutaja matatizo yote yanayoikumba jamii. Anachokifanya ni kuteua yale maswala anayoyaona kuwa ni nyeti na kuyashughulikia katika kazi yake ya sanaa. Kwa maoni yetu, matatizo ya umaskini, ukatili na ubinafsi yana uzito wa kuweza kushughulikiwa kwani ni maswala ya wakati wote na mahali mwote ulimwenguni.

Katika kufuatilia chanzo cha matatizo haya, ametuonyesha kuwa chanzo chake ni ubepari ambao ametutolea kukua kwake kihistoria na kutuonyesha namna ulivyoanza, sifa zake na jinsi ulivyokwepa nyakati hadi leo.

Baada ya kutoa historia yake, ameonyesha kuwa si vizuri kuendelea kuwalaumu mabepari wa nje huku tukiwasahau wale wa ndani hivyo basi ametambua makundi haya mawili kama chanzo cha matatizo yetu wa nje na wa ndani (kikwetu au kienyeji).

Kundi la wale wa kienyeji limewakilishwa na Bwana na Bibiye na lile la kigeni na Mr. Hans na Maganlal kama daraja ya kukutanisha haya mawili. Hawa ndio maadui na hawana budi kupigwa vita.

Vita hivi dhidi ya maadui wa wanyonge amevionyesha kwa mtazamo wa kimatabaka. Ameonyesha jinsi mapambano haya yameendelea kihistoria hadi kufikia mapinduzi ya umma

yanayoleta ujamaa. Kuanzia Mahoka aliyetaja tu matatizo hadi mzee Burhani ambaye aliyataja, kusema chanzo chake na kisha kutoa mapendekezo ya kuyatatulia matatizo hayo. Lakini kutotoa mbinu za kujikomboa kunafanya harakati zake kushindwa na pia ukweli kwamba yeye ameulizwa na watu wa tabaka lile lile analoliagua. Ananunuliwa na kujiunga na tabaka hili. Hatimaye hatua ya tatu inayowahusisha wote wanaonyanyaswa na kukandamizwa inafaulu kuleta mabadiliko ya kweli na yenye usawa.

Jamii mpya inayoundwa ni jamii yenye usawa kwani tayari wameanza kutumia mali ya Bwana na Bibiye kwa pamoja na kamwe hawawaruhusu kutwaa zile fedha za kigeni. Zitataifishwa na kuwa mali ya umma.

Hata hivyo, kunayo mambo kadha ambayo tunafikiri mwandishi alikuwa na upungufu wa namna ya kuyadhibiti.

Jambo la kwanza ni kwamba muungano wa wafanyakazi haukutiliwa maanani ipasavyo. Tulitarajia kuona wafanyakazi kama vile watumishi, walinzi na wengine wakija pamoja na kuunda jeshi la ukombozi lakini badala yake ni watamba na njia ambao ndio wako kwenye mstari wa mbele na wafanyakazi wanajiunga nao nyakati za mwisho. Ni maoni yetu kuwa alifanya hivi kwa sababu hapa Afrika, makundi ya wafanyakazi yaliyotwaa silaha na kupigania haki zao ni nadra sana. Mapinduzi yametokea ama kwa kupitia kwa jeshi au kupitia kwa vita vya kuvisiana ambapo wanaotumika zaidi ni hawa watamba-na-njia. Ameandika hali ilivyo katika nchi zetu na wala si kama ilivyotarajiwa na waliopendekeza itakavyokuwa vitabuni.

Upungufu mwingine ni kwamba makundi ya tabaka la chini yanaungana kwa urahisi sana kuliko mambo yalivyo katika hali halisi. Engeles (1970:104) anasema:-

> **Katika mapambano ya matabaka, makundi mengine ya tabaka la kati hayawezi kujiunga kabisa na wafanyakazi hadi wayakane mambo yote ya ubepari (TY).**

Kawaida huwa kuna uhasana baina ya makundi yote yanayopatikana katika tabaka hili la chini kinyume na tunavyodokezewa katika tamthilia ya **<u>Pungwa.</u>** Namna kundi la Simba

linavyoungana na walinzi na watumishi kama vile Kibwege, Mwamntabu na Kijuha ni kwa urahisi mno hivi kwamba hatupatiwi fursa ya kuona mikinzano iliyomo kwenye tabaka hili la chini. Mikinzano ya tabaka la juu ilidhihirishwa wazi kwani kuna kudidimiza, kusaga saga na kuwazika wapinzani wake Bwana. Upungufu tu ni kwenye ukweli huu kwamba muungano wa wanyonge ni kwa urahisi mno kuliko ilivyo katika hali halisi.

Aidha, amepuuzia kutuonyesha msimamo wa tabaka la kati la Mahoka na Burhani ambao mara wako upande wa wanaonyanyaswa na mara upande wa wanyanyasaji. Tulitarajia kuona hatima yao katika jamii hii mpya kwani watu kigeugeu kama hawa ni hatari katika jamii na wanaweza kuwa wasaliti hata kwa mapinduzi yenyewe.

Elimu na itikadi kwa wafanyakazi ni jambo ambalo halikushughulikiwa vilivyo na mwandishi. Hakuna mahali ambapo tumekuta wafanyakazi kama vile walinzi na watumishi wakifundishwa kuhusu haki zao na kutayarishwa kiitikadi ili kuyapokea mapinduzi na harakati zake. Hiki, kama tulivyoona katika sehemu ya madharia ni kiungo muhimu sana katika kuleta mabadiliko. Wanaambiwa tu kwamba adui wao ni mtu mwenye mashetani wakubwa wenye nguvu na mazingaombwe makubwa. Kuwa wingi, mbinu zao za kivita na umoja wao ndio silaha. Matayarisho haya ni kama yamepachikwa tu mchezoni kwani yanatokea tu kwa ghafla na kuelekea kileleni mwa mapinduzi.

sababu mojawapo labda mwandishi aliyafahamu maneno ya Engeles (1970:103) anayesema kuwa matayarisho haya huchukua muda Mrefu kisirisiri kabla ya kujitokeza hadharani kama mapambano halisi. Kwa vile mchezo huu unatarajiwa kuonyeshwa jukwaani, na utumike kama chombo cha kuelimishia jamii, basi Mohamed alistahili kuwashawishi kuwa yanawezekana kwa kuwaonyesha haya mapinduzi yanavyopangwa.

Udikteta wa Simba haukujitokeza katika jamii mpya ingawa udikteta wa wafanyakazi unaruhusiwa ili kuhakikisha kuwa mali imetaifishwa na ile ya mtu binafsi kutoweka kabisa. Baada ya hapa, tabaka la watawala litajimaliza lenyewe kwani hakutakuwa na umuhimu wake tena wala umuhimu wa serikali. Kuna uwezekano wa Simba kupenda madaraka hivi kwamba

akatae kutoka madarakani au kujiachisha kazi yeye mwenyewe. Ingawa Simba anasema kuwa hakuna mkubwa wala mdogo, kwamba wote ni wakubwa, bado anachukuliwa kama kiongozi na hivyo kuchukuwa ile nafasi ya tabaka lililoondolewa. Mwandishi hatupatii suluhisho la tatizo hili na hivyo basi jamii ya ujamaa iliyoundwa haijatimilika katika ukamilifu wake.

Aidha, Bwana naye anakubali kuicheza ile ngoma shingo upande na hatujui kama mawazo yake yatabadilika kabisa na kuwa ya kijamaa hata baada ya kucharazwa bakora. Kwa vile hatukumuona akitolewa mawazo haya kichwani, kuna uwezekano kuwa atazidi kutamani maisha yake ya jana na hivyo kutafuta tena mbinu za kuirejelea ile kazi yake na tabaka lake Ingawa hali ni tulivu kwa sasa lakini hatuna hakika kuwa itaendelea hivyo na kuwa mikinzano na mitafaruku ya matabaka sasa imekoma.

Dhana ya kupungwa ni dhana inayopatikana katika utamaduni wa waswahili naye mwandishi ameitumia kama mbinu ya kuwasilishia ujumbe wake. Mbinu hii imetumika kwa mafanakio makubwa kwa kuonyesha jinsi mashetani ambao ni mabepari wanavyoweza kututawala wakishirikiana na watawala wa nchi zetu. Suluhisho lake ni kupungwa na tumemuona Bwana akipungwa. Imani hii ya kupungwa imetumiwa kwa ajili ya kuendeleza maudhui na imefanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Hata hivyo, wanaoutazama mchezo huu wanaweza kutatizwa na imani hizi kwani sio wote walio waswahili na wale ambao hawajasoma utangulizi wanaweza wakatatizika. Kwa maana imani hii ya Pungwa itakuwa pingaminzi katika kuyaelewa maudhui.

Kuna mbinu ya sauti ambayo inatokea na hatuoni mwenye kuitoa sauti ile. Katika ukurasa wa kwanza kwa mfano, tunakutana na sauti ya mzuka. Huu ni ufanisi wa mwandishi kutumia mbinu vilivyo ili kuwasilisha ujumbe wake.

Sauti hii inawakilisha ubepari ambao hauwezi kufungamanishwa na mtu fulani wa mahali fulani. Sauti inaashiria kuwa ubepari ni wa kila mahali na kuwa si wa mtu mmoja au nchi moja kama vile sauti pia yaweza kutolewa na mtu yeyote.

Nyimbo na ngoma navyo vitatumika kuonyesha maisha katika jamii ambayo yanafuata mdundo fulani kuonyesha maisha yanavyoendelea katika jamii.

Mbinu nyingine aliyoitumia mwandishi ni ndoto. Ndoto imetumika kuonyesha namna viongozi kama Bwana wanavyoishi katika maisha ya ndotoni mbali na ukweli kuwa wenzao waliowazunguka wamedidimia katika umaskini. Kuna ndoto za maisha mema na pia wasiwasi juu ya hali ya mitafaruku katika jamii ni mambo yanayoelezwa vizuri sana kwa kutumia ndoto kama mbinu ya fasihi.

Wahusika nao wamepewa majina ya majazi ili kusimamia hali fulani au kundi fulani katika jamii na haya yamesaidia katika kuyasukuma maudhui mbele. Mwantabu, Kijuha, Kibwege, Mahoka, Bwana, Bibiye, Mzuka yote ni majazi.

Haya yatatosha kuonyesha kuwa mwandishi amefanikiwa katika mtindo wake ambao umemsaidia sana katika kuuweka ujumbe wake wazi. Mambo haya mawili - maudhui na mtindo yanaenda Sambamba.

Mbali na upungufu wa hapa na pale, tamthilia ya **Pungwa** imefaulu kwa kiasi kikubwa katika kuyaelezea maswala muhimu yanayoikumba jamii ya nchi zinazoendelea hivi leo.

## ***TANBIHI***

1. Hussein, E; 1971 — Mashetani, Oxford University Press, Nairobi, Mchezo huu ni jazanda kuhusu wakoloni, wakoloni mamboleo, na mabepari.

2. Ngugi wa Thiongo:1986 — "Writing Against Neo Colonialism" Katika Kirsten, H, (Mhariri) Criticism and Ideology Second Africa writers conference Bohcslangen, Stockholm, UK 96.

3. Marx, K; 1959 — Capital, Eastern, (Mhariri), Random House, New York. UK 324.

4.Kama nambari 2 hapo juu, UK 96

5. Kama nambari 1 hapo juu, UK 24

6. Fanon, F, 1969: — The Wretched of the Earth, Penguin Books, Middlesex, UK 141

7. Ngara, E, 1985: — Art and Ideology in the African Novel, Heinman, NairobiUK 21

8. Marx, K. — Kama nambari 3 juu UK 330

9. ------ — Kama nambari 1 UK 56. Maneno haya ni ya mhusika Juma katika tamthilia ya Mashetani

10. ------ — Kama nambari 3 hapo juu. UK 319

11. ------ Kama nambari 6 UK 192

12.Howe, I
(Mhariri) 1970: A handbook of socialistic thought Howe and Brydone (printers) ltd, London UK 104.

# *MAREJELEO*


1.Engeles, F, 1979 Katika Howe, I (Mhariri), A handbook of socialist Thought, Lowe & Brydone (printers) ltd, London.

2.Fanon, F, 1967 The wretched of the Earth, Penguin Books, Middlesex

3.Hussein, E, 1971 Mashetani, Oxford University Press, Nairobi.

4.Marx, K, 1959 Capital, Random House, New York.

5.Mohamed, S.A 1978 Asali Chungu, Shungwaya Publishers, Nairobi

1980 Utengano, Longman, Nairobi

1988 Pungwa, Longman, Nairobi

6.Ngara, E, 1985 Art And Ideology in the African Novel Heinman, Nairobi.

7.Ngugi wa Thiongo

1986: Writing Against New Colonialism Katika Kristen H., (Mhariri), Criticism and Ideology, Second African writers Conference, Bohslangen, Stockholm.

# SURA YA TATU

## 3.1. *MUHTASARI WA HADITHI YA KIVULI KINAISHI*

Tamthilia hii imejengeka kwa kutumia dhana ya Giningi ambayo mwandishi anaeleza kuwa ni makazi yaliyo ndani ya vichwa vya watu wa Ungunja na Pemba. Katika kutumia dhana hii ya Giningi, mwandishi anaonyesha maisha dhahiri katika jamii nyingi bila kujifunga katika jamii moja ingawa dhana hii imetokana na mazingira na utamaduni wa waswahili.

Mchezo huu unaanza katika mandhari na mazingira ya fasihi simulizi. Ni wakati wa jioni naye Bi Kizee amezingirwa na watoto wanaomwomba awatolee hadithi. Anapokataa kuwa hana hadithi, wanamshauri awatolee hadithi ya Giningi, jambo ambalo linaleta wasi wasi na woga kwa sababu jina hilo halitajwi vivi hivi hadharani. Wazee na utawala unaoongozwa na Bi Kirembwe wanaogopewa hivi kwamba hata kunongona ni shida. Kwa ajili hii, watoto wanashauri kuwa hadithi itolewe kimya kimya. Inavyoonekana kuanzia mwanzo ni kwamba watoto hawa si wa kawaida kwa sababu wana machachari na upekuzi mwingi.

Hadithi anayowalolea inahusu kijana mmoja itwaye Mtolewa ambaye amehitimu chuo kikuu na kujipatia digrii kadhaa. Anapoamua kutafuta kazi, anakumbana na ukweli wa nchi ya Giningi kuwa hawezi kupata kazi bila kwanza kutoa hongo au chai.

Anaamua kujiingiza katika shughuli hii chafu inayomwezesha kujiunga na kundi la watawala wa Giningi huku akifanya hivyo shingo upande. Katika UK 30, tunaambiwa kuwa Mtolewa anapita kwa furaha ya kujitia na kujilazimisha.

Pindi tu baada ya kujiunga na kundi la watawala, Mtolewa anagundua kuwa haruhusiwi kusema lolote analofikiria au kupendekeza hadi amepewa kibali cha kufanya hivyo. Sauti tu inayojulikana kuwa rasmi ni sauti ya Bi. Kirembwe ambaye ni kiongozi wa nchi ya Giningi. Wengine wote, akiwemo Mtolewa wamepewa unga wa ndere ili uwazuge akili wapate kuita

nyeupe kuwa ni nyeusi na nyeusi waiite nyeupe- yaani ukweli wauite uogno na uongo wautie kuwa ndio ukweli. Mtolewa anakubali kutumika kwa serikali kama hii kwa muda kwa ajili ya mahitaji yake.

Baadaye kupitia kujisaka na kujidadisi akili na kupitia sauti ya wazee wa alikotoka, anagundua kuwa ameingia kwenye kundi lisilostahili. Anaamua kuliasi tabaka la juu na kujiunga na kundi la wari ambao pia wanahasirika kwa utawala huu wa Bi. Kirembwe. Wao pia wanaasi na kumwendea Mtolewa ili awaonyeshe njia ya kujinasua na mtego huu walimoingizwa. Mtolewa anaamua kuwahamasisha na kuwafundisha haki zao na sasa wamegundua ukweli na wanaweza kuutofautisha ukweli kutoka uongo na porojo. Wanaiita nyeupe kuwa ni nyeupe na nyeusi inakuwa ni nyeusi kama ilivyo katika hali halisi.

Kwa ajili ya kazi hii mpya aliyoianza, Mtolewa sasa amekuwa hatari kwa kundi la wazee na Bi. Kirembwe na kama tulivyotarajia, anauawa. Kuuawa kwake hakusaidii lolote kwani aliyoyaanzisha sasa hayazuiliki kwani wari si wari tena wa Zamani, ni Wari wapya wanatambua ukweli na haki zao na jinsi ya kuzidai. Pamoja na hili, wale wafanyakazi kama vile wakulima, Walimu na Madaktari sasa wameanza kuuliza maswali na kutowajibika kazini. Kwa hivyo, hata kama Mtolewa ameangamizwa kwa kuuawa yale aliyoyaanzisha yataendelea kuishi kwani Wari na wafanyakazi wataendelea kuyatekeleza huku wakipigania haki zao. Ingawa amekufa lakini kivuli chake kitaendelea kuishi kupitia kwa wari na wafanyakazi. Kwa hivyo Kivuli Kinaishi.

## 3.2. ***<u>WAKATI NA MATATIZO YA JAMII YA GININGI</u>***

Tulidokeza kwa kifupi tu katika sura ya pili kuwa mojawapo ya sifa za nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti ni kuwa msanii aonyeshe ni jamii ya wakati upi anayoizungumzia na kisha aeleze matatizo yanayoikumba jamii ile kihistoria huku akizingatia uhalisia wake.

Mohamed (1980) akijitambulisha kama myakinifu anasema:-

> **Tungo zangu zinaibuka na hali halisi ya jamii lakini si jamii fulani finyu; Ila zinagubika jamii pana ya dunia yenye madhila na mateso kwa wanyonge na kibri kwa watukufu.**

Tunatarajia basi tamthilia ya Kivuli Kinaishi iibuke kutokana na hali halisi ya jamii na jamii ile iwekwe katika kipindi maalum kihistoria.

Jamii inayosawiriwa katika kivuli kinaishi ni jamii ya kisasa ambayo imekwisha jitawala. Kwa hakika miongo kadha imeshapita baada ya kujipatia uhuru. Isitoshe, jamii hii iliamua kufuata siasa ya ujamaa na kushauriwa waishi pamoja ili wapatiwe huduma bora na serikali kama vile matrekta, Zahanati na shule bora.

Nyerere (1968:249) anaelezea Azimio la Arusha na akatilia mkazo usawa na heshima za kibinadamu, kushirikiana mali inayotokana na juhudi za wananchi, na kazi kwa kila mtu ili unyonyaji ufutiliwe mbali. Ili kutekeleza haya kwa haraka na kwa urahisi, watu walipelekwa kwenye vijiji vya ujamaa ambapo waliishi kwa pamoja. Lakini haikupita muda Mrefu kabla ya watu kuanza kuuliza ahadi zile zote walizopewa na serikali zilishia wapi.

Kwa hivyo mwandishi anaelekea kuzungumzia jamii ya Tanzania baada ya Azimio la Arusha na baada ya kuishi kwenye vijiji vya ujamaa. Ingawa Azimio la Arusha lilitolewa mwaka wa 1967, halikutekelezwa hadi miaka ya sabini. Kwa hakika ni hadi 1974 ndipo wananchi waliamrishwa kuanzisha vijiji vya ujamaa. Baada ya vijiji vya ujamaa, mambo tena yakawa hobela hobela hadi 1977 wakati viongozi wa chama cha TANU walipoamua kujisaka na kuchukua Azimio kwa uzito zaidi na hivyo wakaibuka na jina jipya la chama - Chama Cha Mapinduzi (C.C.M). Lakini matendo ya viongozi hayakubadilika. Kilichobadilika ni jina la chama. Hali katika jamii haikuwa nafuu kwani viongozi waliendelea kuneemeka na wananchi wakaendelea na matatizo yao yaliyozidi. Siasa ya Chama Kimoja, ya kujitegemea na kufuta unyonyaji haikufaa chochote kwani ilikuwa maneno matupu.

Ilipofika mwaka wa 1985 wakati wa Nyerere "kung'atuka", hali ilikuwa mbaya zaidi hata kuliko ilivyokuwa kabla ya Azimio la Arusha. Watu walikuwa wameanza kuuliza maswali hadharani na wengine kutambua kuwa viongozi hawakuwa wanaujamaa kama walivyotangaza kupita vipasa sauti mikutanoni, redioni na hata kwenye magazeti.

Kivuli Kinaishi inajihusisha na jamii ya Tanzania baada ya Azimio la Arusha na hasa baadya ya vijiji vya ujamaa vilivyoshika kasi mwaka wa 1974 na kuendelea. Mwanaginingi 1 anatudokezea haya vizuri sana anaposema:

> **MWANAGININGI I:**
> **Lakini tuliambiwa ..tuli.. tuliambiwa tutapewa matrekta kuburuga eneo kubwa kama tutaishi pamoja ... na sasa tuliishi pamoja, pia tuliambiwa tutaletewa mbolea za kizungu, hatukuletewa kumwangalia..(UK 18)**.

Ni wakati huu ndipo Nyerere alikuja na "Kilimo cha kufa na Kupona" na tunamuona Mwanaginingi I akiongezea:

**MWANAGININGI I:**

> **Samahani.. lakini.. nilifanya kazi kubwa mkuu wa wakuu.. nilifanya kazi kama punda (anazidi kutetema)... kama buldoza. (UK 19)**

Maelezo haya yanaonyesha vile wakulima mashambani walivyoagizwa kuishi pamoja kwa ahadi mzomzo na hatimaye kuulizwa kufanya kazi kufa na kupona ilipodhihirika kuwa zile ahadi zilikuwa ngumu kutekeleza. Ndipo serikali ikajificha katika siasa ya kujitegemea ili kuficha ukweli wa kushindwa kwake kutekeleza ahadi walizozitoa. Hali ni mbaya hivi kwamba waalimu hawana hata chaki darasani, madaftari wala viti vya kukalia hamna. Madaktari nao hawana hata madawa ya kimsingi wala vyombo vya pima pima na mengineyo. Kila wanapouliza wanaambiwa wajitegemee. Hii ndiyo jamii anayoisawiri S.A. Mohamed.

Lakini mwandishi hakujikita katika jamii finyu ya Tanzania bali ameshughulikia mataifa mengi

ya bara la Afrika hasa mataifa yaliyoanzisha ujamaa na siasa ya kujitegemea huku yakizingatia mfumo wa chama kimoja. Mtangazaji anamwita Bi. Kirembwe Mama na Baba yaani Mama upande na Baba wakati mmoja, nao wasichana wanamwita "Mama wa mama na baba wababa!"

Hili linatukumbusha wakati wa enzi ya chama kimoja nchini kenya wakati chama kilichotawala kilipopewa jina lilo hilo kuwa KANU ni baba na mama wa taifa la Kenya. Jina hili lilifanyiwa kejeli na wapinzani wa serikali na vyombo vya habari visivyokuwa vya serikali kuanzia mwaka wa 1990 wakati upinnzani ulikuwa umepamba moto. Kuna nchi nyingi za kiafrika ambazo zilikuwa chini ya utawala wa chama kimoja wakati huu mbali na Kenya na Tanzania. Nchi kama vile Malawi, Ethiopia, Ivory Coast na nyingine nyingi zinajumlishwa hapa. Kumbuka mwandishi ameshatuonya kuwa kazi zake hazishughulikii jamii moja finyu. Jamii kama vile Tanzania inatumika tu kama kielelezo kwani matatizo anayoyajadili na hali ya nchi kwa jumla inafanana na ile ya nchi nyinginezo.

Tungelipenda kumaliza sehemu hii kwa kuyataja matatizo yanayojitokeza katika jamii kama anavyoyaona mwandishi ili kuona kama ameyatambua na kuyaelewa vilivyo. Tutajadili kwa kinaga ubaga matatizo haya na chanzo chake katika sehemu zinazofuata.

Tatizo la kwanza ni utawala wa kiimla ambapo Mtu mmoja anatawala na sauti yake inakuwa kama sheria. Katika kuuendelea mfumo huu, dhana ya chama kimoja huzuliwa na kutekelezwa. Mfumo huu ndio unaotumika kuitawala Giningi. Aidha, kuna Unyonyaji na ufisadi mwingi katika nchi ya Giningi jambo ambalo linakubakika na kufanywa halali. Haramu hii imefanywa halali hivi kwamba ikiwa haushiriki, basi unaonekana kuwa wewe ndiye mwehu na mwenye akili pungwani.

Utawala huu wa kiimla huzusha tatizo lingine la ukatili na uhasama ambapo kuna kuuawa na kuangamiza wapinzani ama wale wenye mawazo yanayotofautiana na yale ya kiongozi.

Tatizo la Propaganda limejitokeza hivi kwamba elimu sasa imekuwa propaganda na kila njia

inatumiwa ili kuwazuga watu akili wasiweze kutambua matatizo yao, au wakiyatambua, wasisema bali wajifanye kuwa kila kitu ni shwari.

Mwisho, kunalo tatizo la wasomi kutotekeleza wajibu wao kwa jamii inayowategemea. Wanataka kujinufaisha wao binafsi bila kujali hatima ya wale waliowainua au kule walikotoka. Haya basi ndiyo matatizo yanayojitokeza katika jamii ya Giningi na maoni yetu ni kwamba yana uzito wa kutosha kushughulikiwa kwani yanaathiri jamii nyingi za kiafrika na athari zake zinaendelea kusikika hadi leo.

## 3.3. *UTAWALA WA KIIMLA*

Katika tamthilia hii, S.A. Mohamed ameonyesha jinsi nchi zinazoendelezwa chini ya mfumo wa kibepari na ujamaa zinavyoendelezwa kwa utawala wa kiimla ambao ni utawala unaotumia mabavu ili uweze kutekeleza unyonyaji wake. Matokeo ya utawala kama huu ni dhuluma, ukandamizaji na mauaji.

Katika kueleza hali hii, Ngugi(1986:96) anasema kuwa tawala hizi mpya katika mataifa yaliyopata uhuru zilipigwa darubini na kubanwa kutoka sehemu mbili. Kwanza ikawa ni matakwa ya mabepari ambao walitaka maslahi yao yalindwe na pili upinzani kutoka kwa wananchi ambao waligundua kuwa walizidi kuogelea ndani ya umaskini na kuwa udhalimu na ugandamizaji kisiasa ulizidi badala ya kupungua. Wananchi walishuhudia hali ambayo tawala mpya zilitegemea mataifa ya nje ili ziendeleze uchumi wao, uporaji wa mali ya taifa na ukandamizaji kwa wale waliotaka kuuliza maana ya matendo haya. Kwa hivyo mtawala huyu mpya alifaidika maradufu - kutoa kwa mabepari wa nje ambao walimtuza na zawadi mara kwa mara ili akubaliane nao na pia kutoka kwa mali ya taifa ambayo aliipora bila ya kizuizi.

Mabepari wamehodhi nyenzo zote za uzalishaji mali na wanajitwalia sehemu kubwa ya faida inayotokana na mali wanayozalisha wafanyakazi. Jambo hili linathibitishwa na Mwanaginingi wa kwanza na Bawabu (I) wakati anapojaribu kumhonga Bawabu I kile kipeto cha mpunga na kuambiwa kuwa "huo ni mpunga wa wazee na wanausubiri" Hawezi hata kuweka akiba kwa ajili ya wanawe.

Picha tunayoipata hapa ni kuwa mabepari wa kigeni wanashirikiana na wale wa kienyeji ili kumpunja na kumwangamiza mnyonge. Ingawa Bi Kirembwe anawakilisha watawala wa kiimla hapa Afrika lakini anaweza pia kuwakilisha ubepari wa nje kwani katika ukurasa wa 34 Mtangazaji anaeleza sifa za Bi Kirembwe kuwa yeye ni wa enzi na utukufu, mbaki na mselea milele, hafi na wala hachoki. Sifa hii si ya binadamu wa kawaida bali inawakilisha jinsi ubepari unavyotukuzwa na ilivyo vigumu kuondoa, kuwa umekuweko tangu zamani za octovus na daima utaendelea kuwepo.

Ili kutekeleza unyonyaji huu kwa urahisi, Fanon (1967:132) anasema kuwa baada ya kugundua kuwa hawana uwezo wa kiuchumi na kuwa wamekosa mbinu za kuiunganisha jamii, watawala wapya walitahayari na kuanza kutetea tabaka lao na katika fufanya hivi wakazua dhana ya chama kimoja. Hii ilikuwa tu njia ya kuyalinda maslahi yao na kuzima sauti yoyote iliyotofautiana na yao. Ingelikuwa rahisi kuyatekeleza haya chini ya mfumo wa chama kimoja. Matokeo yake ni utawala wa kiimla, utawala wa Mtu mmoja ambaye ndiye kiongozi wa chama na tena kiongozi wa nchi. Alichokisema kikawa sheria na wengine wakatarajiwa kuimba wimbo huo huo. Mfumo huu ulizaa vibaraka ambao jukumu lao ni kusifu lolote lililosemwa na kiongozi liwe baya au zuri, la manufaa au upuuzi. Waliotofautiana na kiongozi kama huyu walichukuliwa kuwa maadui wa taifa zima na hivyo kuangamizwa.

Jamii ya Kivuli Kinaishi inatawaliwa na utawala kama huu. Inatawaliwa na chama kimoja na kuendeshwa kwa dhuluma, mauaji na ukandamizaji. Watu wamenyimwa uhuru wa kusema hivi kwamba hata hawaruhusiwi kujadili mawazo na kutoa maoni yao hadharani kwa sababu wanachelea kusikika wakiwa na maoni tofauti na yale ya Bi Kirembwe. Mawazo yake ndiyo mawazo rasmi na kila mtu ni sharti akubaliane naye. Yeye ni mjua yote na anayoyatamka ni sheria.

Hali hii ya kuchelea kusema hadharani ndiyo iliyosababisha Bi Kizee kuitoa ile hadithi kimya kimya kwani anawaeleza viongozi kuwa ni wenye nguvu, uwezo, pato, hasira kali, wanaotisha na wenye kukosa imani au huruma hasa wanapoingiliwa kwenye viambo vyao (UK 6).

Kwa sababu ya madaraka, uwezo wao kiuchumi na mamlaka basi wanakuwa wakali na watumiaji nguvu dhidi ya wapinzani wao.

Moja ya sifa muhimu za kipindi hiki cha utawala wa chama kimoja ni kwamba viongozi hawa walipandishwa hadhi na vibaraka wao hadi kufikia hatua ya kuamini kuwa wao ni watu mashuhuri na maalum katika jamii.. Wengi wao wakajiona kuwa wamemkaribia Mwenyezi Mungu kuwa hawawezi kufanya kosa katika maamuzi yao. Kwa mfano, nyimbo zilizotungwa

ili kumsifu Mwenyezi Mungu zilibadilishwa na pale palipokuwa na jina lake kukapachikwa lile la kiongozi lakini mahadhi, maneno na mdundo wa ngoma ukawa ule ule. Wakapewa majina ambayo kwa kawaida hupewa Mwenyezi Mungu. Wengine wakaitwa 'Mtukufu' huku baadhi yao wakijiita 'Rais wa maisha' Wengine wakaambiwa kuwa wapande 'Juu,Juu' Juu Zaidi!".

Kupanda juu ni kuelekea mbinguni na juu zaidi ni kupita mbinguni na kiti cha Mwenyezi. Hizi zote ni juhudi za viongozi hawa na vibaraka wao kutaka kuwafanya wanajamii waamini kuwa wao si watu wa kawaida.

Tunamwona Bi. Kirembwe akiitwa mwanasiasa nambari moja, hakimu nambari moja, yeye ndiye baba na mama. Anaitwa mfalme wa wafalme, jina ambalo lilipewa Masihi Issa na hii kwa hakika ni kukufuru.

Utawala wa kiimla kama tulivyokwishaona, haumruhusu mtu yeyote kutoa sauti iliyotofautiana na ile ya kiongozi. Haustahimili upinzani wa aina yoyote iwe ni kutoka ngazi ya viongozi au kwa mwananchi wa kawaida.

Katika ngazi ya uongozi wa kitaifa, wale wazee watatu wanapoonyesha nia ya kutaka kutoa maoni yao ya jinsi ya kuiendesha Giningi wanaingizwa mashakani ingawa ni mawazo mazuri na yenye manufaa kwa taifa zima. Wanaingia kwenye maangamizi kwa sababu maoni yao yametofautiana na yale ya Bi Kirembwe. Kufikiri kinyume na Bi. Kirembwe ni makosa na ukatili huu unadhihirika wanapoomba msamaha lakini Bi. Kirembwe anawakatalia mbali.

Wazee hawa wanawakilisha wale mawaziri na viongozi wengine ambao hujitokeza na mawazo tofauti na yale ya kiongozi wa kiimla kama Bi. Kirembwe. Kama ilivyotarajiwa, hawakupata msamaha wowote bali walielekezwa kaburini bila ya huruma. Viongozi kama hao hawastahimili upinzani wowote dhidi ya mawazo yao hata kama ni kwa manufaa ya umma au jamii. Fauka ya hayo, kiongozi anapoonekana kuwa sifa zake zinaelekea kupendwa na watu, basi anachukuliwa kuwa tishio kwa kiongozi na anaondolewa njiani haraka. Hili ndilo linalomzibu kijana Mtolewa na kumletea mashaka na maafa. Ukandmizaji dhidi ya wapinzani

haupo tu kwenye viongozi bali pia katika watu wa tabaka la chini. Hili linadhihirisha kuwepo kutoaminia kwa makundi yaliyo katika tabaka moja.

Makachero wamepachikwa miongoni mwa watu ili kupeleleza na kuona ni kidudumtu kipi kilicho na maoni tofauti na maoni 'rasmi' ambayo ni maoni ya kiongozi.

Wafanya kazi katika Giningi - wakulima (mwanaginingi I), waalimu (Mwanaginingi II) na Madaktari (Mwanaginingi III) hawaruhusiwi kusema lolote kuhusu matatizo yanazuia utekelezaji wa shughuli zao kazini. Kuna makachero wanaowakilishwa na Bawabu ambao hii ndiyo kazi yao ya kupeleleza na kuwaingiza ndani wenye maoni na tabia kama ya hawa watatu.

Kutajia serikali haya matatizo ni sawa na kuchochea na huu ni uhalifu unaotosha kukuelekeza kwenye maangamizi. Kujitegemea, kuajibika na uwazi ni mambo yanayoambiwa umma wakati wao wanaendelea kula mali ya taifa.

Sheria za nchi zilizo chini ya utawala wa kiimla ni sheria za ukatili, ukandamizaji na mapendeleo. Zinawakandamiza wanyonge huku wenye mali na madaraka wakiwa na uwezo wa kuinunua haki.

Kunatokea mambo matatu iwapo mnyonge atajikuta mbele ya vyombo vya sheria. Kwanza ni atiwe mzuga ili asitambue ukweli. Hili likishindwa afungiwe korokoroni asitangamane na wengine (Kizuizini) au afungiwe kifungo cha maisha au hata kunyongwa. Makosa kwa mfano yanayoelekeza wale wafanyakazi kukatwa mkono ni madogo mno.

Kwa upande mwingine, wale wenye makosa makubwa ya kukwepa kulipa kodi ambayo ni sawa na kosa la jinai wanawachiliwa waendelee na shughuli yao kwa vile wana uwezo wa kutoa hongo. Mwanaginingi IV na V wanaowakilisha wafanyabiashara wa ndani na wale wa masoko ya nje wanaachiliwa waendelee na shughuli zao na kusifiwa na Bawabu licha ya kwamba wanainyima nchi pato lake na hivyo kusababisha ukosefu wa vifaa muhimu katika utekelezaji wa shughuli za kijamii. Kodi hii ndiyo hutumiwa katika kulipa mishahara, kununua vifaa vya

shule na hospitali na mahitaji mengine. Kwa hivyo hii ni sheria inayotambua matabaka na yenye kutetea wale wa tabaka la juu na kunyanyasa watu wa tabaka la chini.

Kama tulivyoona, hali hii haikuathiri tu mfumo wa kibepari bali hata nchi zile zilizokuwa chini ya ujamaa.

> Ngara (1986:18) anasema:
> **Katika jamii yenye matabaka nguvu za kiuchumi hupatikana kwa tabaka tawala ambalo pia huhodhi nyenzo za uzalishaji mali (TY).**

Kwa hivyo, ni wazi kuwa utawala wa kiimla ni lazima katika nchi isiyo na usawa na yenye matatizo ya kiuchumi ambayo husababisha mitafaruku ya kimatabaka. Wanyonge wanazugwa akili kupitia mikutano ya siasa, shuleni na kupitia dini ili waiite nyeupe kuwa ni nyeusi na nyeusi iitwe nyeupe. Wauone ukweli na wajifanye kuwa hawauoni na wala wasiseme lolote.

Wanaojaribu kusema wanakiona cha mtema kuni wawe katika ngazi ya uongozi au wanaotawaliwa. Wote huishi kwa uoga na kutoaminiana kwa sababu hukumu kwa wanaokaidi na kukiuka hili ni kizuizini, kifungo cha maisha au hata kunyongwa.

## 3.4. *UFISADI NA UOZO WA JAMII*

Tabaka tawala haliwezi kuhodhi njia zote za uchumi na kuwa na mali nyingi kupita kiasi bila kutumia mbinu za ulaghai, udanganyifu na kulifumba macho lile tabaka la chini. Mfumo huu ni sharti utazaa ufisadi kwani hakuna binadamu wa kawaida anayekuwa na uwezo wa kuzalisha mali nyingi kiasi hicho kwa kutumia jasho lake. Mfumo huu huzaa na kuunga mkono mbinu za ufisadi ambazo hutumiwa ili kuwaibia maskini kwa minajili ya kuwatajirisha matajiri.

Mfumo huu huzaa hali ya ubinafsi na tamaa ya mali hivi kwamba kila mtu yu mbioni kujilimbikia zaidi na zaidi. Akisha jilimbikia mali ya kutosha, anatafuta madaraka ili ayatumie katika kuilinda mali ile.

Katika Kivuli Kinaishi, kuna tatizo hili la tamaa na upapiaji mali, ufisadi, ubinafsi na uzandiki mwingi. Sasa hali ya kuhongwa na kula mlungula inafanywa hadharani na watu kama vile Bawabu wanaotaka utajiri wa haraka. Kupitia kwa Mtolewa, tunaiona jamii ambayo kwa hakika imeoza ikaozeana.

> **MTOLEWA: Kuishi Giningi .. kulowea Giningi Katika raha zake ninazozisikia, katika anasa zake za ulafi na unywaji na wingi wa vitu, na burdani ya mwana kumkobea mama na binti kumkobea baba, na ustaarabu wake wa malezi yake ya kimaendeleo. (UK 14)**

Kile Mtolewa anachokiita raha za Giningi kwa hakika ni kinaya kwani ukweli wa mambo ni kwamba jamii hii ni yenye uozo mwingi. Kunao wachache kama vile Bi. Kirembwe, wazee, Bawabu na wafanyabiashara ambao wamelimbikiza mali na sasa kazi yao ni anasa, ulafi na unywaji katika vilabu, mahoteli na mikahawa mikubwa mikubwa. Kwa mfano tunaona Bi. Kirembwe na wezee wamechinja magombe mawili kwa ajili ya kusherehekea na kujistarehesha.

Pia huwa kuna vitu vingi madukani ingawa raia wa kawaida hawawezi kuvinunua kwani ni vya bei ghali nao hawana pesa. Wao wamebakia tu kuvimezea mate. Kwa upande mwingine, tabaka la juu ambalo limelimbikiza mali kwa njia za ufisadi, unyanganyaji na ujanja limejaa unafiki na uozo wa mama sukari kutafuta wavulana barubaru na wabichi ili kutosheleza ashiki zao za kimwili. Nao 'Baba sukari' hufukuzana na ndogo ndogo ambavyo ni visichana vinavyotoshana na binti zao ili waponde nao raha.

Kwa mfano, wazee wa Giningi wana mazoea ya kucheza na wari na visichana vidogovidogo kwenye mikutano ya hadhara na sherehe mbali mbali huku wakivimezea mate. Hivi ndivyo hali ilivyo katika nchi nyingi za Kiafrika wakati visichana vya shule na vyuo huenda kuwachezea wakubwa huku vikitingiza viuno vyao bila ya kujua hatari inayovikabili. Katika kuiweka hali hii kwa hali iliyo wazi, mwandishi anatoa maelezo yafuatayo:-

> **Wazee wamekaa vitini wanakunywa na kula na mbele yao wasichana wazuri wa kuteuliwa wanacheza sindimba. Wari wako pembeni, wameketi chini na kujiinamia. Hao hawali wala hawanywi chochote .. wazee wanatabasamu kwa mazungumzo ya kichini chini na mara kwa mara wanaonyeshana mschichana aliyetia fora huko nyuso zao sinapasua matamanio (Uk 55)**

Kwa wazee, haya ndiyo wanayaita 'Maisha Mema' ingawa kwa hakika ni maisha yaliyojaa uozo wa kijamii.

Ufisadi nao umegawika katika sehemu mbili. Kuna ufisadi katika kiwango cha kitaifa na ufisadi katika ngazi za chini au tabaka la chini katika jamii.

Katika kiwango cha viongozi au tabaka la juu, tunakutana na Mwanaginingi I anapotaka kumhonga Bawabu kile kipeto cha mpunga anaambiwa kuwa apite huo ni mpunga wa Giningi na kuwa wazee wanausubiri. Kwa hivyo cha Giningi ni cha wazee- Mali ya taifa ni mali ya watawala. Wazee wana sehemu yao katika faida hii inayotokana na jasho na bidii ya wakulima. Mali hii ndiyo wanayoitumia kuchinja magombe na kujistarehesha kwa mlo na vinywaji huku

Giningi ikiendelea kuzorota kielimu, kiafya na ukulima.

Mabawabu nao wanawanyanyasa na kuwaitisha hongo wafanyakazi ambao ni wenzao badala ya kuungana na kutetea haki zao.

Katika mfumo ambao usawa haupo, wale watendao makosa madogo madogo kwa ajili ya mahitaji ya lazima ndio hutiwa mbaroni, kushtakiwa na kufungwa ilhali wenye makosa makubwa huweza kununua haki zao. Kwa mfano mkulima anapopatikana na kipeto cha mpunga alichoweka kando kwa ajili ya wanawe na daktari akiwa na vidonge vitano akipelekea watoto wake wagonjwa wote wanakatwa mikono. Lakini wale wafanya biashara za ndani na wale wa kuagiza na kusafirisha nje ya nchi wanahepa kulipa kodi na wanatekeleza shughuli zao kimagendo. Wanafaulu bila matata kuibia serikali kiasi kikubwa cha pesa kwa sababu wanaweza kutoa hongo na kuwapa zawadi wanaolinda sheria kama vile mabawabu.

Makosa yao hayatambuliwi kuwa ni makosa ingawa kama tulivyotangulia kuona, makosa yao ndiyo husababisha kukosekana madawa, vifaa vya elimu na ukulima katika nchi ya Giningi. Katika hali halisi, ni kawaida wafanyabiashara hawa kuwapa maofisa wa forodhani, polisi na hata mahakimu mlungula ili kuwaziba midomo yao. Wachache wanafaidi huku walio wengi wakihasirika.

Ufisadi huu haukutambua wasomi kwani nao wamo chini ya mfumo ambao una uhaba wa kazi na watafutao kazi hulazimika kutoa chai ili wapate kazi. Kulingana na Rodney (1982:149) wanaotafuta kazi ni wengi kuliko nafasi za kazi na hili huwapa fursa wenye mali na waajiri kutengeneza faida kubwa zaidi kwani wanawalipa mshahara wanaoamua wao wenyewe.

Matatizo haya ya ufisadi na uozo wa jamii yana mwanzo wake katika ubepari ambao ni mfuno wenye matabaka. Tabaka la Bi. Kirembwe na Wazee wamehodhi mali ambayo wanaitumia katika anasa zao na shughuli chafu za kuharibu wasichana wa watu huku walio wengi hawana hata mahitaji muhimu ya kimsingi kama vile chakula, nyumba, madawa na vifaa vya shule. Mfumo huu anaouongoza Bi. Kirembwe pia umepewa mtazamo wa kihistoria kwani ni mfumo

mkogwe uliokuweko tangu enzi za hapo kale. Kutokana na Bi Kizee, palikuwa watu wenye mji nao, ambao pia walikuwa na uwezo na uluwa lakini kwa sababu ya kukiuka utu na desturi, matendo yao yalikuwa mabaya hivi kwamba jamii yao iliharibika kwa sababu ya wao kujifisidi wenyewe. Huu ni mtazamo wa kihistoria na umethibitishwa kwa matendo ya Bi. Kirembwe na Wenzake.

## 3.5 ***ELIMU KWA WANYONGE***

Elimu hutekeleza jukumu muhimu katika kuibadilisha hali mbaya ya kiuchumi na kisiasa inayoikumba jamii. Wanyonge kifedha ambao ndio wengi na wenye kunyanyaswa ni sharti wazinduliwe na waonyeshwe jamii ilivyo, matatizo hayo yafuatiliwe kihistoria. Hatimaye waonyeshwe wanalopaswa kutenda ili hali hiyo irekebishwe na kuboreshwa zaidi. Wanastahili kumfahamu adui wao ni yupi na jinsi ya kukabiliana naye.

Katika Kivuli Kinaishi, S.A. Mohamed ameonyesha elimu hii katika viwango vitatu. Kiwango cha kwanza ni elimu kwa vijana ambayo inaamua kutumia mbinu ya fasili similizi kama njia mojawapo ya kuelimishia. Mbinu hii ndiyo anayoitumia Bi. Kizee na ni muafaka hasa kwa jamii kama ya Giningi ambapo watu hawana hata uhuru wa kuongea.

Elimu kwa vijana hutiliwa mkazo sana kwani ndio wanajamii na wanamapinduzi wa kesho. Wao ndio matumaini na tegemeo la kesho. Mwandishi anaonyesha imani hii kwa vijana kwani ndio wanaotolewa ile hadithi ya kuzindua. Pia anaonyesha kuwa vijana hawa wasitengwe kwa ajili ya umri wao kwa kudhani kuwa hawatayaelewa mambo yaliyo katika jamii. Ndiyo sababu anawasawiri wale watoto alivyofanya.

Mtoto wa kwanza kwa mfano anasema kuwa wao pia wana haki ya kujua yote ili wajitayarishe na yajayo kesho, wayajue yajayo usoni. Kwa hivyo, vijana waelimishwe kuhusu maovu, udhalimu na maonevu yanayotendewa jamii na watawala walio wachache. Aidha, elimu hii kwa vijana inachukuwa mtazamo wa kihistoria kwani kutokana na Mtoto II tunapata maoni haya:-

**MTOTO II: Ah, sisi tunataka kujua tu; kujua jinsi ya kale yenu ilivyokuwa; leo yetu sisi sote ilivyo na kesho yetu itakuwaje.. nyinyi wazee ndio mnaotwambia hadithi ni nyenzo za kuelimishia hapa Afrika. (Uk 7)**

Ili waelewe matatizo ya leo ni sharti watafute chanzo chake katika miaka iliyopita na ili waigeuze leo iwe kesho bora ni sharti watambue jana makosa yalitokeaje na makosa yapi tuliyomo sasa na tuyaondoe vipi ili kesho iwe bora.

Kupitia kwa hadithi ya Mtolewa, wanagundua kuwa matatizo yao yametokana na viongozi wakatili, walafi na wahuni ambao walirithi mfumo wa kisiasa na kiuchumi unaoendeleza unyonyaji na ukandamizaji. Mchezo unapoelekea ukingoni, tunapata kuwa wale tuliowadhania kuwa ni watoto na hawataelewa sasa wanatoa maoni mazito sana kuhusu hadithi waliyotazama. Mtoto I anasema kuwa inatisha, Mtoto II kuwa inasikitisha, Mtoto III kuwa inakasirisha na Mtoto IV kuwa inakatisha tamaa. Hadithi hii imewatisha, ikawasikitisha, ikawakasirisha na ni mmoja tu aliyekatishwa tamaa na anakemewa na wenzake kuwa hiyo haifai. Hili ni kuonyesha kuwa hakuna haja ya kukata tamaa kwami kuna matumaini ya kesho. Watu wakikata tamaa huwa hawana ule moyo wa mapambano tena lakini wakisikitika, watishwe na ile hali, na wakasirike, basi wanaweza kuchukuwa hatua.

Elimu kwa vijana ni swala lililopewa kipaumbele na mwandishi na kuonyesha kuwa wasidharauliwe kuwa hawajafikia kiwango cha kuambiwa ukweli. Aidha, vijana kama kundi maalum katika jamii halina budi kushirikishwa kikamilifu katika harakati za kuleta mapinduzi yanayotarajiwa. Ni sharti washirikishwe kikamilifu kwenye mapambano dhidi ya mfumo dhalimu uliojaa unyonyaji.

Kunayo aina ya pili ya elimu ambayo inamfaidi mtu binafsi bila ya kuwajali wanajamii wenzake. Rodney (1982:239) anasema kuwa kulikuwa na mushikili katika elimu iliyotolewa na wakoloni kwani nia yao haikuwa kudumisha mfumo wa jamii iliyokuwepo wala kuleta mabadiliko kwa wenyeji. Nia yao kuu ilikuwa ni kuwatayarisha baadhi ya waafrika ambao

wangelitoa huduma za usaidizi katika ngazi za chini za utawala kama makarani, maakida na wanyampala. Mfumo wa elimu wa kikoloni ukawa ni mfumo wa kuwadhalilisha wenyeji kwa sababu haukuwapa nafasi ya kupanda ngazi kwani walikuwa na elimu duni. Wakoloni waliogopa kuwa wangelitumia ile elimu ya juu kudai haki na uhuru wao. Pia hawakutaka wajiunge na tabaka lao la juu.

Uhuru ulipokaribia, wakoloni waliwatwaa vijana wachache kwa haraka haraka na kuwapeleka Ulaya ambako walijiunga na vyuo vikuu vya huko kwa minajili ya kuwatayarisha ili waweze kushika madaraka mkoloni atakapoondoka. Elimu waliyoipata haikuwa na manufaa kwa jamii zao kwani ilizingatia hali na utamaduni wa Ulaya kuliko nchi tawaliwa. Waliporejea nyumbani, ikawa waliyofunzwa hayakuweza kuzifaidi chochote jamii zao isipokuwa wao wenyewe. Nchi zao zilipopata uhuru, wakarithi mfumo huu wa elimu na mabadiliko yoyote waliyoyafanya viongozi hawa wapya yakawa yanafanana na kule walikosomea kwani ndiyo waliyoyafahamu na kuyazoea. Mfumo huu ndio uliomtoa na kumvinyanga Mtolewa.

Yeye kama walivyo wasomi wengi katika nchi zinazoendelea ana tamaa ya kupata kazi na kufanikiwa maishani. Jambo hili linamlazimu kutoa hongo ili apate kazi kwani ndiyo hali ya kawaida siku hizi. Mfumo huu wa elimu uliwatayarisha vijana kupata kazi maofisini na kazi kubwa kubwa za utawala. Baadaye anapandishwa madaraka na kujiunga na kundi la watawala wa Giningi. Sharti moja la kujiunga ni kupeana bahasha na anafanya hivyo na kubakia bila raha isipokuwa ya kujitia. Hii ni ishara kuwa baadhi ya wasomi wamejikuta katika mkururo huu wa ufisadi kwa kukosa jingine kwani wanataka na wao wajikimu kimaisha. Mtolewa anaingia kwenye mdundo huu wa ngoma ya ufisadi shingo upande kwa sababu hana la kufanya.

Wasomi kama Mtolewa wanahitaji kujisaka wenyewe ili waondoe ukengeushi walio nao na pia kutambua jukumu lao katika jamii. Mtolewa anajisaka mawazo na nafsi yake ili aurekebishe mwenendo huu muovu. Kupitia kwa sauti ya wazee inayopitikia mawazoni mwake, anagundua kuwa ameusaliti umma, wazazi wake waliomzaa na kumlea, na wote waliomsomesha. Anawakilisha wasomi wengi wa nchi za kiafrika ambao umma uliwaamini na kuwategemea kuwa wao ndio watakaoleta nafuu baada ya kupata kisomo kitakachowawezesha kuhudumu

vema. Wengi wa wasomi hawa walitokana na jamii maskini lakini walipopata fursa ya kufanya kazi na kupandishwa madaraka, waliwasahau wale waliowaacha kwenye tabaka la chini.

Hata hivyo, ule ukweli kwamba Mtolewa ametoka kwa wenzake walio na hali duni haumpatii raha katika tabaka lake jipya. Jambo hili linamfanya aliasi tabaka lake jipya na kurudi alikotoka baada ya kuona maonevu na dhuluma wanazotendewa walio wengi.

Wasomi walioinuliwa kutokana na msaada wa umma hawana budi kurudi na kutoa msaada waliotarajiwa kuutoa ili kutatua matatizo yanayowakabili wale waliowainua. Wasiende kule juu na kusahau walikotoka. Huu utakuwa ni usaliti. Wanahitajika sana wawatumikie walio wengi. Jukumu lao kubwa ni kuwaelimisha walio wengi na kuwaunganisha ili wapate haki zao. Wanalolihitaji ni kuelimishwa na kuunganishwa ili wachukuwe hatua. Mtolewa analichukuwa jukumu hili la kuelimisha wari ili waiondoe kasumba ya unga wa ndere vichwani mwao, wapate kujua matatizo na chanzo chake na kuyataja hadharani. Kwa hivyo Mtolewa anaamua 'Kurudi' nyumbani yaani katika kulisaidia kundi lililomlea na kumkuza.

Kwa vile Bi. Kirembwe na Wazee walitumia elimu na siasa kuwapumbaza walio wengi, sasa wanahitaji elimu na siasa mpya ili wafumbuke macho na wazibuliwe masikio yao wapate kutambua na kusikia kweli; Nyeupe iitwe nyeupe na Nyeusi iitwe nyeusi; Amefaulu sana katika jambo hili kwani wari wamekataa kutulia tena.

Hii basi ndiyo elimu inayofaa jamii. Maoni yetu ni kuwa +ipenge,e hiki cha elimu kimeshughulikiwa ipasvyo kwenye tamthilia hii kuliko kilivyoshughulikiwa katika tamthilia yake ya Pungwa. Baada ya elimu hii ya kuzindua, tunatarajia kuona harakati za ukombozi kupamba moto katika jamii ya Giningi.

### 3.6 *HARAKATI ZA UKOMBOZI WA WANYONGE*

Baada ya kuona umuhimu wa elimu katika harakati za kuwatayarisha wanajamii ili wazindukane na walete mabadiliko ya kweli na yenye kuleta usawa, S.A Mohamed anashughulikia jambo jingine muhimu linaloona na hili nalo ni harakati zenyewe za kutaka kuleta ukombozi wa walio wengi na jinsi ya kuzitekeleza harakati hizi.

Katika jamii yenye matabaka kama ile ya Giningi, mitafaruku na mikinzano ya kijamii haikosekani. Hii ni kwa sababu walio na mali hujaribu kila mbinu ili wazidi kuihodhi ile mali na wasiokuwa na njia kumiliki chochote wakijaribu ili wapate fursa ya kujiruzuku. Mikinzano na mitafaruku hii huendelea hadi pale ambapo wanaoonewa huchukuwa hatua madhubuti za kuhibadilisha hali hii. Harakati hizi zinaendelea kwa muda hadi mapinduzi yanapojiri na hazitokei kwa ghafla au kwa sadfa.

Jamii ya Giningi imegawika kwenye matabaka mawili makuu. Tabaka la kwanza ni la Bi. Kirembwe na Wazee ambalo ndilo tabaka linlotawala na kuhodhi mali yote na nyenzo za kuizalishia mali ile. Kwa ajili ya tabia yao ya ufisadi na kufuja mali ya umma, wameamua kuwa wakali, wakatili na wakosa imani (wakosa utu) ambao wako tayari kuzitumia nguvu zao kisiasa na uwezo wao kifedha ili kumzima yeyote atakayewaingilia kwenye hii mali yao. Tabaka hili pia linajumisha wafanya biashara matajiri ambao hupata utajiri wao kwa udanganyifu.

Wakiwakilishwa na Mwanaginingi IV na Mwanaginingi V, watu hawa wanaendeleza ufisadi wa hali ya juu na kununua haki wanavyotaka. Hili ndilo tabaka la juu ambalo mali yote imo mikononi mwake.

Nalo tabaka la chini linawakilishwa na wafanyakazi kama vile Mwanaginingi I anayesimamia wakulima nchini, Mwanaginingi II anayewakilisha waalimu na Mwanaginingi III anayewakilisha madaktari. Kundi hili la wafanyakazi linanyonywa na kudharauliwa ajabu na tabaka la juu. Marx(1959:323) akigusia hali hii anasema:

**Mabepari wameivua hadhi kila taaluma na uataalamu wake ambao hapo awali walikuwa wakihwshimiwa sana. Wamewabadilisha madaktari, wnasheria, makasisi, waandishi na wansayansi na kuwaajiri na kuwaingiza katika kazi za kuajiriwa na kulipwa mishahara. (TY)**

Katika <u>kivuli Kinaishi</u>, tunaona makundi haya yakidharauliwa na kupatiwa shida na walinzi na mishahara wanyolipwa ni midogo mno.

Pia katika tabaka hili kuna kundi la wari na wasichana ambao hawalipwi chochote wala hata kuwa hawali. Hawa ni lile kundi la watamba-na-njia ambao ni kutoa starehe na vibarua kwa tabaka la juu. Kunalo pia kundi kati ambalo halijitambui liko wapi nalo ni kundi la Mabawabu. Hawako kwenye tabaka la wazee lakini pia wankataa kujitambulisha na lile tabaka la chini.

Hawa ndio hutumika ili kuwanyanyasa wenzao wa tabaka la chini. Wanaweza kuwakilisha makachero, polisi, jeshi na mahakimu ambao wanatumiwa na tabaka tawala ili kuwanyanyasa wale wa tabaka la chini.

Mbali na mitafaruku baina ya tabaka tawala na lile la chini, mitafaruru ambayo inadhihirishwa na mikinzano kati ya Bi. Kirembwe na wale wafanyi kazi watatu na pia kati ya wazee na wari, kunayo mitafaruku ya ndani mwa tabaka.

Katika tabaka tawala, Bi Kirembwe wanazozana na Mtolewa, Wazee watatu na hata Mtangazaji. Huu ni ushahidi tosha wa kuwepo kwa mzozo katika tabaka la juu.

Lile la chini nalo linazozana lenyewe kwa lenyewe wakati mabawabu wanapowaingiza wale wafanyakazi kwenye shida.

Mitafaruku hii ilianza na kuendelezwa na makundi mbali mbali katika tamthilia ya <u>Kivuli Kinaishi.</u> Watoto ndio wa kwanza kuonyesha hali ya mwamko wa kisiasa wakati walipomtaka Bi Kizee awatolee hadith ya Giningi. Kwa mara nyingine, wao ndio waliosababisha ile hadithi

ya Giningi kutolewa. Kama wasemavyo wenyewe, walitaka kujua ukweli wa maisha yanayowazunguka, historia ya mambo yaliyo katika jamii ya Giningi ilianzaje na linalopaswa kutendwa ili kuleta kesho yenye matumaini.

Baada ya mchezo tunaona kuwa sasa wameyafasiri mambo vyema na kuwa wamehamasishwa na kuhamaki vya kutosha na wako tayari kushiriki bila ya kukata tamaa ili waiunde jamii bora.

Si ajabu kuwa kundi la kwanza la kupata mwamko wa kisiasa ni vijana kwani Bwana Marx huwapa vijana nafasi kubwa sana katika utekelezaji wa mapinduzi haya. Pata vijana na jamii ya kesho itakuwa mikononi mwako.

Kundi la pili katika jamii linalopata mwamko wa kisiasa ni kundi la wafanyakazi. Wanaanzisha sauti za kutoridhika awali kabisa hata kabla makundi mengine katika jamii hawajazinduka kisiasa. Hii ni kwa sababu Marx (1959:330) anaamini kuwa ukombozi wa wafanyakazi utaletwa na wafanyakazi wenyewe. Hawa ndio watakaoleta hizi shughuli zao za kujikusanya pamoja kama tabaka na hatimaye kama chama cha kisiasa. Shughuli hizi zinatatizwa na mashindano yaliyoko baina ya wafanya kazi wenyewe.

Hali hii inadhihirika wazi mchezoni kupitia kwa mabawabu na wale wafanyikazi wengine (wakulima, waalimu na madaktari).
Harakati hizi zinaanza wakati hawa wafanyakazi wanapoanza kulalamika hadharani kuhusu hali ilivyo nchini mwao. Wanayataja matatizo yao na hata kutoa chanzo cha matatizo hayo bila kuogopa litakalotokea.

Mkulima kwa mfano anaona kuwa shida zake zimeletwa na serikali ambayo iliahidi mambo kadha kwa wakulima kama matrekta na mbolea, ahadi ambazo haikuzitekeleza. Amegundua kuwa tatizo si lake kama anavyodokeza Bawabu bali yeye alifanya kazi kipunda. Waalimu nao wanasema wazi kuwa matatizo yanayowakumba kazini ni viti vya kukalia wanafunzi na meza, Madaftari na vitabu vya kusoma hakuna, hakuna hata chaki za kuandikia, atlasi na rangi hamna na hata mabanda yenyewe yanaporomoka. Isitoshe, mshahara wake ni mdogo mno hivi

kwamba hata haumfikishi tarehe mbili. Nayo hali ya kiafya imezorota kweli kweli kwani kuna magonjwa ya malaria, kipindupindu, maradhi ya tumbo na mengineyo. Haya yamezidi kwa sababu mazingira wanamoishi wanajamii ni machafu, hali zao za maisha ni duni hivi kwamba hata hawezi kumudu lishe bora, mahitaji ya kimsingi ya matibabu hakuna- madawa hata ya msingi hayapo, vifaa vingine vya hospitali pia hakuna. Kwa hivyo pale ambapo neno Matatizo halikusikika mbeleni, sasa linatajwa hadharani, tena mbele ya Bawabu.

Hali hii ni kinyume na sera zilizowekwa na tawala mpya za kiafrika zilipojipatia uhuru na kusema kuwa majukumu yao yalikuwa dhidi ya maadui watatu - Njaa, Magonjwa na Ujinga. hawa ndio maadui wakubwa walioazimia kupambana nao lakini inaelekea kuwa wameshindwa kwani sasa kuna njaa zaidi, magonjwa zaidi na ujinga zaidi. Kwani shughuli hizi zimezorota badala ya kurekebishwa na kuimarika.

Kundi jingine lililoamka kisiasa ni kundi la wari ambao wanawakilisha vibarua, watumishi nyumbani na watamba-na-njia. Kundi hili linatambua kuwa linahasirika chini ya utawala wa Bi Kirembwe na linaamua kujiunga na Mtolewa ili awaunganishe na kuwafahamisha ni lipi la kutendwa zaidi.

Kundi la wasomi wazalendo linalowakilishwa na Mtolewa limeamua kuasi utawala uliopo na badala yake kujiunga na tabaka la chini ambalo ndilo lililowazaa, kuwalea na kuwakuza viongozi kama hao ingawa sasa wamepanda madaraka na kujiunga na tabaka la juu. Kwa kutumia Mtolewa, mwandishi anaonyesha umuhimu wa kiongozi atakayewaunganisha na kuwaongoza watu katika mapambano haya. Kuhusu jambo hili, Trostsky (1971:ii) anasema:-

> **Kwa wakati huo huo, hakuwezi kukatokea mapinduzi bila kiongozi wa wafanyakazi (TY).**

Kiongozi ni muhimu na Mtolewa anatambulika kutoa maongozi haya lakini wale anaowaongoza ni watamba-na-njia badala ya wafanyakazi. Said Ahmed Mohamed anaelekea kuunga makundi haya mkono maksudi kwani katika tamthilia ya <u>Pungwa</u>, walioleta mapinduzi

si wafanyakazi bali ni hawa hawa watamba na njia. Katika tamthilia hii, wanaoonyesha mori ya mapambano zaidi na ambao tayari wana kiongozi wao ni wari na wala si wafanyakazi. Tunaamini kuwa imani hii ya mwandishi inatokana na ukweli ulivyo hapa Afrika kwamba ni vigumu kulikutanisha na kuliunganisha kundi la maproletarii. Imetokea kuwa mapinduzi karibu yote yameletwa na jeshi ambalo ni sehemu tu ya tabaka la juu. Machache tu yamefaulu, na watamba-na-njia hawa ndio huwa rahisi kujiunga na vita vya kuvisia kama vile vya Yoweri Museveni wa Uganda. Msimamo huu ni tofauti na ule aliouchukuwa Marx kuhusu watamba-na-njia na wale wasio wafanyakazi kama tulivyotangulia kuona.

Kundi lingine linalojitambulisha na harakati hizi za mapambano ni lile la wazee watatu ambao wanawakilisha viongozi wazalendo. hata kama wamo katika tabaka la juu, bado wana hisia za Giningi yote kwa jumla na wana azma ya kuiona Giningi iliyoneemeka na kustawi zaidi. Wanatoa sauti zao huku wakidhani kuwa wanachangia katika maendeleo ya Giningi lakini wamechukuliwa kuwa wapinzani na maadui wa Bi. Kirembwe na wanaingia mashakani.

Kwa hivyo, S.A. Mohamed ameonyesha mapambano haya yalivyopamba moto si tu katika kundi la wafanyakazi bali katika wazalendo walio katika makundi yote ya jamii nzima kwa jumla.

Wazalendo hawa wanatoka kwenye makundi yote mawili - tabaka la juu na lile la chini. Ni maoni au falsafa ya mwandishi kuwa makundi yote yaliyo na uzalendo hayana budi kuungana na kushirikiana katika kuileta hali bora katika jamii.

Hali tunayokumbana nayo mwishoni mwa mchezo ni kuwa ingawa wengi wa wale waliyoanzisha harakati hizi wanauawa au kuangamizwa, hali walioianzisha haitoweki na badala yake ndiyo inazidi kupamba moto. Mtolewa na wale wazee watatu wanauawa, wale wafanyakazi wanakatwa mkono na wari wanajaribu kuzuiiliwa lakini hili halileti utulivu tena kwani jamii yote ya Giningi sasa imeshaamka. Kwa maneno ya Bi. Kirembwe mwenyewe, kila kitu pale Giningi sasa kimeharibika na anaona kuwa kimeharibiwa na Mtolewa ingawa Mtolewa anasema kuwa mambo yalianza kuharibika kitambo na sababu ni Bi. Kirembwe

mwenyewe.

Nidhamu na utii hakuna tena, kuna wimbi la fujo na zogo hivi kwamba waalimu hawakai shuleni tena, waganga wanakimbia wagonjwa, makuli hawana hamu ya kubeba mizigo bandarini tena, makarani hawawajibiki, na wari na wimbi la hadaa na unyang'anyi vimetapakaa kote nchini. Hii ni hali ya kuthibitisha kuwa Giningi sasa inadidimia na kuwa ni jamii inayokalia bomu na yaweza kulipuka wakati wowote.

Ingawa walioanzisha harakati hizi wamekufa na wengine kukatwa mikono, hali ya mambo waliyoiazinsha haitakufa na itaendelea kuishi. Kivuli cha haki na ukweli hakiwezi kuuawa.

Ingawa hatuyaoni mapinduzi yakitekelezwa mchezoni hali iliyopo inaashiria mageuzi kwani hata yule kigogo wa vigogo, Bi Kirembwe ameanza kutetemeka na kuogopa hali iliyopo.

Tungelipenda kumaliza kisehemu hiki kwa kusema kuwa mwandishi ametilia mkazo mbinu ya kutotii na kuasi serikali badala ya kutumia silaha. Hii ni moja ya mbinu za kuleta mageuzi na wala si lazima iwe mbinu ya kutumia silaha. Kwa hivyo kuna mbinu tatu

Mbinu ya uchaguzi ambako wawakilishi wa wafanyakazi huchaguliwa na kuenda bungeni na kuwatetea kutoka huko juu. Pia kuna uasi wa kitaifa ambapo watu wote hukataa kutii sheria na kukataa kulitumikia taifa au serikali dhalimu. Mwisho huwa kuna njia ya kutwaa silaha na kuingia msituni. Katika tamthilia hii ya **Kivuli Kinaishi**, msani amehiari kutumiwe mbinu ya maasi ya jamii nzima.

## 3:7 *UJAMAA - MATUMAINI YA KESHO*

Ingawa jamii mpya haikuundwa katika Kivuli Kinaishi, kunazo dalili kuwa jamii mpya iko mlangoni inakuja. Kupitia kwa zile sauti nyingi tunapata mawazo haya:-

**SAUTI NYINGI: (Kutoka nje ambako zinajongea ndani) Sisi ni vizazi**

> **vipya vya Giningi, Vizazi vya walioang'amua. Vizazi vya waliodidimia.. Sisi sasa tuna kinywa kipana..Tuna uwezo wa kuamua tunavyotaka, kuamu wenyewe.. kwa maslahi ya sote...Hatutachagizwa tena na uchawi, tunakuja.. tunakuja.. (UK 128)**

Sauti hii inawakilisha kundi la wengi na ambao ndio huunda tabaka la chini ndiyo sababu sauti zao zikawa nyingi. Kwa sababu ya wingi wao, wanamfanya hata Bi. Kirembwe atetemeke na kutambua kuwa siku zake zinahesabika na wakati si wake tena. Vizazi hivi ni vizazi vipya vya Giningi ambavyo vimepata ujasiri mpya ingawa jana viliangamizwa na kudidimizwa. Sasa wana kinywa kipana cha kupasa sauti yao kwa pamoja ili waamue wanavyotaka. Wanaamua wenyewe kwa maslahi ya wote ambayo inaashiria kuwepo kwa ujamaa katika jamii inayokuja.

Hata na wale watoto wamekataa kuwachia wakati utekeleze maamuzi yake. Wanaamua kuuathiri wakati badala ya wabakie tu wakisubiri wakati ulete mabadiliko yake. Jamii ikifika mahali ambapo ile ya Giningi imefika, huwa hatua inayofuatiwa ni hatua ya kuunda jamii mpya.

## *HITIMISHO*

Katika kazi hii ya Kivuli Kinaishi, mwandishi ameonyesha matatizo yanayoikumba jamii ya Tanzania baada ya Azimio la Arusha. Ingawa ametumia nchi kama vile Tanzania (nchi ambazo zilikuwa zimeanza kutekeleza siasa ya ujamaa), matatizo anayoyataja hayawezi kufungamanishwa na nchi moja tu. Ni matatizo yanayozikumba jamii nyingi katika bara la Afrika.

Kuna matatizo kama vile utawala wa kiimla unaoendelezwa kwa utawala wa chama kimoja ambao kwa hakika ni utawala wa mtu mmoja. Katika mfumo huu kuna ukatili na mauaji kwa yeyote aliye na sauti tofauti na ile ya kiongozi. Aidha unyonyaji na ufisadi ni mambo yaliyotapakaa jamii nzima. Kunayo elimu potovu na propaganda wanaowekewa watu vichwani. Hatimaye kuna matatizo ya wasomi kutotekeleza wajibu wao ipasvyo kwa wale walio wengi na waliowainua kupitia jasho lao. Kwa maoni yetu, haya ndiyo matatizo makuu yanayoikumba jamii ya Giningi na mengine yote yanaweza kuingizwa katika moja ya haya. Pia ni maoni yetu kuwa matatizo haya yana uzito na uhalisia katika jamii za kiafrika na yanapasa kutambuliwa na kushughulikiwa.

Katika tamthilia hii, mwandishi amepunguza makali yake dhidi ya ubepari wa nje na katika kutafuta chanzo cha matatizo haya, anawataja viongozi kama ndio chanzo cha matatizo. Tabia zao za ulafi ubinafsi, na unyonyaji ndiyo sababu ya matatizo haya. Hata ile sababu inayotolewa na Bi. Kirembwe kuwa wanaposafirisha vifaa vyao vinanunuliwa kwa bei duni na wapigapo makelele juu ya urari wa mizani ya mauzo na matumizi mabwana wakubwa wanaonunua hutia pamba masikioni, lakini ifikapo kuviuza vyao wavyuza kwa bei wanayoitaka, haichukuliwi kuwa ina uzito tena. Tunaufahamu ukweli ni kwamba Bi. Kirembwe ndiye hufuja mali kwa kuchinja magombe, kutwaa mpunga wa Giningi na uchumi wote kwa jumla ili wajinufaishe. Kwake msanii, tatizo ni viongozi.

Sababu hii inatukumbusha Nyeree alipokuwa akiwalaumu mabepari kwa ajili ya ujanja huu wa kuamua bidhaa zetu watulipe kwa bei ipi na vyao watuuzie kwa bei ipi. Tatizo ni mfumo

unaokosa usawa lakini unaongozwa na kutiliwa mbolea na viongozi wenyewe.

Mfumo huu ukiongozwa na viongozi wetu umeigawa jamii katika matabaka mawili hata kama baadhi ya nchi zinatangaza siasa na sera za Ujamaa, kuna Bi Kirembwe na Wazee katika tabaka la juu na wafanyakazi, wari, wasichana na mabawabu katika tabaka la chini. Huu ndio ukweli wa mambo katika jamii hii ya Giningi.

Tumeona pia kuwa elimu inyaotolewa ni elimu potovu ya kuwazuga watu akili na kuwajaza propaganda tele ili wasitambue matatizo yao wala kuona chanzo cha matatizo hayo. Kwa hivyo wanajamii na waliowengi wamehitaji elimu mpya ambayo wanapata kupitia kwa harakati kama za Bi Kizee akitumia mbinu ya fasihi similizi, Mtolewa akiwafundisha wari na wengine kama vile wafanyakazi wanaoyaona haya wenyewe. Elimu kwa vijana, wafanyakazi na makundi yote yanayonyanyaswa inatiliwa mkazo.

Elimu hii inafaulu kuwazindua na wanaanza kuwapinga wanyonyaji na wadhalimu. Wafanyakazi wameanza kuteta juu ya hali mbaya kazini mwao, wari wameanza kuwauliza wazee ukweli, makuli hawabebi mizigo bandarini tena. Inakuwa ni zogo na fujo moja kwa moja. Makundi mengine yanajiunga nao kama vile wasomi wazalendo wakiwakilishwa na Mtolewa na Wazee wanowakilisha tabaka la juu lakini lenye mtazamo wa maendeleo kwa wote. Kufikia hatua hii, kundi la wanaogandamizwa limeshaamka na hali si shwari tena. Tunachotarajia ni mapinduzi.

Tunadokezewa juu ya jamii itakayoundwa baada ya mapinduzi haya kuwa ni jamii ya ujamaa - yenye haki na usawa.

Ni dhahiri kuwa mwandishi ameyathibithi vilivyo na kuyaelewa matatizo yanayoikumba Giningi. Pia amepata chanzo cha matatizo haya kuwa ni uongozi mbaya. Amefaulu kutuonyeha jamii iliyogawika kimatabaka kukiwa na tabaka la juu na lile la chini. Katika kufanya hivyo, amejitambulisha na tabaka la wanyonge na walio wengi kwani ameelekea kuwaonea imani wafanyakazi, wari na wasichana wa Giningi.

Kama alivyofanya katika Pungwa, hakutilia tu mkazo juu ya mapinduzi yatakayohusisha wafanyakazi pekee bali ni makundi yote ya jamii yanayohasirika chini ya mfumo huu. Elimu na itikadi vimetolewa kwa wanajamii na watu kushauriwa wachukuwe hatua.

Ameonyesha pia kuwa moyo wa mapambano ndio unaohitajika hata kama watakaouanzisha watatokomea - mfano wa Mtolewa.

Tatizo tu la kazi hii ni kwamba ni ndefu mno kuliko ilivyo tamthilia ya kawaida ya kuonyeshwa jukwaani. Aidha, mwandishi ametumia hotuba ndefu ambazo hutatiza ujumbe kueleweka na pia wakati wa uigizaji. Hotuba kama zile za Bi Kirembwe ni ndefu mno na inafaa zaidi katika riwaya kuliko tamthilia. Athari za uandishi wake wa riwaya hazikujificha katika tamthilia hii. Licha ya haya, mchezo huu umefanikiwa pakubwa hasa katika upande wa maudhui na usawiri wa wahusika ambao husaidia katika uendelezaji wa maudhui.

## *TANBIHI*

**1** Mohamed,.S.A.1980 — Sikate Tamaa,Longman Nairobi, Katika sehemu yautangulizi.
- 1990: Kivuli Kinaishi, Oxford University Press, Nairobi

2. Nyerere, J.K. 1968: Freedom and Socialism, Oxford University ress, Nairobi uk. 249.

3. Ngugi wa Thiongo 1986 Writing Against Neo-Colonialism," Katika Krsten, H.P (Mhariri) Criticism and Teleology, Second African Writers Conference, Bohislamingens, Stockholm (uk. 96)

4. Fanon, F, 1967: The Wreched of the Earth, Penguin Books, Sussex, uk. 132

5. Ngara, E., 1985 Art and Ideology in the African Novel Heinman, Nairobi uk.

6. Rodney, W. 1982: <u>How Europe under-developed Afrika,</u> Howard University Press, Washington D.C. uk. 239.

7. Marx, K. 1959: <u>Capital,</u> Katika Eastmass, M., (Mhariri) Random house, New York, uk. 323

8. Trosky, L., 1971: <u>Literature and Revolution,</u> The University of Michigan Press, U.S.A. uk. ii

## ***MAREJELEO***


1. Fanon, F, 1967: The <u>Wreched of the Earth, Penguin</u> Books, Sussex, England

2. Marx, K. 1959: <u>Capital,</u> Eastman, M (Mhariri) Random house, New York,

3. Mohamed, S.A. 1980: <u>Sikate Tamaa,</u>Longman Publishers, Nairobi,

4. Ngara, E., 1985 <u>Art and Ideology in the African Novel</u> , Heinman, Nairobi

5. Ngugi wa Thiongo 1986 Writing Against Neo-Colonialism", Katika Krsten, H.P (Mhariri) <u>Criticism and Ideology,</u> Second African Writers Conference, Bohislamingens, Stockholm

6. Nyerere, J.K. 1968: <u>Freedom and Socialism,</u> Oxford University press, Nairobi

7. Rodney, W. 1982: <u>How Europe under-developed Africa,</u> Howard University Press, Washington D.C.

8. Trosky, L., 1971: <u>Literature and Revolution,</u> The University of Michigan Press, U.S.A.

# SURA YA NNE

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutajadili maudhui yanayojitokeza katika tamthilia ya tatu ya S.A. Mohamed aliyoichapisha mwaka wa 1995 na kuipa jina la Amezidi.

Tamthilia hii imeandikwa kwa ufundi wa hali ya juu sana hivi kwamba inawahitaji wahusika wawili tu ambao hujibadilisha badilisha ili kuonyesha hali mbali mbali katika jamii. Ametumia mbinu kama ile aliyoitumia mwandishi Fugard, A. alipoandika tamthilia yake ya The Blood knot. Alitumia wahusika wawili - Morris na Zachary.

Tamthilia hii ni juu ya vijana wawili Ame na Zidi wanaoonyesha hali ya umaskini mkubwa katikati ya watu wenye mali nyingi iliyowazunguka. Jamii yao ni jamii huru hapa Afrika na ilianza kujitawala kitambo kwani tayari sasa watu wamelimbikiza mali na kuna mabadiliko mengi.

Katika onyesho la kwanza, Ame na Zidi wanaonyesha hali ya umaskini kuonyesha kuwa wao ni kutoka tabaka la chini. Chakula chao kilichosalia sasa ni mhogo mmoja, tena uliovunda. Wakiumaliza huo, hawana tena namna nyingine ya kujipatia riziki yao. Na suruali wanazovaa zimeraruka makalioni na sasa mtu hawezi kutambua tena kama ni suruali au ghuba.

Umaskini wao ni mwingi hivi kwamba hata kisu cha kuumenyea ule mhogo hawana na wanaamua kutumia kucha zao. Kiberiti cha kuuchomea ule mhogo hawana na inawabidi waule ukiwa mbichi. Chakula chao ni kile ambacho hata wakitupiwa mbwa watakinusa tu na waende zao.

Hali hii inawalazimu kuomba msaada kutoka jumuiya ya Ulaya (EC) badala ya kungoja viongozi wao wafanye hivyo kwani hawakumbuki sababu wanaishi kwenye shibe na raha daima. Katika onyesho la pili, Ame na Zidi sasa wanaonyesha mchezo unaotokea ndotoni ili kuonyesha jinsi tabaka la juu linavyoishi maisha ya anasa huku wamezingirwa na watu waliojaa umaskini. Kupitia hawa vijana wawili ambao sasa wanawakilisha tabaka la juu, tunapitishwa katika hali zao nzuri za maisha. Nyumba

yao si nyumba bali ni kasri; ukubwa na mapambo yaliyomo ni ya kushangaza.

Kunayo masofa matatu ya kutoka Parisi, Ufaransa, meza, makabati, video, televisheni, simu, magari mawili aina ya MBW na Benzi. Matanda yao ni yale ya kujimwaya na moja linaliambia jenzake "songa huko". Chakula chao ni kitamu sana na nikingi ajabu. Ajabu ni kwamba, hawa watu hawapendi kazi ingawa wanalipwa mishahara minono, marupurupu na hata kuchukuwa hongo. Wanaamua kutoenda kazini maksudi na kusingizia ugonjwa na wanafanya mipango na daktari vuai awandikie cheti cha uongo nao watamlipa.

Katika onyesho la tatu tunaona jinsi ilivyo vigumu kwa maskini hata kuhifadhi wapenzi wao au familia zao. Mari anamkataa Zidi kwani haoni chochote cha kumweka na hawezi kuishi kwa ndoto za maisha mazuri. Mari ni mmoja wa wale wanataka maisha ya anasa na starehe bila kujali yatatoka wapi. Utajiri wa tabaka la chini ni kama kichekesho kwani hautoshi chochote.

Onyesho la nne latuonyesha hali ya elimu ilivyo chini ya mfumo uliorithiwa kutoka kwa wakoloni. Ni elimu isiyoweza kuyatatua matatizo yaliyopo kwani haiwezi hata kusaidia kuunda nyambizi ingawa wanafunzwa juu ya 'Archimides Principle' inayoeleza jinsi nyambizi inayvyoweza kuundwa. Wanafunzi na Waalimu wao wanaamua kuudadisi mfumo huu wa elimu na wanajitokeza na mfumo mpya unaotambua ukweli wa jamii ulivyo.

Onyesho la tano linaonyesha mambo yanayotendeka maofisini wanavyofanya viongozi walio na wajibu wa kulinda mali ya umma na vile vile kutoa huduma kwa umma. Kule ofisini, Bosi akishirikiana na msaidizi wake wanaiba mali ya umma. Wanatayarisha orodha ndefu za uongo juu ya vitu walivyovinunua kwa bei maradufu. Pesa hizo wanagawana wenyewe kwa wenyewe na hili linatudokezea alikotoa ile mali ya kununua masofa kutoka Paris.

Katika onyesho la sita, mkaguzi wa hesabu ya mali ya umma anakuja na badala ya atekeleze wajibu wake, anaamua kujiunga na Bosi na wanageuza hesabu za vitabu na kuchoma nyaraka na ofisi yote ili ushahidi usiwepo. Mkaguzi anapewa nusu milioni na kuburudishwa na anapitisha ripoti hiyo ya uongo.

Onyesho la saba laonyesha Mari ambaye alijaribu kupanda daraja akiwa sasa amerudi na kutaka kuolewa na Zidi lakini Zidi anakataa. Lakini wote wanaanza kujisaka na kugundua kuwa miti imemea miyoni mwao. Kwa Mari ni Msowera na kwa Zidi unaitwa mjinga. Wanaamua kujisaka, kuing'oa miti hii na kujitoa kwenye hili shimo.

Onyesho la nane linaonyesha matajiri wakifananishwa na umbu wanyonyaji. Kuna njaa, magonjwa, na ukame mwingi hadi wanaamua kuomba msaada na wanaletewa msaada wa paja la nyama kutoka EC. Msaada huu umeoza na unaleta madhara kuliko yale ya mwanzo kwani wanaumwa na tumbo baada ya kulitafuna lile paja bila kulipika.

Onyesho la tisa laonyesha jinsi nchi ya Amezidi inavyosherehekea siku yake ya uhuru kwa njia kuu. Wanawaalika wageni Laki Nne na kutumia shilingi milioni Arobaini kuwalisha. Hatutarajii kuona haya kwa nchi ambayo watu wake wanakufa kwa njaa na kukosa maji ya kunywa kwa miaka.

Onyesho la kumi linafananisha Afrika na kuzimu, yaani ahera. Zidi anakufa na kwenda ahera naye Ame anamfuata baadaye.

## 4:1 ***<u>MATATIZO YA AMEZIDI NA CHANZO CHAKE</u>***

Jamii ya Amezidi ni jamii ya kiafrika ambayo imeingizwa kwenye shida na viongozi wake. Ni jamii huru inayojitawala lakini ambayo wananchi wa kawaida wanaendelea kudidimia na kuingia katika umaskini mkubwa kwa ajili ya matendo ya viongozi wao.

Kwa hivyo, tatizo la kwanza ni umaskini ambao umesambaa kila mahali hasa kwa tabaka la chini ambalo halijiwezi kifedha. Mfumo wa elimu usioifaa jamii ni tatizo lingine katika jamii hii ya Amezidi. Ufisadi nao umesambaa katika jamii hiyo kama ndui. Hali imezorota kwa sababu ya vitendo hivi vya kuifisidi. Aidha, uajibikaji kazini haupo tena ila kila mtu anajitakia mema bila ya kujali ile mali aliyopewa kuilinda kwa niaba ya umma. Kufungamana na hili ni tatizo la uharibifu wa mali ya umma bila kujali kwani wanadai kuwa ni mali ya umma, mali isiyo na mwenyewe.

Matatizo haya yamewekwa wazi na tena kwa njia sahili hivi kwamba kila mtazamaji au msomaji anaweza kuyapata. Tamthilia hii ni tofauti na zile nyingine mbili zilizotangulia (Pungwa na Kivuli Kinaishi) kwani matendo, lugha pamoja na wahusika si tata na kila msomaji au mtazamaji anayaona wazi yanayotendeka. Ni maoni ya tasnifu hii kuwa msanii alitaka ujumbe huu uwafikie wengi hata wasiokuwa na ujuzi wa kutosha wa fasihi wala si kwa wasomi au wahakiki peke yao.

Matatizo haya ni ya kweli na wazi katika jamii nyingi za Afrika na badala ya kupungua ndiyo kwanza yamezidi.

## 4:2 **UMASKINI**

Umaskini ni zao la mfumo ambao wachache wamehodhi nyenzo zote za uzalishaji mali huku walio wengi hawana chochote isipokua nguvu zao wanazoziuza kwa wale watakaozihitaji ili walipwe mshahara kidogo utakaowasaidia kuyakimu mahitaji yao. Mashamba, viwanda na mali yote ya taifa huwa vimo mikononi mwa hawa wachache ambao hutumia serikali na sheria za nchi kama vyombo vya kuilinda ile mali isinyakuliwe na walio wengi.
Marx (1963:81) anasema:

> **Ili wajikimu kwamahitaji yao, wasionacho hulazimika kutoa huduma kwa wenye-nacho hivyo basi kuwategemea kimaisha (TY).**

Marx anaendelea kusema kuwa kadiri watu hawa wanavyolipwa mishahara midogo ndivyo wanavyozidi kufukarika zaidi na kwa ajili ya wingi wao hawana jingine isipokuwa kukubali watakachopewa. Haja kubwa ya mabepari ni faida ambayo inatokana na utoaji wa bidhaa nyingi, kuziuza kwa bei wanayoitaka na kisha kuwalipa wafanya kazi mishahara wanayoitaka wao. Kwa hivyo, umaskini unakuwa ni matokeo ya mfumo wa kijamii usiotambua usawa.

Katita nchi inayoendeshwa kwa misingi ya kibepari, kama tulivyokwisha ona, huwa na umaskini mwingi unaodhihirika kupitia njaa, ufukara na ukosefu wa kazi. Hii ndiyo hali tunayokumbana nayo katika tamthilia ya Amezidi.

Wale vijana wawili, Ame na Zidi wanaishi katika umaskini mwingi. Chakula chao cha mwisho ni mhogo, tena mhogo uliovunda. Hawana kisu, cha kuumenyea ule mhogo na wanaamua kutumia kucha zao. Sababu wanayatoa kuwa kisu kile hakijaagiziwa kutoka Marekani ni kufunika ule ukweli kuwa hawawezi kukimudu. Hata kiberiti kinawakosa na wanaamua kula ule mhogo huku ukiwa bado mbichi. Hiki chakula chao ni kibaya hivi kwamba hata ukimtupia mbwa, atakitazama, anuse na aende zake.

Mavazi yao yanaonyesha umaskini huu. Suruali zao zimeraruka makalioni na sasa mtu hawezi kujua kama ni suruali au ghuba.

Hali hii inazorota zaidi wakati ukame unapokuja na hawa vijana maskini wanaamua kupeleka maombi ya msaada kutoka EC (Jumuia ya Ulaya). Wanajua kuwa wakiwaachia matajiri hawataomba kwani hawakuathirika hata kidogo na hali hii.

Zidi ni maskini hivi kwamba hata mpenzi wake Mari anamtoroka na kwenda kutafuta maisha mema kwingineko. Huu ni umaskini unaowakumba watu wa tabaka la chini katika nchi za kiafrika.

Aidha kuna umaskini katika kiwango cha kitaifa. Kupitia kwa redio, tunaarifiwa kuwa katika kijiji cha Fujo, maelfu kwa maelfu wanakufa kwa njaa kila siku na Redio ya Amezidi inatoa ukame wa miaka mingi kuwa ndiyo sababu. Lakini ukweli ni kuwa ukame unatumiwa kama kisingizio sababu mali ya umma ambayo ingetumiwa kuuasaidia umma sasa imeporwa na viongozi. Katika ule wimbo wa tajiri unaoimbwa darubini (uk..35), tunaona kuwa matajiri wenye tumbo kubwa wamekula makaa ya mawe, almasi, mabonge ya dhahabu, shaba gredi ya kwanza, mafuta ya petroli, chuma na 'uranium'!

Chanzo cha umaskini huu ni matajiri na viongozi ambao wamejinyakulia kila kitu kwa wizi na unyang'anyi na kuwaacha watu wa tabaka la chini wakitaabika. Hata kile kijiji cha Fujo ni jina la majazi ili kuonyesha kuwa ni fujo na huduma zao dhidi ya uchumi ambazo zinazua hali hii ya umaskini.

Tabia mbaya ya viongozi ya kupora na kufisidi uchumi zinazoendelezwa na viongozi kama vile Bosi na msaidizi wake ndicho chanzo cha umaskini katika nchi ya Amezidi. Mali nyingine iliporwa na mabepari wa nje ambao sasa wanatoa msaada usiofaa kitu. Ni misaada inayotoa harufu mbaya.

Misaada inayotolewa kwa nchi maskini huwambatana na masharti fulani ambayo ni sharti yatolewe kabala ya kutolewa misaada ile. Wakati mwingine, hasa wakati wa vita baridi, mabepari hawa walitaka wapewe ruhusa ya kuanzisha kituo cha kijeshi na waendelee na mazoezi yao katika ardhi ya nchi hizi kama sharti la kutoa ile misaada.

Na hii misaada inapowasili huwa hakuna uwezo wa kuitekeleza kwani hakuna ujuzi wowote. Hawana kiberiti, mafuta, kuni wala moto na wanaamua kulitafuna kwa meno yao. Hatuoni likiwafaidi wale maelfu wanaokufa katika kijiji cha fujo. Wakati mwingine, misaada hii huporwa na viongozi kabla hata ya kuwafikia wanaoihitaji.

Katika hali halisi, ile ile misaada inayotolewa ili kuwaruzuku wanaokufa kwa njaa huchukuliwa na kuporwa na viongozi. Misaada ya mahindi, pesa na madawa huuzwa na viongozi kabla ya kuwafikia wale wanaoihitaji.

Kwa hivyo S.A Mohamed ametuonyesha umaskini wa watu binafsi katika nchi kama vile Ame na Zidi lakini kupitia kwao, tunaonyeshwa umaskini wa nchi hizi jinsi ambavyo zinategemea misaada ambayo ina harufu mbaya na masharti mengine.

Chanzo cha umaskini huu ni viongozi na hili ndilo tatizo kubwa.

## 4:3 <u>**UAJIBIKAJI KAZINI**</u>

Kutoajibika kazini ni tatizo jingine linalosababisha hali hii ya umaskini katika nchi ya Amezidi. Viongozi wanao wajibu muhimu wa kutoa mafunzo, mwelekeo na pia kuwa mfano bora wa jinsi maendeleo ya taifa yanavyoletwa kwa haraka na kusababisha usawa kwa wote kwa kutoa huduma bila mapendeleo. Kwa hivyo, viongozi wanahitaji wawe na uajibikaji kwa umma katika nyadhifa zao mbali mbali wanazoshikilia serikalini, kwenye mashirika ya umma na makampuni nchini.

Nyerere (1967:1) anasema kuwa kusiwe na kiongozi wa chama au serikali ambaye anahusika na vitendo vya ubepari na umwinyi. Viongozi hawaruhusiwi kujilimbikizia mali na kujitajirisha haraka haraka

huku wakitumia madaraka yao. Wanapewa madaraka haya ili watumikie umma na wala sio wawe mabwana wakubwa.

Katika mwongozo uliotolewa kwa viongozi wa chama na serikali, hawakutakiwa wawe na zaidi ya kazi moja wala kuwa na biashara au mashamba ila kazi zao - kazi moja mtu moja. Hali kama hii ingesababisha kukosekana usawa kwani watumishi hawa wangelikuwa mabwana badala ya watumishi wa umma. Usawa ni jambo linalosisitizwa na nchi zinazoendelezwa kwa misingi ya kijamaa.

Viongozi wanakuwa kiungo muhimu katika kufanikisha ujamaa na maendeleo ya wananchi. Ogude (1982:11) anakubaliana na haya kwa kusema:

> **"Uongozi wa kimapinduzi ni muhimu na sharti upatikane" (TY).**

kwa ajili ya umuhimu huu unaopatiwa uongozi bora, viongozi wanapaswa kuwajibika na wawatumikie wale wanaowaajiri kwa kutoa kodi ili walipwe mishahara yao.

Viongozi tunaokumbana nao katika tamthilia ya Amezidi ni kinyume kabisa na matarajio ya vile tunavyotarajia kiongozi awe. Kupitia ule mchezo wa Ame na Zidi katika onyesho la pili, unaotokea ndotoni, tunapewa fursa ya kuona jinsi hawa viongozi wanavyoishi kwa maisha ya anasa na ulundikaji mali nyingi hata kuzidi mahitaji yao. Hiki ni kinyume cha matakwa ya usoshalisti ambayo yanahitaji kuwa watu walipwe na umma kulingana na mahitaji yao na tena watoe jasho kwa kufanya kazi kwa kulingana na uwezo wao ili wapate malipo halali.

Mishara yao pekee haiwezi kununua vitu vyote tunavyoona kule kasrini na hivyo lazima kuwe na njia zingine za kujipatia mali ile. Ni wazi kuwa wametumia nyadhifa zao vibaya ili kujinufaisha wao wenyewe bila kujali hatima ya umma wanotumikia ambao ndio mwajiri wao. Mwandishi ameendeleza wazo hili katika onyesho la tano tunapokutana na Bosi na msaidizi wake wakipanga namna ya kuibia umma mali yake. Wanafaulu kutokana na ushirikiano wao na wakaguzi wenye tamaa kwa hivyo, wale wanaotarajiwa wailinde mali ya umma ndio wanaoihujumu na hawawajibiki katika ulinzi huu.

Aidha, viongozi wanaamua kualika wageni laki nne katika sherehe za uhuru na kutumia shilingi milioni

Arobaini ili kuwastarehesha. Huku ni kutoajibika kwa mali hii kwani tunajua kuwa kuna watu wanaokufa kwa njaa na magonjwa nchini na hakuna haja ya kujigamba mbele ya wageni hawa ambao punde tu baada ya sherehe, viongozi hawa watakimbilia kule kule kwao ili kuomba misaada.

Watumishi hawa wa umma hawapendi kazi na watafanya kila juhudi hata za kudanganya na kusingizia ugonjwa ili wasiende kazini. Wanawahonga madaktari ili wawaandikie vyeti vya kupumzika majuma kadhaa. Ni walaghai na wazembe watakaotumia kila sababu ili waepuke kufanya kazi bali wakati wa kupokea mshahara watakuwa pale bila kukosa. Huku ni kuiba wakati wa umma na hii ni kutoajibika. Ugonjwa huu umetapakaa katika ngazi za viongozi na wale walio chini yao na kwa matendo kama haya, si ajabu kuwa kuna umaskini, njaa na magonjwa ya kila aina katika chi ya Amezidi kwani watu wanapokea mishahara bila kuzalisha mali.

Ruhumbika (1983:1) anayo mawazo kama haya kwani viongozi huchukua muda Mrefu wa kupanga sherehe ndefu na nyingi sizizokuwa na manufaa na hapo wakatumia pesa nyingi. Wanasahau huduma zao na hawajishughulishi na matendo yatakayozalisha mali.

Nchi maskini kama ile ya Amezidi haiwezi kuendelezwa vile inavyoendeleza mambo yake. Hili litawaletea janga na matatizo mengi.

Kwa hivyo, uajibikaji katika bara Afrika ni jambo la nadra na hii ndiyo sababu ya hali kuwa mbaya. Vyeo na madaraka ya viongozi vinatumika kwa manufaa yao binafsi huku nchi ikiendelea kudidimia. Mali na wakati wa umma vinaibiwa bila ya kujali. Wafanyakazi wote wa ngazi za juu na chini hawawajibiki tena na imekuwa sasa tatizo la kitaifa. Hii ndiyo hali halisi katika nchi zinazoendelea na si ajabu kuwa nchi hizi ni maskini.

## 4:4 <u>RUSHWA NA UFISADI KATIKA JAMII</u>

Rushwa na ufisadi ni matokeo ya jamii ya kibepari iliyogawika katika matabaka. Tabaka la juu linalomiliki mali na nyenzo za kuitolea mali ile, huwa limepata mali kwa njia za unyonyaji na kuwapunja wale walio maskini. Kama hawakuwahadaa na kuwanyang'anya mashamba yao, basi

waliwaibia jasho lao kwa kuwalipa mishahara duni huku wakijiwekea faida kubwa.

Viongozi, ambao wamo katika tabaka la juu, hutumia madaraka na uwezo wao ili kujilimbikizia mali kwa njia sizizo halali. Hujiingiza kwa njia za magendo, ufisadi na kuitisha hongo wakitumia vyeo vyao ili wapate kujitajirisha haraka. Wanapotajirika, hutumia mbinu zote ili walinde ile mali isije ikadaiwa na wenyewe, wale wa tabaka la chini ambao ndio wengi.

Rushwa na ufisadi vimejaa katika jamii ya Amezidi. Bosi amepanga njama ya kuiba mali ya umma kwa kutayarisha orodha ndefu za vitu vilivyonunuliwa ambavyo kwa hakika ni vya uongo. Wanachokifanya wakubwa kama hawa ni kushirikiana na makampuni yanayowauzia vitu na kukubaliana kuwa wawauzie kwa bei fulani na asilimia kumi au ishirini itakuwa yao. Ndiposa tunapata Bosi akiwa ameagiza vitu vingi kwa bei ambayo tunaitilia mashaka. Isitoshe vile vitu anavyoviagizia havina uhusiano wowote na uzalishaji mali ambayo italifanya taifa kutajirika.

Fenicha inayohitajika katika ofisi ya bosi itagharimu shilingi laki moja na nusu, Zulia la uajemi shilingi elfu kumi na sita, mapankaboi shilingi elfu thelathini na sita, meza ya 'executive' shilingi elfu tisa, simu mbili pamoja na uunganishaji na utiaji wake shilingi elfu kumi na tatu, na meza kibete cha kahawa shilingi elfu nne. Pesa hizi zote zinatumika kwa kuipamba ofisi ya Bosi huku shughuli nyingine muhimu kama vile vyakula na madawa ni haba mno katika nchi nzima. Huku ni kufuja pesa za umma na ni sawa na wizi na unyang'anyi.

Katika hali halisi, kuna makundi katika wizara au kampuni yanayoshirikiana katika uhalifu huu na kisha kutafuta njia za kuziba ushahidi wowote kwa kutoa stakabadhi za uongo. Bosi na msaidizi wake wanakubaliana kuwa bosi 'ampatie' asilimia kumi na pia pesa nyingine za kuweka siri pale ofisini. Kuhusiana na mkaguzi wa hesabu, Bosi hana wasi wasi kwani asemavyo, ni hali ya kumtuma mwizi kwenda kumshika mwizi mwingine.

Ajabu ni kwamba mabosi hawa "wanakula" lakini hawawaruhusu wengine walio chini yao 'kula' bali huwatolea onyo kali! Inakuwa kinaya kwamba Bosi anawaonya wafanyakazi walio na mtindo wa kudokoadokoa fedha za taifa, mali ya umma ambayo ni mali ya wananchi, huku wengine wanatumia

wizi wa kalamu. Lakini tujuavyo, Bosi na msaidizi ndio hutumia vitendo hivi na wao ndio wezi nambari moja. Wao hujifanya wakali wanapoulizwa kujibu maswali na mara nyingi hawawaruhusu walio chini yao kuwauliza maswali yoyote kwa uoga kuwa huenda wanayafahamu madhambi yao na watayaleta hadharani.

Mkaguzi wa hesabu anapokuja, huwa amepangiwa 'mazuri' yanayomsubiri. Anapewa burudani kwa vinywaji na mlo na kisha kuandikiwa hundi yake ili anyamazishe mdomo wake iwapo atagundua kosa lolote pale. Kwa mfano, mkaguzi anapogundua kuwa kuna kasoro ya shilingi milioni moja, anaitisha hongo ya nusu bin nusu; yaani, wagawane pesa hizo nusu kwa nusu ili Bosi abakie na nusu milioni naye mkaguzi aende na ile nusu nyingine. Lakini tayari Bosi ameshaitafuna ile milioni moja na kuimaliza. Sasa inambidi achote* nyingine kutoka mali ya umma na baadaye wanazichoma nyaraka baada ya kupatiwa cheki au hundi yake. Wanamalizia kutia moto nyaraka na ofisi nzima ili kusiwe na ushahidi wowote.

Jambo hili linatukumbusha wakati wa ushuru uliotozwa magari barabarani nchini Kenya. Katika stesheni za ushuru huu kule kule barabarani, kuliwahi kutokea mioto ya mara kwa mara, nyaraka zote kuungua na hivyo wasijue idadi kamili ya pesa zilizokusanywa! Mabasi na malori yalinunuliwa kutokana na pesa hizi kwani ni ajabu karani wa serikali ambaye mshahara wake ni shilingi elfu nne kununua lori ya shilingi milioni nne kwa muda wa mwaka mmoj! Hii ndiyo hali halisi katika nchi za kiafrika kwani kila mtu yu mbioni kujitajirisha bora tu anayo fursa ya kujinyakulia. Hajali kama mali ile ni ya umma na kuwa kitendo chake kitawanyima wengine huduma muhimu.

Wafisadi na walaghai hawa hawaishii tu kupora mali ya taifa bali hata misaada inayotolewa baada ya wao kuuzorotesha uchumi wa taifa pia inaporwa. Ame na Zidi wanaling'ang'ania lile paja la nyama lililotokea EC (European Community) na kisha kukubali kugawana wenyewe kwa wenyewe bila kuwakumbuka wengine.

Katika sherehe kama zile za kusherehekea uhuru, viongozi wanaamua kualika wageni laki nne na kutumia shilingi milioni arobaini. Hii ni kutafuta tu njia ya kupora mali kwani wanafahamu kwamba fursa kama hii hutokea kuwa na manufaa kwao maana ndio wanaosimamia mipango yote ya sherehe -

bora tu kuwe na stakabadhi na nyaraka za kudhibitisha kuwa pesa zilitumika na kuzipata nyaraka kama hizi si kazi ngumu.

Tamaa ya kujipatia mali na utajiri wa haraka ni mambo yanayopatikana katika jamii au nchi nyingi za kiafrika na wengi wa viongogi hujiingiza katika shughuli chafu za ufisadi na rushwa ili kufikia lengo lao la kulimbikiza mali. Mambo haya huwa ni matunda ya mfumo wa kibepari ambao hutilia mkazo mali ya mtu binafsi na hivyo kuendeleza ubinafsi badala ya ujamaa. Maovu haya yote yanatokana na mfumo wa kisiasa na kiuchumi usiotambua usawa, haki na ujamaa.

## 4:5 <u>ELIMU KWA JAMII</u>

Kama tulivyokwishasema katika sura zilizotangulia, elimu ni jambo linalotiliwa mkazo kwani wanajamii wanahitaji kuelimishwa ili watambue haki zao, wazidai na kisha wazihifadhi. Marx (1959:323) anasema.

> **Historia ya mawazo na fikira inathibitisha kuwa mawazo yanayotolewa wakati wowote ule yanaambatana na mfumo uliopo. Mawazo ya kipindi chochote kile yamekuwa ni mawazo ya utawala wa wakati huo. (TY).**

Kwa hivyo, mfumo wa elimu uliopo katika jamii ya kibepari umejaa mawazo ya kibepari na hauna budi kubadilishwa. Mwandishi anatakiwa aupige mfumo huu darubini ili pale palipo na mawazo ya kibwanyenye papandwe mawazo yanayoendeleza ujamaa.

Katika jamii ya Amezidi, elimu iliyopo inafundisha mambo ambayo hayaifai jamii kwa wakati ule. Tunakutana na mwalimu darasani akiwafundisha wanafunzi "Archimides Principle" ambayo haina uhusiano wa moja kwa moja na matatizo yanayoikumba jamii wakati huu. Hata mwalimu anapoandika, anaandika kama kichina au kijapani kuonyesha jinsi mfumo huu ulivyochanganyikiwa. Wanafunzi nao wanamuuliza mwalimu wao ni kwa nini baada ya kuikariri "Archimides Principle" kwa muda Mrefu hawajawahi kuunda hata nyambizi. Hii ni kinaya kwani 'Archimides Principle' yasema kuwa mwili wa kitu chochote uzamapo kwenye maji wote au sehemu yake utajaribu mwibuko nayo

nyambinzi huzama na kuibuka majini.

Wanashangaa ni kwa nini basi hawajaitumia kanuni hii ili waunde nyambizi. Mfumo huu hauwezi kuwafanya wanafunzi wajitegemee. Wanaendelea kuukebehi mfumo huu kwa kusema kuwa hawana haja ya kufikiria na kusumbua akili zao wakati ambapo wana watu kule Ulaya ambao watafikiria kwa niaba yao, wafanye utafiti na kisha waunde. Wao wataenda kununua kile kilichotengenezwa na kiko tayari kwani wana pesa za kutosha. Wanaona kuwa hii ni njia moja ya kuwatuma wazungu watufanyie kazi kwani mzungu naye alitutuma siku nyingi sana. Lakini tukumbukapo umaskini uliopo katika nchi ya Amezidi, mawazo kama haya ni ya kusikitisha. Kuagiza vitu ambavyo vinaweza kutengenezewa nchini ni kupoteza pesa ambazo zingetumika kwa mambo mengine. Elimu hii haiwatayarishi wanajamii kufikiria.

Wanafunzi na Waalimu wao wameanza kuukataa mfumo huu na wameanza kujishughulisha na mambo yanayoikumba jamii moja kwa moja. Wameanza kuwachunguza matajiri na kuona kuwa wao ndio chanzo cha matatizo ya Amezidi kama tunavyoona kwenye ule wimbo ulio ukurasa wa 35-36. Aidha wameanza kuidadisi jamii yao na sasa wamesikiza na kusoma hata vyombo vya habari na kupitia kwa redio wanagundua kuwa hali ni mbaya na kuwa maelfu kwa maelfu wanakufa njaa nchini mwao. Hawaonyeshi kuridhika na maelezo ya serikali ilipotoa sababu ya njaa kuwa ni ukame. Pia wanatambua njama na harufu mbaya inayoambatana na ile misaada inayotolewa na Marekani, Uingereza na Ufaransa. Wamegundua kuwa harufu hii mbaya inatoka nje na ndani mwa nchi ya Amezidi kwani mabepari pamoja na viongozi ndio maadui wakubwa wa nchi ya Amezidi.

Aidha, wamegundua kuwa kuna uhaba wa kazi na kuwa hakuna kazi baada ya masomo na kuwa vijijini wanaposhauriwa waende kulima hali ni mbaya sana kwani hakuna trekta, ng'ombe wamekufa, na hata mbolea hakuna. Elimu hii mpya imeanza kumulika matatizo ya jamii na kuona chanzo cha matatizo hayo.

Nyerere (1967:1) alieleza kwa marefu hali hii ya elimu ambayo ilirithiwa kutoka kwa wakoloni. Kama tulivyotangulia kuona, elimu hii, anasema Nyerere, haikupangwa na wakoloni ili kuwandaa vijana kulitumikia taifa lao bali ni kutimiza haja ya kuingiza desturi za kikoloni na kuwafunza watu

waitumikie nchi ya kikoloni. Walitaka kupata makarani, maofisa wa vyeo vya chini, wanyampala na walimu wa shule za msingi. Dini nazo zikatoa mafunzo ya kusoma na kuandika na elimu nyingine ili kuendeleza imani yao. Mawazo haya yanafanana na yale ya Rodney (1982:243) kama tulivyoeleza katika sura iliyopita.

Uhuru ulipokaribia, kulitokea uhaba wa wasomi watakaoshika hatamu za uongozi. Hawa wakatayarishwa kwa haraka. Mkazo wa elimu ukawa ni kutowa fikra ya ubwana na kufanya kazi ofisini na kujipatia mishahara minono. Jamii ikaamini kuwa elimu ilikuwa ni daraja ya kuukimbia umaskini kwa kujipatia mishahara mikubwa na kupanda tabaka. Ubinafsi ukaendelezwa zaidi kuliko utaifa. Ushirikiano na faida kwa wote haukutiliwa maanani.

S. A. Mohamed, ameonyesha umuhimu wa elimu ya kuwazindua wanajamii. Ameonyesha kuwa elimu kwa vijana ni muhimu kwani ndio viongozi wa kesho na ile potovu inatakiwa itolewe vichwani mwao.

## 4:6 KASUMBA YA KIKOLONI

Ingawa watu wa jamii ya Amezidi sasa wamepata uhuru na wanajitawala, wangali bado na kasumba ya kikoloni ya kuamini kuwa mzungu na yote yanayohusiana naye ni bora kuliko yetu wenyewe.

Kasumba hii ya kikoloni ambayo ilipandwa wakati walipokuwa wanatutawala haikutoweka hata baada ya sisi kupata uhuru wa bendera. Mawazo yao yaliyokuwa yanadhalilisha mtu mweusi na utamaduni wake yaliendelezwa kupitia kwa vyombo kama vile elimu, dini, nyimbo na densi, vyakula, majina na mavazi, miongoni mwa vinginevyo. Ilisemekana kuwa elimu yetu haikuwa nzuri, tukapewa nyingine iliyokuwa na sera ya kuwatumikia na kuwafaidi wakoloni. Kila lililokuwa letu lilidharauliwa, kupezwa na hatimaye kupuuzwa kabisa.

Wakati wa kujinyakulia uhuru ulipofika, watu walirithi elimu ya kizungu, mavazi ya kizungu, dini, densi, vyakula, majina na hata mbinu za kutembea zikawa ni za kizungu. Mambo haya yote yalikuwa yametutayarisha katika kujidharau sisi wenyewe na chochote kilicho chetu. Kwa upande mwingine, tunayakubali yote yatokayo Ulaya na kwingineko hata kama hayana manufaa kwetu. Hali hii ni hali

sawa kabisa ambayo S. A. Mohamed anatusawiria katika tamthilia ya Amezidi.

Ame na Zidi katika ule mchezo wao wa ndotoni wanaamini kuwa fanicha nzuri ni ile itokayo Paris, Ufaransa ingawa kuna mafundi wazuri wa fanicha nchini. Wanatumia maelfu ya pesa za kigeni kuagizia vitu toka Ulaya wakati ambapo wanaweza kuvipata nchini na hivyo kuokoa pesa za kigeni. Isitoshe, kila kitu wanakiagiza kutoka Marekani, Uchina, Japani na Ulaya. Wanafikia hata kuagiza kisu na kiberiti.

Mwafrika anajidharau peke yake kwamba hawezi kuvumbua chochote kwani Wamarekani, Warusi, wafaransa au waingereza wameshavumbua kila kitu. Kwa hivyo hao hawaoni haja ya kujisumbua na fikira za kuvumbua ilihali wenye kufikiria na kuvumbua wapo. Wao wazungu wafikirie, wavumbue na wawauzie nao watalipa tu. Hii ni kejeli au kinaya kwani tujuavyo hali ya nchi ni mbaya hivi kwamba wanastahili kuokoa kila senti itakayohitajika.

Kutokana na mfumo wa elimu wenye mawazo ya kikoloni walioaridhi, viongozi wamekuwa wazembe hivi kwamba hawafanyi kazi ila kutarajia mshahara wa bure. Hii inatokana na ukweli kwamba elimu iliwafunza na kuwatayarisha wafanye kazi ofisini. Kama tulivyoona hapo awali, elimu hii ilitilia mkazo maendeleo ya mtu binafsi kuliko maendeleo ya umma. Matokeo yakawa ni ubinafsi wa mtu kutaka kujiendeleza yeye na familia yake bila kuwajali wanajamii wengine.

Mabosi nao wamo mbioni kuzitengeneza ofisi zao zionekane kama za wazungu na huku pia wakipata asilimia kumi kama kiinua mgongo. Ndivyo ilivyo katika maisha halisi - kila kandarasi itakayopatikana, asilimia kumi humwendea mkubwa. Naye mkubwa huwagawia washiriki wa kundi lake katika maovu haya. Hii ni kasumba ya kikoloni kwamba ofisi ya bosi ni sharti ionekane ikiwa bora zaidi na pia kuwa Bosi ni lazima awe na mali nyingi kupita kiasi. Awe na Mercedes na BMW, fenicha ghali, video na televisheni na mengine mengi ya anasa.

Kwa hakika hakuna haja ya kuipamba ofisi ya bosi huku madawa ya msingi yanakosekana kwenye zahanati na watu wanaendelea kufa kutokana na kipindupindu.

Kwa sababu hawakufunzwa na wakoloni jinsi ya kujitegemea, wanashindwa kuyaendeleza mambo yao wenyewe kwani baada ya kuangusha uchumi wa nchi, wanarudia wale wale waliowatimua ili wawape misaada ya kuwaruzuku. Hii ni sera ya kuwategemea 'mabwana' zao ambao waliondoka lakini wangali wapo kwa vivuli vyao. Wanatumia mali ya taifa vibaya huku wakiwa na mawazo kuwa mabwana zao wa kikoloni wataitwa kuleta misaada wakati wa shida.

Viongozi wengi huyaharibu mambo nchini mwao na kisha kutoa taarifa za uongo ili kuwahadaa watu wa nchi za magharibi, kwa mfano, wakati wananchi wanakufa kwa maelfu katika nchi ya Amezidi, viongozi wanatoa taarifa kuwa haya yamesababishwa na ukame wa miaka mingi. Ukweli ni kwamba wao ndio wamepora mali yote kwa ajili ya anasa zao za kibinafsi. Wanajali sana kile wanachofikiria wale waliokuwa wakoloni na mataifa ya nje kuliko athari na hatari zinazowakumba watu wao. Kwa upande mmoja, hawataki wapate sifa mbaya mbele ya mabwana zao wa kizungu na kwa ule mwingine, wanawadhulumu wananchi wenzao. Ukweli ni kwamba mabwana zao wanayajua haya yote nao hutoa misaada kwa sababu za kibinadamu na pia hutoa vifaa na vitu ambavyo havihitajiki huko kwao.

Kwa hivyo, watu wanaojiita kwamba wana uhuru bado wangali wanatawaliwa na mawazo yaliyowekwa na wakoloni kuwa kila kinachotoka kwao ni chema na cha watu wengine ni kibaya. Elimu inayothaminiwa ni elimu ya "Archimides Priniciple", masofa mazuri ni yale yatokayo Ulaya naye bosi anataka kuipamba ofisi yake ikae kama ile ya wazungu. Wanaharibu mambo yao ya kiuchumi maksudi, mradi tu wazungu wapo na watatoa misaada! Hii ni kasumba ya kikoloni na ni tatizo lililoko katika jamii zinazojitawala na chanzo chake ni mbegu mbaya iliyopendwa na wakoloni ili kutufanya sisi kujidharau na kutukuza kila kilicho chao.

## 4:7 HITIMISHO

Ni maoni yetu kuwa mwandishi ameyadokeza matatizo yanayoikumba jamii kwa uwazi na urahisi zaidi kuliko zile tamthilia mbili zilizotangulia.

Matatizo ya umaskini, ufisadi, kutoajibika kazini, elimu potovu na kasumba ya kikoloni miongoni mwa mengine ni mambo yanayojitokeza na yana uwezekano wa kuwafikia wasomaji na watazamaji wengi kwa urahisi kwa sababu ya lugha nyepesi iliyotumika na mtiririko unaofuatiliza kwa urahisi.

Kipengele cha elimu kwa jamii kimeshughulikiwa kwa undani zaidi kwani tumeonyeshwa matatizo ya mfumo uliopo na jinsi mfumo huu ulivyobadilishwa na wale wanaohusika bila kutegemea watu kutoka kundi jingine waje kuwatengenezea mambo. Kuna matumaini kuwa mfumo huu mpya wa elimu utafanikiwa kwani umelenga vijana ambao ni kundi muhimu katika kuunda jamii ya kesho. Pia wamejihusisha na mageuzi haya wenyewe bila kuletewa mawazo kutoka tabaka la juu.

Jamii ya Amezidi ni jamii iliyogawika katika matabaka mawili, tabaka la juu na lile la chini. Tabaka la juu linaishi kwa anasa na huku likihodhi na kupora mali ya umma. Bosi na msaidizi wake pamoja na mkaguzi wa serikali ni viongozi serikalini wanaoafikiana katika uporaji wa mali ya umma. Katika tabaka la chini, wamo kwenye umaskini, njaa na magonjwa tele.

**TANBIHI**

1. Fugard, A., 1975: The Blood Knot Oxford university Press. Nairobi Kitabu kizima kina wahusika wawili tu Zachary na Morris.

2. Marx, K. , 1963: Early writings, C. A. Watts Co. LTD, LONDON, uk. 81.

3. Nyerere, J. K., 1967: Elimu ya Kujitegemea, Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali; DAR-ES-SALAAM. uk. 1.

4. OGUDE, j. A., 1982: The Emegence of Socialist Realism in Africa Literaure: A Study of Sembene Ousmane, Ngugi wa Thiong'o and Alex Laguma, shahada ya M. A. Chuo kikuu cha NAIROBI. uk..11

5. Ruhumbika, G. 1983: Uwike Usiwike Kutakucha, East African Literature Bureau, ARUSHA. uk..1

6. Marx, K., 1959: Capital, Random House New York uk.. 323.

7. Kama Nambari 3 hapo juu, uk.. 1

## MAREJELEO


1. Fugard, A., 1975: The BloodKnot, Oxford University Press. Nairobi

2. Hussein, E., 1971: Mashetani, Oxford University Press Nairobi

3. Marx, K., 1963: Early Writings, C. A. Watts & Co, ltd, London

   The Communist Manifesto, 1967: Penguin Books: Middle sex.

   Capital, Random House, New York.

4. Mohamed, A. S.1995: Amezidi, East African Educational Publishes, Nairobi.

5. Nyerere, J. 1967: Elimu ya Kujitegemea, mpiga chapa wa serikali, Dar-es-salaam

   1968: Freedom and Socialism Oxford University Press, Nairobi.

7. Rodney, W., 1982: How Europe Underdeveloped Africa Howard University Press, Washington D.C.

7. Ruhumbika, G. 1983; Uwike Usiwike kutakucha east African Literature Bureau, Arusha.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO

Katika sura zilizotangulia, tumekuwa tukitaja na kujadili maudhui mabali mbali yanayojitokeza katika tamthilia tatu za S. A. Mahamed. Katika sura hii hitimisho, tutaona mawazo muhimu yanayojitokeza katika tamthilia zote tatu huku tukitilia maanani nadharia tunayoitumia ya uyakinifu wa kisoshalisti.

Ni muhimu sana mwandishi kuonyesha matatizo yanoyoikumba jamii na kwamba matatizo haya yawe na uhalisia. Yaelezwe kama yalivyo kwa njia sahili. S. A. Mohamed ameeleza matatizo haya katika tamthilia zote na kuonyesha uhalisia wa haya matatizo.

Tatizo la kwanza lililojitokeza wazi wazi katika tamthilia zake ni tatizo la umaskini. Watumishi, walinzi na wale wafuasi wa simba katika Pungwa; wote wanaonyesha umaskini mkubwa, wakulima, waalimu, madaktari, waume na wasichana, katika kivuli kinaishi wanaogelea kwenye bahari ya umaskini. Nao Ame na Zidi katika onyesho la kwanza katika tamthilia ya Amezidi wanaishi katika hali iliyojaa umaskini. Tena umaskini huu wa watu binafsi unaonyesha Ame kudokezea umaskini katika kiwango cha taifa kwani ikiwa wengi katika jamii ndio maskini, basi jamii ile inakuwa ni maskini. Wale wachache hawaleti nafuu kwani wanajifikiria wao wenyewe.

Unyonyaji na Ufisadi ni matatizo yanaenda sambamba na yamejitokeza katika kazi za mwandishi. Kunayo mifano kochokocho katika tamthilia zake kuthibitisha hili. Bwana na Bibiye katika tamthilia ya Pungwa wamechukuwa mali yote na kwenda kuiweka katika mabenki ya Ulaya, wamehodhi nyenzo zote za kuzalisha mali na wanaishi katika maisha ya anasa. Naye Bi Kirembwe na Wazee katika Kivuli kinaishi wameichukuwa mali yote ya taifa na wanaendelea kuitumia katika shughuli zao za anasa za kuchinja mag'ombe, vinywaji na anasa nyinginezo. Walinzi nao wanaendelea kuitisha hongo kutoka kwa wananchi. Na katika tamthilia ya Amezidi.

Bosi na msaidizi wake wanaendelea na njama zao za kuibia umma mali yake kwa kutengeneza nyaraka za uongo, kuchoma zingine na hata ofisi nzima. Wanashirikiana na wakaguzi wa hesabu ili

kuyatekeleza haya. Aidha, viongozi hawa wanapoteza mali nyingi katika sherehe na mikutano isiyo ya muhimu kwa mfano, hakukuwa na haja kualika wageni laki nne na kutumia shilingi milioni arobaini ili kusherehekea siku ya uhuru.

Udhalimu na ukatili ni matatizo mengine yanayozikumba jamii katika michezo hii na pia jamii za Afrika kwa jumla. Katika tamthilia ya Pungwa, Bwana ameamua kuwadididimiza, kuwasagasaga na kuwazika wapinzani wake ama wanaotaka kushindana naye katika shughuli ya ulimbikizaji au wale wasio na chochote lakini wanataka kudai haki zao. Bi kirembwe wa kivuli kinaishi na wazee wake wanatumia ukatili mwingi ili kuwanyamazisha wale walio na sauti ya mwamko ambao wanatofautiana naye kimaoni. Anawaua Mtolewa na wale wazee watatu, na kuwakata mikono mwanaginingi I, II na wa III. Ingawa ukatili na udhalimu huu havijitokezi wazi wazi katika tamthilia ya amezidi kile kitendo cha kuwakemea wafanyakazi na kuwakataza wasitoe maoni yao hadharani ni udhalimu wa kutowapa wafanyakazi na wengine wanaoonewa nafasi ya kujitetea.

Tatizo jingine ni elimu potovu ambayo imewafumba macho walio wengi ili wengi wasitambue shida zao wala kuona chanzo cha shida hizo. Watawala huzua mawazo, itikadi na mfumo wa elimu ambayo haina nafasi ya kuonyesha matatizo halisi, chanzo na suhulisho kwa matatizo hayo. Mwandishi ameshughulikia tatizo hili vilivyo katika tamthilia za kivuli kinaishi na Amezidi kuliko alivyofanya katika Pungwa. Katika tamthilia ya Pungwa, ameonyesha tu Simba akitoa maelezo machache kwa wafuasi wake na zaidi ya hapo, hakuna elimu zaidi inayotolewa. Katika kivuli kinaishi, kuna elimu potovu kupitia kuwatia watu mizuga na kuwapatia unga wa ndere. Mawazo haya ni sharti yabadilishwe.

Uongozi mbaya na kutoajibika kazini ni tatizo linaloimumba jamii yoyote ile ya kiafrika. Bwana na Bibiye hawawajibiki kwa umma. Bi kirembwe na wazee wanatoa uongozi mbaya na wao hawaajibiki kwa majukumu waliyokabidhiwa na umma. Naye Bosi, msaidizi wake, na mkaguzi wa hesabu wameshindwa kutekeleza wajibu wao kwa haki na ukweli.

Hatimaye kuna usaliti ambapo viongozi wameusaliti umma. Badala ya kuutumikia umma kwa uaminifu, hawa viongozi sasa wameugeukia na kuanza kupora mali yake na kuugandamiza badala ya kuulinda. Haya basi ndiyo matatizo anayoyataja na ni maoni yetu kuwa ameielewa jamii anayoandikia

na kutaja mambo mazito na ya kweli kwani hivi ndivyo hali ilivyo katika nchi nyingi za kiafrika.

Mwandishi pia ametafuta chanzo cha matatizo haya. Ameyatambua mambo mawili yaliyosababisha hali hii katika jamii. Ubepari wa ndani na wa nje ndicho chanzo cha matatizo haya yote. Katika uaguzi wa Burhani, kuna mashetani wawili wanaomtaabisha Bwana - wa ndani na wa nje. Yule wa nje ana nguvu zaidi ya yule wa kienyeji. Hali hii ya kulaumu mabepari wa nje inapunguza makali katika tamthilia za kivuli kinaishi na Amezidi. Katika tamthilia hizi, ameona kuwa chanzo ni uongozi mbaya ambao umeusaliti umma na kujitambulisha na mabepari wa nje. Hata zile sababu zinazotolewa na viongozi kama Bi Kirembwe kuwalaumu mabepari wa nje zimekataliwa kwani wakati wa kuwalaumu mabepari huku sisi wenyewe tukisahau kujichunguza umepita. Kihistoria, mwandishi ameonyesha kuwa matatizo haya yalianza na ubepari ulioanza na kuzaa ukoloni na ukoloni ukazaa ukoloni mamboleo - yote yakawa na lengo moja: la kudumisha ubepari ule ule.

Kuna umuhimu wa kuonyesha matabaka yaliyomo katika jamii, historia ya matabaka hayo, mitafaruku na mikinzano yake pamoja na kujitambulisha na tabaka moja, hasa lile la wengi na wanaonyanyaswa. Matabaka yaliyotambuliwa na mwandishi ni mawili kama ilivyo hali halisi afrika. Hapa Afrika hatuna tabaka la tatu ambalo ni tabaka la kati kama ilivyo huko Ulaya. Kule Ulaya kuna tabaka la juu, kati na chini lakini hapa ni lile la juu na chini. Lile la kati halipo. Bwana na bibiye wa Pungwa, Bi Kirembwe na wazee katika kuvuli kinaishi, Bosi na msaidizi wake pamoja na mkaguzi katika Amezidi wote wanawakilisha tabaka la juu. Nao watumishi, walinzi na jeshi la simba wa Pungwa, wakulima, madaktari, walimu, wari na wasichana katika kivuli kinaishi na Ame na Zidi katika onyesho la kwanza wote wanawakilisha tabaka la chini la wale wanaonyanyaswa. Mikinzano na mitafuruku imeonyeshwa kihistoria kuanzia Mahoka hadi Burhani na hatimaye Simba katika tamthiliya ya Pungwa. Katika kivuli kinaishi mitafuruku hii inawashirikisha wakulima, waalimu, madaktari, wari na wasichana kwa upande mmoja na Bi kirembwe na wazee kwa upande mwingine. Mitafaruku hii imekuweko tangu uhuru kupatikana na watu kugundua kuwa haukuwaletea nafuu. Bosi na wafanyakazi wake kule ofisini wanapingana hata kama hawapatii ruhusa ya kusema chochote au kuuliza swali lolote. Kwa hivyo mitafuruku na mikinzano imekuweko, iko na itaendelea kuweka mradi unyonyaji upo na matabaka yapo katika jamii.

Mwandishi amejitambulisha na wanyonge na wale wanaonyanyaswa. Amewasuta wale wa tabaka la juu na kuwashutumu bali amewatetea wale wa tabaka la chini na kuonyesha kuwa wanao uwezo wa kubadilisha mambo. Simba na kikosi chake, Ame na Zidi, na Wari, wasichana na wafanya kazi ndio wanaendelea na mapambano ya kuleta mageuzi.

Elimu na itikadi kwa wanajamii wanaogandamizwa ni kiungo muhimu na kama tulivyoona, S. A. Mohamed ameonyesha umuhimu huu katika tamthilia zote ingawaje amelimulika zaidi katika tamthilia mbili za mwisho kuliko alivyofanya katika tamthilia ya Pungwa. Simba anawaelimisha watoto, mtolewa anawaelimisha wari nao wafanyakazi wanao mwamko wa kisiasa. Katika harakati hizi za kuelimisha, elimu potovu inawekwa wazi na kutupiliwa mbali na ile yenye manufaa kuanzishwa. Kwa mfano katika tamthilia ya Amezidi, wanafunzi na waalimu wao wanaukataa ule mfumo wa awali wa elimu na kuanza kujifunza ule unaoambatana na kuingiliana na mahitaji yao ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Nayo itikadi ya mwandishi imejitokeza wazi katika kazi hizi. Kugeuzwa kwa wafanyikazi na wanyonge wengine kimawazo ni jambo lililofanywa maksudi na tabaka la juu ili lipate nafasi ya kunyonya kwa urahisi. Sasa mwandishi amependekeza elimu mpya itolewe ili kuwazindua wanajamii. Anaamini kuwa mabadiliko ya wanyonge yataletwa na wanyonge wenyewe ingawa hafungii nje makundi mengine yenye mawazo ya kizalendo kama vile Mtolewa, wazee na Simba, miongoni mwa wengine. Aidha, anayo imani na vijana na itikadi yake kuhusu hili ni kuwa maisha au harakati ambazo haziwahusishi vijana ni kama kutayarisha wazee ili waende kushiriki kwenye mashindano ya mbio miaka ijayo.

Mitafaruku ya matabaka ina nia ya kuleta mapinduzi. Badala ya kungojea na kutegemea wakati ulete mabadiliko, walio wengi wameulizwa wajiingize katika kutekeleza kwani wanaweza kuchangia ili yaje haraka badala ya kuendelea kusubiri.

Mapinduzi ni jambo ambalo limejitokeza katika kila tamthilia. Katika tamthilia ya Pungwa, amependekeza kutumiwe silaha ili kuleta mabadiliko katika jamii. Simba na askari wake ndio wanaotumia silaha kuleta mapinduzi na makundi mengine yanaungana nao baadaye, mapinduzi yale yanatokea kwa ghafla kutokana na mapendekezo ya Engeles kuwa yanaendelea chini kwa chini kabla ya kulipuka kwa ghafla. Katika kivuli kinaishi na Amezidi hatuyaoni haya mapinduzi yakitokea ingawa

harakati zinaendelea. Hali ya kuleta haya mapinduzi imeandailiwa ingawa mapinduzi haya hayasisitizi utumiaji wa silaha kama alivyofanya katika tamthilia ya Pungwa. Hapa anashauri kutumiwe maasi ya kutoajibika na kutotii sheria za wanyonyaji. Haya ni mabadiliko makubwa kwa mwandishi kwani yanatokea katika tamthilia zote mbili za mwisho.

Mabadiliko haya ni dhihirisho kuwa imani ya mwandishi katika utumiaji silaha ili kuleta mapinduzi imepunguza makali na hasa hapa Afrika. Pia ikumbukwe kwamba wakati akiandika tamthilia za kivuli kinaishi (1990) na Amezidi (1995), mabadiliko yalikuwa yameanza kutokea ulimwenguni na siasa ya ukomunisti kuwachwa katika nchi za Ulaya ya Mashariki. Huku kwetu Afrika, utawala wa chama kimoja ulikuwa umeanza kuporomoka moja baada ya nyingine na demokrasia ya vyama vingi kuanzishwa. Hili pamoja na ukweli kwamba mapinduzi mengi ya silaha hayafanikiwi kuleta mabadiliko ya kweli, lilimfanya aubadilishe msimamo wake kuhusu mapinduzi yanayojiri kwa kutumia silaha.

Uundaji wa jamii mpya yenye haki na usawa ni jambo lililotiliwa mkazo katika kazi hizi tatu. Askari wa Simba, watumishi pamoja na walinzi wamefaulu kutaifisha mali ya mabepari inayowakilishwa na Bwana na Bibiye katika Pungwa. Wanakula matunda pamoja na wote kutumia sofa pamoja na ukweli kuwa sasa wote ni sawa na hakuna anayejichukulia kama kiongozi. Katika kivuli kinaishi; tunadokezewa kuwa sasa hali ya kuleta haki na usawa imeanzishwa kwani kivuli cha wale walioanzisha shughuli hii bado kinaendelea. Zile sauti nyingi zinatufahamisha;

**SAUTI NYINGI**: Sisi ni vizazi vipya vya Griningi,
Vizazi vya walioangamia ..........................
Vizazi vya waliodidimia ............................
Sisi sasa tuna kinywa kipana....................
Tuna uwezo wa kuamua tunavyotaka........
Kuamua wenyewe ......Kwa maslahi ya sote.......(uk. 128).

Huu ni ushahidi tosha kuwa jamii ya kesho ni jamii ya haki na usawa, jamii ya ujamaa. Na katika Amezidi, tunafahamishwa kupitia ule wimbo (uk. 91) kuwa wananchi sasa wamesimama nguvu moja, wako tayari kuzibeba nafsi zao wenyewe na hatima yao sasa watajia mria wenyewe.

Maoni yetu ni kuwa mwandishi amefaulu katika kuwasilisha maswala muhimu yanayozikumba nchi nyingi za kiafrika. Ameonyesha matatizo, chanzo cha matatizo hayo, namna kuyatatua matatizo hayo na kuunda jamii mpya yenye haki na usawa. Hata hivyo tasnifu yetu itakuwa haijakamilika iwapo hatutaonyesha ufanisi wa mwandishi kama mwanatamthilia kwani hii ndiyo mara yake ya kwanza kujitokeza katika uwanja huu. Ni matumaini yetu kuwa wahakiki wengine watalifuatilia swala hili la S. A. Mohamed kama mwandishi wa tamthilia na pia kushughulikia kipengele cha fani kwa undani zaidi.

Mwandishi autumia utangulizi ambapo ametoa yale mawazo muhimu yatakayotawala mchezo mzima. Katika tamthilia ya Pungwa, ametumia wimbo katika ile sauti ya mzuka, sehemu aliyoiita chanzio. Katika Amezidi, ametumia mbinu hii ya wimbo kama utangulizi wake na kuuita wimbo wa Mzee, sehemu hii anaiita kianzio. Mbinu hii ilipendekezwa na Aristotle naye S. A. Mohamed ameitumia.

Mtiririko wa hadithi katika tamthilia zake tunaweza kusema kuwa ni sahili. Ni maoni yetu kuwa alifanya hivyo maksudi. Kutokana na ukweli kuwa aliandikia jamii nzima na wala si wasomi peke yao. Hili ni muhimu kwani mwandishi hutakiwa ailewe jamii anayoiandikia hasa kiwango cha elimu. Isitoshe, kule kutumia imani za kiafrika kama kupungwa, dhana ya giningi na kutawishwa kwa wari kunafanya kazi hii ijitambulishe zaidi na bara la Afrika kwani mila hizi zimesambaa sehemu nyingi sana, lakini pia hiki kinaweza kuwa kizuizi kwa wale ambao si waswahili hasa na ambao imani kama hizi hazipatikani kule kwao.

Mwandishi ametumia lugha ya kishairi ili asiwachoshe watazamaji na pia kutoa mawazo mazito kuifikia hadhira. Hili pia lilikuwa pendekezo la Aristotle. Kama kuna kipengele ambacho amekithibiti mwandishi ni utumiaji wa lugha ya ushairi. Ameamua kuitumia lugha hii kwenye mawazo mazito kama ya viongozi au kutoa jambo zito kama vile wimbo unaozungumzia ubepari.

Wahusika wameteuliwa kwa ustadi na wengi wao wamepewa majina ya kimajazi kama vile Mtolewa kuonyesha vile jamii ilimtoa katika mapambano kama sadaka ya kuikomboa jamii. Kibwege, Kijuha, Mahoka, Amezidi, Bwana na Bibiye, Simba na Burhani yote ni majina ya majazi yanayowakilisha wazo au tendo fulani katika jamii.

Hadhira nayo imehusishwa na mwandishi kama anavyopendekeza Bretcht. Anatoa mapendekezo kuwa hadhira isilishwe papai kwa kijiko bali ipewe nafasi ya kushiriki katika machezo, wafikiri au watafakari badala ya kukaa tu na kustareheshwa. Hata ikiwezekana, waweze kutoa uamuzi wao wenyewe.

Urefu wa tamthilia kama vile kivuli kinaishi unaweza kutatiza kwani ni Mrefu mno kama mchezo wa kuigiza. Inaonekana alijaribu kumwiga Shakespear ambaye aliandika michezo mirefu mirefu bila ya kutambua kuwa michezo ya Shakespear ilikuwa na muundo wa kuwa na vilele (upeo) kadhaa katika mchezo mmoja.

Aidha, ametumia maneno mengi sana katika mhusika mmoja. Kwa mfano, Bi Kirembwe anatoa taarifa ndefu ndefu ambazo zitawatatiza waigizaji pamoja na ukweli kwamba haya yatazuia kueleweka kwa maudhui.

Kwa vile tasnifu hii haijihusishi na mtindo, tungelipenda kuhitimisha kwa kusema kuwa, mbali na upungufu wa hapa na pale wa mtindo, maudhui yake ni mazito na yenye umuhimu kwa jamii. Maudhui haya yameelezwa kwa kutumia uyakinifu wa kisoshalisti kuliko hata ilivokuwa katika riwaya zake. Hii ni kwa sababu ameonyesha matatizo, chanzo chake, elimu kwa wanajamii wote wakiwemo vijana. Ameonyesha matabaka, mitafaruku na mikinzao yake, harakati za ukombozi na jamii mpya. Ni maoni yetu kuwa amefaulu kimaudhui na tutanufaika iwapo mhakiki mwingine atajitokeza na kuhakiki mtindo wake kuona kufaulu au kutofaulu kwake katika kipengele hiki.

## MAREJELEO


Beard na Verma, 1981: Katika Judith, B. (Mhariri) "Doing your research project" A guide for First Time Research in Education and Social Sciences. Milton Keynes, Philadephia University Press, Philadephia.

Brecht, B. , 1964: Brecht in Theatre (Kilitafsiriwa na Willet, J.) Shen Vat Press, London.

Engels, F. 1979: Katika Howe, I., (Mhariri), A handbook of Socialist thought, Howe & Brydone (Printers) Ltd, London.

Fanon, F., 1967: The Wretched of the Earth, Penguin Books, Middlesex.

Fokema, D.W., 1977: Theories of Literature in the Twenth Century, C. Hurst & Co., London.

Fugard, A., 1975 The Blood Knot, Oxford University Press.

Gitahi, G., 1980 The Development of a Writer's Social Perspective: An Assessment of Ngugi Wa thiong'o's Selected Texts, M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Gorky, M., Hakuna Mwaka: On Literature, Progress Public Publishers, Moscow

Hussein, E., 1971: Mashetani, Oxford University Press, Nairobi.

\- 1983: "Hatua Mbali Mbali za Kubuni na Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle" Katika Fasihi III, Makala za Semina, Dar-es-Salaam.

Marx, K., 1959: Capital, Eastern M., (Mhariri), Random House, New York.

\- 1963: Early Writings, C.A. Watts & Co. Ltd, London.

Miriji, T., 1991: Mtindo Katika Pungwa ni Hatua Katika Kuwazilisha Ujumbe, B.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi, Kitivo Cha Elimu, Kikuyu.

Mlama, P.O., 1983: "Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya Tanzania" Katika Fasihi III Makala za Semina, Dar-es-Salaam

Mohamed, S.A., 1978: Asali Chungu, Longman Publishers, Nairobi.

- 1980: Sikate Tamaa, Longman Publishers, Nairobi.
- 1980: Utengano, Longman, Nairobi.
- 1988: Pungwa, Longman Kenya Ltd, Nairobi.
- 1990: "Ulimwengu wa Mwandishi wa Kiswahili Kilugha" Katika Mbatiah, M. (Mhariri), Mwamko Nambari Tatu.
- 1990: Kivuli Kinaishi, Oxford University Press, Nairobi.
- 1995: Amezidi, East African Education Publishers, Nairobi.

Ngara, E., 1985: Art and Ideology in the African Novel, Heinman, Nairobi.

Ngugi wa Thiong'o, 1986: "Writing Against Neo-Colonialism" Katika Kristen, H., (Mhariri), Criticism and Ideology, Second African Writers Conference, Bohslangen, Stockholm.

Nyerere, J.K., 1967: Elimu ya Kujitegemea, Mpiga Chapa wa Serikali, Dar-es-Salaam.

- 1968: Freedom and Socialism, Oxford University Press, Nairobi.

Rodney, W., 1982: How Europe Underdeveloped Africa, Howard University Press, Washington D.C.

Ruhumbkika, G., 1983: Uwike Usiwike Kutakucha, East African Literature Bureau,

Arusha.

Suchkov, B., 1969: "Realism and its Historical Development" Katika Prof. S., Mozhnyagen (Mhariri) Problems of Modern Aesthetics, Moscow.

Styan, J.L., 1960: The Elements of Drama, Cambridge University Press, Cambridge.

Trotsky, L., 1971: Literature and Revolution, The University of Michigan Press, U.S.A.